ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Saba - Tarehe 01 Disemba, 2016

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na kwa idhini yako naomba kuweka mezani hoja kuhusu Matokeo Hatarishi katika Sekta ya Uwekezaji wa Viwanda. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 135

Lengo la Kuanzishwa Kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

Mhe. Omar Seif Abeid: (Kny. Mhe. Said Omar Said) - Aliuliza:-

Katika hali ya ubora na upatikanaji wa haki kwenye eneo la kuendesha kesi, Serikali imeunda Idara ya Mwendesha Mashtaka. Idara hii ndiyo yenye mamlaka ya kuamua kuwa kesi fulani ipelekwe Mahakamani au hapana.

Je, wananchi wanajua chombo cha kutoa haki ni Mahakama na Hakimu ndiye mwenye uwezo wa kutoa haki. Je, kitendo cha kuweka chombo chenye uwezo wa kuzuia dai au kesi kutofikishwa Mahakamani ni hali ya Utawala Bora.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 135 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali imeunda Idara ya Mwendesha Mashtaka ili kuimarisha ubora wa upatikanaji wa haki na Utawala Bora hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilianzishwa mwezi Julai, 2002 baada ya mabadiliko ya Nane ya Katiba ya Zanzibar 1984, ambapo afisi hii ilipewa jukumu katika kifungu 56A cha Katiba, la kuendesha mashtaka katika Mahakama za Zanzibar isipokuwa za kijeshi. Pia katika kutekeleza majukumu yake afisi hii ipo huru na hailazimiki kufuata maelekezo ya mtu au mamlaka yoyote.

Kwa hivyo, kuanzishwa kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kumeimarisha Utawala Bora, kwa sababu Afisi hii inawawakilisha wananchi wa Zanzibar na serikali yao, katika kuwasilisha ukweli kwenye Mahakama zetu kwa kufuata misingi ya Utawala wa Sheria.

Miongoni mwa majukumu ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni kuratibu upelelezi ili kuhakikisha ushahidi uliokusanywa unakidhi vigezo vya kisheria, kwa kuwasilisha ushahidi huo Mahakamani ili iweze kutoa haki kwa mwenye kustahiki.

Aidha, kuwepo kwa afisi hii kunasaidia sana kupunguza uwezekano wa watu kubambikiziwa kesi kutoka kwa watu wenye mamlaka au wanaotumia vibaya madaraka na nguvu ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa wito kwa jamii kwa ujumla kuwa iwe tayari kutoa ushahidi, ili kuthibitisha kesi zilizopo Mahakamani na kuimarisha utoaji wa haki.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kumuuliza swali moja dogo la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na mrundikano wa mafaili mengi katika vituo vya polisi Unguja na Pemba, kunakoaminika kwamba ucheleweshaji wa kesi unatokana na Idara hii ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali.

Je, kuna utaratibu gani unaochukuliwa na Idara ya Mahakama au wana mipango gani watu wa Idara ya Mwendesha Mashtaka, kuhakikisha kwamba kesi zote au mrundikano wa mafaili yaliopo polisi yanafika kwao kwa wakati, na wao

wanayapeleka Mahakamani, ili kuondoa mrundikano na malalamiko ya wananchi, kwamba wanacheleweshewa kesi zao na hazifiki Mahakamani. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote ni kwamba sikubaliani na mawazo ya Mhe. Mwakilishi, kwamba kuwepo kwa mafaili mengi Mahakamani kunasababishwa na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka. Isipokuwa Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kuna sababu mbali mbali ambazo zinasababisha suala kama hilo.

Kwa mfano, suala la wananchi kutokuwa tayari au kuwa na muhali kwenda Mahakamani kutoa ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti, hali hii inapotokea wananchi pale ambapo wanapotakiwa kutoa ushahidi Mahakamani huwa wanakataa, na kukataa kwao huwa ni sababu miongoni mwa sababu ambazo zinasababisha kesi kutokwenda kwa kasi. Kwa sababu kama tujuavyo kwamba katika jamii yetu kuna baadhi ya wananchi kesi zao huwa wanazimalizia huko huko vichochoroni, kitu ambacho sio sahihi wakati kesi tayari Ofisi ya Mwendesha Mashtaka imeshapeleka kesi ile Mahakamani, na Mahakama ili iweze kutoa haki inatakikana kwamba mashahidi wahudhurie Mahakamani. Kwa hivyo, kutokwenda kwa mashahidi Mahakamani, hiyo ni miongoni mwa sababu ambayo inapelekea kesi zile kuzorota.

Mhe. Mwenyekiti, kuna sababu mbali mbali ukiachia hiyo, sababu nyengine wakati mwengine zile dharura za wale ambao wanasimamia kesi zile. Wakati mwengine wale ambao wanasimamia kesi za waendesha mashtaka huwa wanakuwa na dharura, kwa maana kwamba inawezekana siku ile kesi ile inaendesha Mahakama moja, lakini wakati mwengine inawezekana wamepangiwa Mahakama nyengine. Kwa hivyo, hii huchukua fursa hii ya kuiomba Mahakama ile kesi yake isisomwe kwa siku ile isomwe siku nyengine. Kwa hivyo, hii vile vile ni sababu ambayo huwa inasababisha kesi kuzorota.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna suala zima la washtakiwa wale ambao wanapewa dhamana, wakati mwengine huwa wanatoroka zile dhamana. Sasa mshtakiwa anapotoroka zile dhamana ile kesi huwa inasitasita kwenda, sasa kwa sababu mshtakiwa mwenyewe hayupo sio rahisi kwamba siku moja au mbili kesi ile kufutwa, lakini Mahakama kama Mahakama inakuwa inatoa muda maalumu ili kuhakikisha kwamba yule mshtakiwa anapelekwa pale Mahakamani. Kwa hivyo, kukawia kupelekwa kwa yule mshtakiwa Mahakamani vile vile na suala hili linapelekea kuzorota kwa kesi Mahakakani.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Mwenyekiti, kuna kesi ambazo zipo Mahakamani na kesi hizo huwa zinapangiwa tarehe, na mashahidi kila siku ya kesi wanakwenda, lakini cha kusikitisha kesi hizo hazizungumzwi na Mahakimu siku ya kesi hizo ndio siku ambazo kuwa wanapata vikao.

Je, Mhe. Mwenyekiti, kesi kama hizi ambazo ziko Mahakamani kwa muda wa mwaka mmoja sasa hivi na kesi hizo kila siku zinaahirishwa zinapofika Mahakamani. Je, Mhe. Naibu Waziri wizara yako ina mkakati gani wa kuzishughulikia kesi kama hizi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kumjulisha Mhe. Mwenyekiti, kwamba kuwepo kwa vikao vya Mahakimu sio sababu ya hizo kesi kucheleweshwa. Kama nilivyojibu katika jibu langu la awali la nyongeza, kwamba sababu ambazo zinazochelewesha kuendeshwa hizi kesi pamoja na mambo mengine ni mashahidi. Kwa hivyo, utakapoona kwamba kesi inachukua muda mrefu, basi usimtafute mchawi, mchawi ni wale mashahidi kutofika kule Mahakamani, lakini mashahidi kama wanafika Mahakamani bila shaka hapana wasi wasi wowote kesi hiyo itaendeshwa kwa haraka zaidi ili kufikia hatua ya mwisho. Kwa hivyo, unapoona kesi Mahakamani zinacheleweshwa, basi ujue kwamba miongoni mwa sababu nyengine ni pamoja na hao mashahidi, mashahidi wanakuwa hawako tayari kutoa ushirikiano na Mahakama. Ahsante.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ya msingi kabisa. Lakini katika majibu yake na hoja iliyokuwepo katika swali la msingi ni ucheleweshwaji wa kesi kupitia Ofisi ya *DPP*, kwa maana mafaili pale yanakaa sana. Sasa katika kupima *performance* ya utekelezaji wa hili labda Mhe. Naibu Waziri anijibu tu, ofisi yake inapokea wastani kwa mwezi mafaili mangapi na mangapi wanayashughulikia katika kumaliza ushauri na kupelekwa Mahakamani au kupelekwa mbele au kurudi katika utaratibu wa utekelezaji wa kazi zake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nikiri kwamba swali la Mhe. Mwakilishi linataka zaidi uchunguzi, utafiti na kwa mantiki ya kwamba linahitaji *details* za kutosha.

Sasa swali la kuniuliza ni mafaili mangapi kwa mwezi. Kwa ujumla inawezekana mwezi huu ukapokea 20, kwa mfano mwezi unaokuja ukapokea 25.

Mhe. Mwenyekiti, lakini zaidi nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba napenda nikujibu swali hili kwa maandishi, na ningependa kujibu angalau kwa miaka mitano, kwa sababu ukiniambia kwa mwaka inawezekana sijui ni *gape* kubwa ni miaka mingi, lakini labda nikupe kwa miaka mitano hii tuliyokuwanayo ni mafaili mangapi tunapokea kwa mwezi. Ahsante.

Nam. 121

Utaratibu wa Kutunza na Kuviendeleza Vivutio vya Watalii Katika Msitu wa Jozani na Ngezi

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Zanzibar ina misitu mikubwa ambayo kwa Unguja ni Jozani na kwa Pemba ni Ngezi, na misitu hiyo imekuwa na vivutio mbali mbali kama vile wanyama mbali mbali, makaburi ya zamani na ya asili ya maimamu, ambayo wananchi huyatumia kwa kufanya maombi juu ya matatizo au maradhi mbali mbali, lakini kwa bahati mbaya vivutio hivyo havitangazwi kwa wageni na hata wenyeji wa Zanzibar.

(a) Je, Msitu wa Jozani na Ngezi una vivutio vya aina ngapi na vivutio gani.

(b) Je, serikali ina mpango gani wa kuwapandikiza wanyama waliomo kwenye misitu hiyo ili kuwaenzi na kuweka hadhari ya kupotea kwa rasilimali hiyo ama kwa maradhi au matatizo mengine.

(c) Je, Serikali inafaidika na mapato yanayotokana na makaburi hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye rehema ambaye ametupa pumzi zake na kuwepo hapa leo.

Baada ya shukrani hii sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 121 lenye kipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inakiri kuwepo kwa vivutio mbali mbali vinavyogawika katika aina kuu 8 ambazo ni wanyama, miti, wanadamu. Samahani Mhe. Mwenyekiti.

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inakiri kuwepo kwa vivutio mbali mbali vinavyogawika katika aina kuu 8 ambazo ni wanyama, miti adimu na misitu mikuu, makaburi na mabaki ya viwanda vya historia, ukanda wa bahari, vipepeo, aina za ndege, jamii ya nyoka na maisha ya pamoja kwa wanyama, miti na binadamu na kadhalika.

(b) Mhe. Mwenyekiti, napenda kutanabahisha kwamba serikali kuwapandikiza, kuwaenzi na kuwalinda wanyama, wizara yangu imefuatilia kwa kina suala hili kwa watendaji wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika kuhifadhi Msitu wa Jozani na ule wa Ngezi ulioko kisiwani Pemba. Kwa hivyo, tumebaini kuwa hadhari ya kupotea kwa rasiliamli hiyo, inaweza kuwa ni changamoto kwa wizara yangu katika kuimarisha vivutio vya utalii wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ni muhimu kwanza kufanya *survey* ya tabia ya wanyama wenyewe, maeneo waliopo na eneo tunalotaka kuwapeleka.

Mhe. Mwenyekiti, ni vizuri kufanya *survey* hiyo kwa sababu wanyama waliomo ni adimu na ni vyema wakawa wanatafutiwa eneo jengine ikitokezea kupungua au kupotea kwa eneo moja, basi wawe wanapatikana kwenye eneo jengine, kama ilivyofanyika kwa Paa Nunga. Umuhimu mkubwa ni mkazo wa kufanya ufuatiliaji.

(c) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu faida na mapato yanayopatikana kutokana na makaburi yaliomo kwenye maeneo hayo ni kwamba mara nyingi vivutio hivyo vya kihistoria vinakuwa ni moja ya sehemu mjumuiko wa kuyatembelea au kuyatalii maeneo hayo, kwa hivyo hakuna makusanyo maalumu yanayopatikana kutokana na makaburi ya historia pekee. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru Mhe. Waziri wa Habari kwa majibu yake lakini pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Katika swali langu Mhe. Waziri nilimwambia kwamba nilikuwa nahitaji vivutio vilivyopo kule Jozani na Ngezi, sikutaka katika vivutio ambavyo Idara ya Habari ina vivutio vyote, maana yake kuna vivutio vingi vyengine hata kaburi la Mwanamwari pia hakulitaja, lakini nilikuwa nazungumzia vile vivutio vilivyomo zaidi mule ndani, amenitajia watu, amenitajia upande wa bahari, ametaja mengi lakini sawa acha tuachane huko.

Ni lini utafiti huu ambao uliusema kwamba wa wanyama ambao nilizungumza kwa sababu tuna misitu yetu miwili tu ambayo inajulikana kimataifa, hasa kati ya Ngezi na Jozani, kwa hivyo sisi wanyama wetu wakipotea tutakuwa hatuna pa kukimbilia. Wewe ulizungumza kwamba utatafuta eneo la kuweza kuwatega au kuwaweka pindipo patakapotokea matatizo haya.

Lakini mimi ningeshauri kwamba kwa kuzungumza uwazi, ni lini utafiti wako utafanyika kwa ajili ya wanyama hawa ili kuweka hakiba ya eneo moja watakapopata matatizo eneo la pili tukawapata.

La pili nataka niongeze kwa kusema kwamba Zanzibar na Pemba kuna tofauti ya hali ya hewa gani na kuna matatizo gani ya kwamba kasoro ambazo zinaweza kujitokeza mpaka leo wanyama hawa hawajafanyiwa utafiti wa kuwa katika eneo ambalo litakuwa salama.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi kataka kujua kwamba ni lini tutafanya utafiti wa wanyama hawa. Naomba nimjibu kwamba utafiti huu tayari unaendelea kufanywa na ndio maana katika swali mama nikamwambia kuna Paa Nungu hawa wamefanyiwa utafiti na kuonekana wanaanza kupotea, kwa hivyo wamewekwa sehemu maalumu na sasa hivi pale tunapotaka kuwaona, na mimi hili niombe tu Waheshimiwa Wawakilishi tuwe tunafanya utalii wa ndani tukishirikisha familia zetu, twende kuona vile vivutio au wale wanyama katika sehemu tulizowahifadhi ili kuona historia ya nchi yetu na vivutio vyake.
Mhe. Mwenyekiti la pili naomba kidogo arejee swali lake sikulisikia.

Mhe. Mweyekiti: Mhe. Suleiman rudia swali lako.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa namuuliza kuna ugumu gani au kuna ukubwa gani wa kufanya utafiti huo kwa wanyama wetu waliopo Unguja na Pemba, kwa sababu hali ya hewa ya Unguja na hali ya hewa ya Pemba takriban yote ni moja, kwa hivyo nilikuwa nazungumzia suala kama hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Kama nilivyomwambia kwamba huu utafiti unafanywa na wanyama tumeweka pamoja na mfano kama msitu wa Ngezi kuna Kimapunju sasa hivi ambao walionekana kule Pemba wamepotea hawapo, tayari wapo katika msitu ule wamehifadhiwa, wamewekwa katika sehemu maalumu na wanyama hawa sasa hivi wanapatikana katika msitu ule.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kama alivyozungumzia Mhe. Waziri kuhusu kimapunju ambao wapo kwenye msitu wa Ngezi, lakini mimi kama mwenye Jimbo ambaye ni mwenyeji wa pale napenda kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika huu msitu wa Ngezi kulikuwa na wanyama hao kimapunju unaowazungumza Mhe. Waziri, kwarara, popo wa Pemba, paa, vihodi na vipepeo ambapo kwa sasa wanyama hawa ni ukweli usiofichika kwamba wamepotea kwa asilimia kubwa. Je, Wizara yako kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo ambao ndio wanaoumiliki ule msitu wa Ngezi, wana mpango gani wa makusudi wa kuwarejesha wanyama hao wote na kuwahifadhi ili kiendelee kuwa kivutio kwa watalii na kurejesha haiba ya ule msitu wa Ngezi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Kama nilivyosema kwamba katika msitu huu wa Ngezi, na nakiri kwamba wanyama hawa walikuwepo wengi na kama alivyosema kwamba wameanza kupotea, lakini naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba kama nilivyomwambia kwamba hawa kimapunju walikuwa hawapo katika ule msitu, sasa hivi wapo hawa kima mimi nimjibu tu kwamba nimefanya *survey* nimekwenda kule kwa kushirikiana na watendaji wa Wizara ya Kilimo, na hawa kima wapo.

Lakini niseme tu kama kuna wanyama ambao wameanza kupungua pia naungana na yeye kwamba tutaendelea kufanya hii *survey* na kuhakikisha kwamba wanyama hawa wanapatikana katika sehemu ile, ili iwe kivutio zaidi kwa watalii wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana aliyoyajibu, nataka kuongezea mambo yafuatayo. Kwanza hawa wanyama wana tabia moja hasa kimapunju, ukichanganya na kima wengine kuna tabia ya kuwindana kila mmoja ana mazingira yake ya kuishi, jambo moja ambalo tumejifunza tuliwapeleka kwa mfano msitu wa Ngezi kuna kima ambao tumewazoea kila siku hawapatani kabisa na kima hawa, kwa hivyo kuna kuwindana katika hilo, hilo la kwanza.

La pili ni suala la chakula vile vile kila mmoja ana *taste* yake ya chakula, hawa wameshazoea ndizi ndizi pale wanavuna kila kitu, kwenye msitu ule kama hakipo chakula kile wanaathirika hilo ni jambo moja ambalo linaathiri.

Jengine ni wawindaji. Watu wetu vile vile hawawezi kuzitunza hizi rasilimali ambazo tunazo, kwa mfano paa unakuta pahala pengine watu wanakwenda kuwawinda nje ya utaratibu wanapungua, kwa hivyo ni jambo ambalo linahitaji kila mmoja wetu kwanza aelewe mazingira ya hawa wanyama tunapowapeleka na maana ya Serikali ni kwamba wanataka kuukuza utalii ila mnyama kila pahala aonekane tunahitaji kutoa msaada wa ziada.

Jengine ni suala zima la kuwinda kiharamu nalo limeathiri sana uhai wa hawa wanyama katika misitu yetu mikubwa tuliyonayo.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali jengine la nyongeza.

Mhe. Waziri unasema katika Wizara yako una vivutio vingi vya utalii, katika jimbo langu la Ziwani kuna magofu ya Mkumbuu Shehia ya Ndagoni, katika magofu yale yapo makaburi likiwemo kaburi la mwanamwari, lakini pia vile vile walikuwepo popo wengi wale wa Pemba, popo wale hivi sasa wameshaanza kutoweka. Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuwarudisha popo wale ili lile eneo la utalii, kwa sababu watalii walikuwa wakivutika zaidi na wale popo, lakini popo wengi wameshatoweka. Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba popo wale wanarudi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Kama alivyosema Mhe. Waziri wa Kilimo hapa hawa wanyama ambao wanakuwepo katika sehemu zetu na ikawa ni vivutio zaidi kwa watalii wetu, wanahitaji kutunzwa na pia mazingira nayo yanahitajika kuangaliwa kutokana na hali ya hewa zetu na jamii yetu ilivyo. Kwanza niseme sisi wananchi pia tunahitajika kutunza vivutio hivi na utalii wenyewe ili tuvutie mapato kwa Serikali.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mwakilishi tushirikiane pamoja, hawa popo wanachi wetu tuwape elimu kwamba wasiwahujumu ili wawepo katika mazingira mazuri pale wanapokuja watalii iwe ni vivutio zaidi na wao wavutike watalii wetu.

Nam. 79

Upungufu wa Walimu wa *Arts* Katika Jimbo la Mtopepo

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi - Aliuliza:

Uwepo wa walimu wa Sayansi ni muhimu sana na naipongeza Wizara kwa kufanya bidii za makusudi za kutatua upungufu wa walimu hao katika skuli zetu, na kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa walimu wa masomo ya *Arts* katika skuli mbali mbali.

Na kwa kuwa katika Jimbo la Mtopepo kuna upungufu mkubwa wa walimu hao katika skuli ya Mtopepo na Kidatu juu, wakati wapo vijana wengi waliomaliza masomo yao ya ualimu kwa viwango vya Shahada, Stashahada na Cheti ambao hawajaajiriwa.

(a) Je, kuna mpango gani uliopangwa kwa lengo la kutatua tatizo hili katika skuli zetu.

(b) Wizara ina mpango gani wa kuwaajiri vijana hao ili wazibe pengo la upungufu wa walimu katika Jimbo la Mtopepo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi swali lake Nam. 79 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mhe. Mwakilishi kwa kuziona juhudi zetu katika kulitatua tatizo la upungufu wa Walimu wa masomo ya Sayansi, na Hesabati katika skuli zetu. Pia, Wizara inaelewa kuwa wapo vijana wengi waliohitimu masomo ya ualimu kuanzia ngazi ya cheti hadi shahada ya kwanza ambao hadi sasa hawajaajiriwa. Kwa vile wahitimu ni wengi, utaratibu wa ajira unategemea kuwepo kwa idadi ya nafasi tupu na waombaji wenye sifa na mshahara. Kwa bahati mbaya, idadi ya wahitimu wa mafunzo ya ualimu ni wengi kuliko mahitaji halisi na hivyo haitowezekana kuajiriwa wahitimu wote katika skuli za Serikali kwa sasa. Kwa hivi sasa mahitaji makubwa ya walimu ni kwa masomo ya sayansi na Hesabati.

Kwa upande wa mahitaji ya walimu wa masomo ya Sanaa, upungufu uliopo sio mkubwa kama inavyodhaniwa. Katika ziara tulizofanya hivi karibuni katika skuli 27 za Mkoa wa Mjini/ Magharibi tumegundua kuwa katika baadhi ya skuli, walimu wengi wa masomo ya sanaa wana vipindi vichache vya kufundisha kwa wastani ni vipindi 16 hadi 20 kwa wiki.Wizara itafanya uhamisho wa baadhi ya walimu hao na kuwapangia kazi katika baadhi ya skuli zenye upungufu wa walimu wa masomo ya sanaa zikiwemo Skuli za Jimbo la Mtopepo. Hata hivyo, napenda nikiri kuwa baadhi ya skuli zenye upungufu wa walimu wa masomo ya sanaa wenye sifa za kufundisha masomo ya Historia, Lugha ya Kiingereza na Jiografia.

Uchunguzi tulioufanya katika skuli ya Mtopepo, tumebaini kuwa skuli hiyo ina upungufu wa walimu wawili tu wa masomo ya lugha. Tayari mwalimu mmoja ameshahamishiwa katika skuli hiyo na kuwaahidi mwalimu mwengine atapelekwa kabla ya kuanza mwaka wa masomo 2017.

Kwa upande wa Skuli ya Mtoni Kidato juu, skulli hiyo haina upungufu wa walimu wa masomo ya sanaa bali ina upungufu wa walimu wa masomo ya Sayansi na Hesabati. Wizara itafanya utaratibu wa kuipatia skuli hiyo walimu wa masomo ya Sayansi mara tu taratibu za ajira za walimu wapya zitakapokamilika. Baada ya maelezo hayo, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Wizara inakusudia kuajiri walimu kwa awamu kulingana na mahitaji na upatikanaji wa fedha. Katika awamu ya kwanza Wizara inatarajia kuwaajiri walimu 106 waliohitimu Stashahada na shahada ya Ualimu katika masomo ya Sayansi na Hesabati. Walimu hawa watagawiwa katika skuli zenye upungufu mkubwa katika Wilaya zote za Unguja na Pemba.

(b) Wizara tayari imeshampeleka mwalimu mmoja wa somo la Sanaa katika skuli ya Mtopepo na mwalimu mwengine atahamishiwa katika skuli hiyo kabla ya kuanza kwa mwaka wa masomo wa 2017. Pia, mara tu taratibu za uajiri zitakapokamilika Skuli ya Mtoni Kidato Juu itapatiwa mgao wa walimu wa masomo ya Sayansi.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mhe. Waziri. Pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza tunajua kwamba Jimbo la Mtopepo lina vijana wengi sana wanahitaji nafasi katika skuli mbili tu ziliopo hapo jimboni, yaani

Skuli ya Mtopepo na Skuli ya Kidatu Juu, sasa kutokana na upungufu huu wazee wengi wanapeleka wanafunzi wao nje ya skuli ya Mtopepo.

1. Sasa nauliza Mhe. Waziri kuna mpango gani wa kuongeza madarasa katika skuli hizi mbili za Mtopepo na Kidatu Juu.

2. Ningependa nijue utaratibu wa kuweka fensi katika ile skuli ya Kidatu Juu, kwa sababu kuna uvamizi wa baadhi ya watu pale katika eneo la skuli.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

1) Ni kweli tunaelewa kwamba Skuli nyingi zina upungufu wa madarasa, lakini sera yetu katika Wizara ya Elimu inaendelea kuwepo ile ile ya kuwahamasisha wazazi, wafadhili na wengineo kusaidia kujenga madarasa mpaka hatua fulani, ikifika hatua hiyo wizara itasaidia kukamilisha jengo, kwa hivyo tunawahimiza wananchi waendelee kusaidia katika kuhifadhi.

Lakini hata hivyo uchunguzi mwengine tuliofanya tumegundua kuwa baadhi ya sehemu wazee hawana uwezo wa kufanya hivyo, sehemu hizo kwa kweli Wizara huzisaidia, lakini kwanza naamini wananchi waJimbo la Mtopepo wanao uwezo wa kufanya hivyo, tuendelee kufanya hivyo na hatimaye Wizara itakamilisha.

2) Suala la kuweka uzio tulizungumza kwamba bado ni suala la kieneo, kwa hivyo tunahamasisha vile vile wananchi kuchangia katika sehemu hizi za kuhifadhi eneo la skuli kwa njia mbali mbali, michango ya wananchi, michango ya viongozi, michango ya Wawakilishi, michango ya Wabunge na wahisani wengineo. Lakini katika mtizamo mkubwa wa kiwizara bado hatujawa na mpango huo mpaka sasa.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo lilioko katika Jimbo la Mtopepo linafanana na lile tatizo lilioko katika Jimbo la Kiwani hususan Skuli ya Mwambe, na kwa kuwa mwaka huu wameandikishwa watoto wa darasa la kwanza wasiopungua 600, na kwa kuwa hapo nyuma tatizo la walimu lipo, na kwa vile wameshaandikishwa watoto wengi litakuwepo wengi zaidi. Je, namuuliza Mhe.

Waziri Wizara yake ina mpango gani wa dharura ili kupeleka walimu Skuli ya Muwambe kutokana na wingi wa watoto walioandikishwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, Wizara inaelewa kwamba skuli ya Muwambe ina upungufu wa walimu na hadhari iliyopo kwamba labda wataandikisha wanafunzi wengi zaidi. Wizara itachukua hatua za dharura ili kuona inapeleka walimu katika skuli ya Muwambe wakati mwaka mpya wa masomo utakapoanza. Hatua hizi zinatokana na baadhi ya fursa za ajira ambazo wizara imeshapata hadi sasa. Katika walimu ambao wataajiriwa hivi karibuni tunakusudia Januari wataanza kufanya kazi basi baadhi tutawapeleka Skuli ya Muwambe.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema awali kwamba tumejaribu kufanya tathmini ya idadi halisi ya walimu waliokuwepo maskuli tukaona kwamba baadhi ya Skuli walimu wapo wengi zaidi, na kwa hivyo tuliwahamisha Skuli hizo na hiyo haitofanyika Unguja tu pia mpaka Pemba, na tayari tumeshamuagiza Afisa Mdhamini Pemba afanye tathmini ya idadi ya walimu kuweza kuhamishwa na kupelekwa sehemu nyengine pale ambapo walimu hawatimizi idadi ya vipindi vinavyotakiwa, basi tafsiri yake ni kwamba katika skuli hiyo walimu ni wengi, kwa hivyo wahamishwe katika sehemu nyengine. Kwa hivyo namuhakikishia Mheshimiwa kwamba skuli yake itafaidika na zoezi hili la kuhamisha walimu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine. Ahsante.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ya msingi na ya nyongeza aliyojibu muda mfupi uliopita.

Mhe. Mwenyekiti, Skuli ya Sekondari ya Makunduchi inachukua wanafunzi kutoka Skuli za Miwaleni, Kiongoni, Kajengwa wanajumuika pale katika madarasa ya Sekondari. Kwenye vyombo vya habari hivi karibuni inasemekana mwalimu mkuu anasema Skuli hii ina upungufu mkubwa sana wa walimu wa *physics*, *biology*, *chemistry*, kiasi ya kwamba inatisha hali hiyo, na mwezi Januari mwakani skuli itapokea wanafunzi wengi kutoka skuli hizo.

a) Je, Mhe. Waziri tatizo la uhaba wa walimu wa masomo haya linaeleweka na wizara yako.

b) Ni hatua gani za dharura zinazoweza kuchukuliwa na Wizara yako ili kulipunguza tatizo hili ili mwezi Januari walimu hao wapatikane,

nasema za dharura kwa sababu katika majibu uliwahi kusema kwamba upo mpango wa kuwaajiri walimu, lakini hili ni la dharura.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli skuli za Makunduchi kama zilivyo skuli nyengine zina upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi ikiwemo *physics*, *biology*, *chemistry*, suala hili linaeleweka sio kwa ajili ya skuli ya Makunduchi Sekondari lakini pia kwa ajili ya skuli nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, ili kukabiliana na suala hili katika hatua za dharura mbali na uajiri wa awamu ya mwanzo ambao utakamilika Januari mwakani, pia serikali sasa hivi imetueleza kwamba tutaajiri na wengine 170 walimu wa sayansi katika kipindi hichi. Kwa hiyo katika ajira hiyo itakapokamilika nadhani kwamba tatizo hili litapungua kidogo, hiyo itakuwa ni awamu ya pili, ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri na Mafunzo ya Amali nimuulize kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli serikali kwa nia njema imeanzisha mfumo mzuri wa sayansi na *arts* ambao mfumo huu zamani haukuwepo au ulikuwepo baada ya kuanzia darasa la 12 kwenda mbele ndio watu walikuwa wanaendelea, lakini serikali mpaka sasa hivi suala la sayansi inakuwa ni suala tata kwa walimu pamoja na mfumo mzima hasa unapoonekana kwamba mfumo wenyewe unapoweza kumuuliza mtoto kuanzia darasa hilo la form II mpaka form IV, hata *laboratory* yake au mwalimu hujawahi kusikia hata kupasua chura, hata kufanya jambo lolote zaidi ya masomo kama yatakuwepo.

a) Swali langu kwamba, je, serikali kama ilikuwa bado katika mfumo wake wa sayansi bado haijakamilisha si bora wangerudia mfumo wa zamani kwanza wakaachia wanafunzi ili kupata nafasi ya kuweza kujiweka sawa mpaka hapo nafasi za *arts* na sayansi ambazo zikawa za uhakika ikawa zina nafasi yake kwa kumuanzisha mwanafunzi.

b) Mhe. Mwenyekiti, taaluma ya wenzetu walianzisha suala la *arts* na suala la sayansi wao wanaanzisha kwa sababu wanafunzi wao pale wanapowabaini kwamba ana uwezo wa *arts* fulani wanaanza kumsomesha ile *arts* ile ili muda mdogo wa miaka 20 anakuwa ameshakuwa profesa, sisi bado mpaka sasa hivi *arts* yetu ni ya kumsomesha anakwenda nayo bila ya malengo...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa uliza swali.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Swali langu ni kwamba mfumo wa zamani, je, ulikuwa una kasoro gani zilizofanya kwamba mfumo wa *arts* wa sasa hivi uchukue nafasi yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Wizara ya Elimu imeshajipanga vya kutosha katika kuendeleza elimu ya sayansi. Hii inatokana na kuwepo walimu wenye sifa za juu kabisa za kusomesha walimu wa sayansi. Lakini pia kutokana na baadhi ya vitendea kazi vilivyopo, kasoro ambazo alizitaja Mheshimiwa kwamba labda wanashindwa kufanya mazoezi ya vitendo, kwamba hata pengine kupasua vyura, ni matatizo ya mbinu za usomeshaji tu, lakini vifaa vingi vya kufanyia mazoezi ya vitendo vinapatikana katika mazingira halisi.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo lililokuwepo ni lile ambalo katika taaluma tunasema kwamba walimu wengi wanashindwa kutumia mazingira yake na akafundishia. Lakini niseme kwamba ili kukabiliana na suala hili na ndio maana serikali ikaanzisha Chuo Kikuu chake cha Taifa *SUZA* pamoja na masuala mengine kuweza kuzalisha walimu wa sayansi na hili kwa kiasi fulani tumefanikiwa, kwa hivyo serikali ipo tayari kuendeleza sayansi na hatuwezi kukaa kando tukasema kwamba hatutaki kuendeleza sayansi, tutapitwa na tutakuwepo nyuma. Wataalamu wetu mbali mbali tulikuwa nao Zanzibar ambao wapo katika fani mbali mbali tunazozijua hao wametokana na mfumo huu ambao Mheshimiwa Mwakilishi anauona labda una kasoro. Madaktari waliopo wengi wamepitia mfumo huo huo, wahandisi waliopo wamepitia mfumo huo huo, wataalamu wetu wa kilimo wamepitia mfumo huo huo. Kwa hivyo sisi tunauona kwamba hauna kasoro na ndio maana tumeweza kupata wataalamu wetu mbali mbali kiasi kwamba sasa hivi tumeshindwa kuwaajiri kutokana na wengi wao na wanaajiriwa katika nchi nyengine duniani hao hao wa sayansi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sikubaliani na Mwakilishi kwamba labda mfumo wetu uko chini, kwa hivyo tusubiri tuutayarishe mpaka utakapofika. Mfumo wetu uko imara na uko juu zaidi.

Kuhusu mfumo je, kuna kasoro gani hapa. Siku zote elimu inabadilika na ndio elimu kama haibadiliki basi hiyo itakuwa sio elimu, kwa hiyo mabadiliko ya mazingira ya sasa ndiyo yaliyotufanya kwamba katika hatua fulani tuweze kutenganisha vipaji vya wanafunzi wetu wale wenye muelekeo wa sayansi tunawaendeleza katika sayansi na wale wenye muelekeo wa *arts* tunawaendeleza katika *arts,* na katika viwango vikubwa zaidi kuliko hiyo zamani ambayo anasema Mwakilishi, leo watu wanasoma mpaka viwango vya

Shahada ya kwanza na ya tatu, hapo zamani wachache kabisa waliokuwa wakiweza kusoma katika fani hizo na kiwango hicho.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa kuna taarifa muhimu, taarifa ya kupima afya, wataalamu wa kupima afya kwa maradhi yasiyoambukiza wamefika leo kwenye Ofisi yetu ya Baraza wanakusudia kuwapima afya zao Wajumbe na kutoa ushauri. Vipimo watakavyopima ni uzito, shindikizo la damu (BP) na sukari. Wataalamu hao wapo ukumbi wa juu na Waheshimiwa Wajumbe wanaombwa kwenda kuwaona. Kwa vile shughuli zetu zinaendelea humu ukumbini, basi tujitahidi kwenda mmoja mmoja au kwa utaratibu ambao hautaathiri shughuli zetu za Baraza, na baada ya kumaliza urejee katika sehemu yako ili tuweze kuendelea na shughuli za Baraza, ahsante.

Nam. 114

Uajiri wa Mabibi na Mabwana Shamba

Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Aliuliza:-

Tatizo la mabibi shamba na mabwana shamba limechukua muda, na tukiangalia tuna vijana ambao wameshasomea fani au taaluma hii ya bibi shamba na bwana shamba lakini mpaka leo hii vijana hao hawajapatiwa ajira.

Je, Mhe. Waziri Wizara yako ina mpango gani wa kuwaajiri vijana hawa ili kuondosha kero ambazo zinawafika wakulima wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 114 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, wizara baada ya kuona upo upungufu wa kuajiri vijana wanaomaliza mafunzo ya kilimo na mifugo, kwanza inawashajiisha wale wanaohitimu mafunzo kuweza kuitumia taaluma yao kwa kuanzisha mashamba yao kwa lengo la kujitengenezea ajira na kuwa mfano kwa wakulima kuweza kujifunza.

Aidha, Wizara inaendelea kutoa taaluma kupitia mabibi shamba na mabwana shamba katika Wilaya na kuweka mfumo wa zoni kama Pemba ambao unasaidia kuwafikia wakulima kwa urahisi zaidi na pale nafasi zitakapotakikana, basi Wizara itaendelea kuwaajiri wataalamu hao.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

a) Mhe. Waziri kwa kawaida hawa mabibi shamba na mabwana shamba huwa wanatakiwa kufanya kazi katika shehia ngapi. Kwa sababu kuna mabibi shamba na mabwana shamba wanafanya kazi katika shehia kuanzia moja mpaka tatu na bibi shamba hawa tayari wameshakuwa wazee.

b) Je, Mhe. Naibu Waziri kuna usafiri wowote ambao mumewapatia hawa mabibi shamba na mabwana shamba ili kuweza kuwafikia wakulima kwa wakati.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza ametaka kujua bwana shamba anahudumia Shehia ngapi.

a) Bwana shamba wa Pemba anahudumia shehia kuanzia mbili mpaka tatu na kwa Unguja anahudumia shehia moja mpaka mbili.

b) Vile vile katika suala la kipando tumewapatia wale ambao ni wakuu wa zoni wanawasaidia wale mabwana shamba anapotaka kwenda katika shehia zake ambazo zile anazihudumia anakwenda na kile kipando anamchukua na kwenda katika ile shehia ambayo anayohudumia.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri wa Kilimo linalohusiana na muktadha wa wanafunzi wa Chuo cha Kilimo Kizimbani hususan mabwana shamba na mabibi shamba.

Katika majibu ya swali mama Mhe. Waziri alisema kwamba wanawashajihisha wahitimu hawa katika suala zima la kuweza kujiajiri au kuitumia taaluma yao bila ya kutegemea uajiri wa serikali.

a) Je, katika Chuo chetu cha Kilimo somo la ujasiriamali litaweza kufundishwa lini ili umfanye kijana aweze kujiajiri bila ya kutegemea serikali, ni lazima umpe somo la ujasiriamali.

b) Chuo kina utaratibu gani wa kuweza kuwafuatilia wahitimu ili kuwaona kwamba kile walichojifunza wanakitumia katika mazingira yao, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, Chuo mpaka sasa hakina somo hili la ujasiriamali. Lakini ujasiriamali ingawa unasomeshwa unapopewa ile taaluma lazima uitumie sehemu ile husika. Ujasiriamali utakuja endapo utatumia yale uliyosomeshwa masomo ya kilimo na mifugo, lakini unaweza ukatumika nyumbani kuna vishamba vidogo vidogo ukatumia ule utaalamu wako ambao umesomeshwa kule chuoni.

Vile vile Mhe. Mwakilishi, nikuahidi kwamba nitashirikiana na Mkuu wa Chuo ili kumshauri ikiwezekana tuweke somo hili la ujasiriamali.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa.

Mhe. Mwenyekiti, kama unavyofahamu asilimia 73 mpaka 75 ya Wazanzibari hapa wapo katika shughuli za ujasiriamali, wamepata taaluma mbali mbali za nyumbani na kadhalika. Ujasiriamali ni shughuli ambazo mtu anajishulisha kufanya shughuli zake na kujizalishia yeye mwenyewe. Sasa ile taaluma ni ile *professionalism*, kwamba unapata taaluma maalumu kwa ajili ya kufanya shughuli maalumu. Taaluma hiyo inatolewa pale chuoni na wanaipata.

Pili, niseme kwamba tunawafuatilia hawa ambao wamepata taaluma, juzi tulikuwa na ndugu zetu kutoka *Fujian University of China* walikuja wakawafunza vijana wetu 50 ambao tayari wapo katika ujasiriamali, wakapata taaluma ya ziada katika sekta ya uvuvi.

Kwa hivyo Chuo kinafuatilia na sisi kama Wizara tunafuatilia, na tunawaunganisha na taasisi mbali mbali waweze kujiendeleza katika shughuli zao.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba mabwana shamba na mabibi shamba wamepatiwa usafiri. Mimi nikiomba kujua tu ni mabwana shamba wangapi na mabibi shamba wangapi wamepatiwa usafiri na ni usafiri wa aina gani ambao wamepatiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, katika jibu langu nimesema Wakuu wa *zone* ndio ambao

wamepatiwa usafiri. Wakuu wa *zone* wanapokwenda katika Shehia wanamchukua yule Bwanashamba na kwenda katika Shehia yake kwa ajili ya usimamizi. Wakuu wa zoni ndio wanaosimamia mabwana na mabibi shamba.

Nam. 131

Kuanza kwa Kilimo cha Umwagiliaji Bonde la Mlemele

Mhe. Shaib Said Ali - Aliuliza:-

Bonde la Mlemele liliopo Jimbo la Chonga na Chambani limo katika mpango wa kilimo cha umwagiliaji zaidi ya miaka 10 sasa, lakini hadi leo hii hakuna hatua inayoendelezwa kutoka bonde hilo.

(a) Je, kuna mpango gani wa kuliendeleza bonde hili ili wananchi wapate mavuno mazuri.

(b) Je, ni sababu gani zilizopelekea bonde hilo lisiendelezwe hadi leo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo,Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Shaib Said Ali wa Jimbo la Chonga swali lake Nam. 131 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, bonde la Mlemele ni miongoni mwa mabonde yaliyoingia katika mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji Zanzibar kupitia mkopo wa *Exim Bank* Korea, ambapo hekta 61 za bonde hilo zitaendelezwa kwa kuwekwa miundombinu ya umwagiliaji maji na wakulima wataweza kulima misimu miwili kwa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji maji Zanzibar ni miradi inayosimamiwa na Wizara na ufadhili wake unatokana na mkopo kutoka Benki ya *Exim* ya Korea. Fedha hizo za mkopo zilikisiwa kuwa ni Dola za Kimarekani milioni hamsini (*USD* 50,000,000) ambazo ziligaiwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ilikuwa ni ya mshauri elekezi ambaye atasanifu michoro, kutengeneza kabrasha la zabuni na kusimamia ujenzi wa miundombinu hiyo, kazi ambayo ilishakamilika kwa asilimia sitini ambapo asilimia iliyobakia ni kusimamia ujenzi tu kazi ambayo inasubiri kukamilika kwa zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

Mhe. Mwenyekiti, awamu ya pili ya matumizi ya fedha hizo za mkopo ililengwa kutumika kwa ajili ya kazi za ujenzi wa miundombinu hiyo ya umwagiliaji maji Unguja na Pemba likiwemo bonde la Mlemele. Zabuni ya kumpata Mkandarasi wa kazi hiyo ili kupambana na changamoto. Miongoni mwa changamoto zilizojitokeza katika zabuni hiyo ni kama ifuatavyo:-

1. Kukosekana kwa ushindani katika mchakato wa zabuni hali hii ilitokana na kuwasilishwa kwa zabuni moja tu; jambo ambalo linakwenda kinyume na Sheria ya Manunuzi ya Umma Zanzibar Nam. 9 ya mwaka 2005.

2. Zabuni iliyowasilishwa katika kipengele cha fedha *(financial proposal)* ilikuwa na kiwango kikubwa sana cha fedha ambazo ni Dola za kimarekani milioni sitini (*USD* 60,000,000) ukilinganisha na fedha zilizotengwa ambazo ni dola za Kimarekani milioni arobaini na sita (*USD* 46,000,000).

3. Kujitokeza kwa mapungufu kwenye kabrasha la zabuni lililotayarishwa na mshauri elekezi kwenye vipengele vya kufanya tathmini ya zabuni hiyo. Jambo ambalo lilimuwezesha mzabuni huyo kupita kwenye eneo la kiufundi licha ya kuwa wataalamu wake aliowapendekeza hawakuwa na uzoefu katika kufanya kazi kwenye miundombinu ya umwagiliaji maji.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya changamoto hizo napenda kumuelewesha Mhe. Mwakilishi kwamba azma ya kuliendeleza bonde la Mlemele ipo pale pale na utekelezaji wake utaanza mara tu baada ya kumpata mkandarasi wa ujenzi.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, bonde hili la Mlemele sasa hivi mradi huu ni wa muda mrefu sana, kiasi ambacho wananchi wa Jimbo la Chambani na Chonga wameshakata tamaa kutokana na bonde hili. Moja kati ya dhima ya Serikali ni kupunguza uagiziaji wa mchele na wananchi kupata chakula chao kwa bei nafuu sana. Je, kama azma hii bado Serikali ipo, kuna mikakati gani ya makusudi kuliendeleza bonde hili ili azma hii ya Serikali ipatikane.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mkakati wa Serikali upo pale pale kutekeleza azma yake ilani ya Chama cha Mapinduzi kama ilivyosema kwamba inataka kutekeleza au kuimarisha mabonde haya eka 1621, kwa hiyo azma yake iko pale pale

tunaomba wananchi wako wawe na subra pamoja na wewe mwenyewe ili tuweze kumpata mkandarasi tuendelee na mradi huu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba tuwatambue wageni wetu katika ukumbi wetu huu wa leo japokuwa ni wageni wa Mhe. Mohammed Said Mohammed maarufu Dimwa Jimbo la Mpendae wakiongozwa na ndugu Ranavi Shah ambao ni kama wafuatao:-

Ndugu Ranavi Shah
Ndugu Adam Zakaria
Ndugu Luchi Seif
Ndugu Baskar Ramaiya

Karibuni sana.

Pia vile vile kuna tangazo jengine hapa kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari Mhe. Ali Sulaiman Ali maarufu Shihata. Anawatangazia wajumbe wa Kamati wakutane katika chumba namba 3 juu mara baada ya kuahirishwa kikao cha Baraza. Ahsanteni.

Tangazo jengine linalofuata ni, kuna kamati ambazo zimepata mualiko wa kuhudhuria semina kutoka *ZRB* ambayo ilikuwa ifanyike tarehe 3 Disemba, katika ukumbi wa *Ocean View* sasa imebadilika, itafanyika katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi hapo juu. Muda na saa ni ile ile, isipokuwa Kamati zenyewe ni kama hizi zifuatazo.

Kamati ya *PAC*, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Ahsanteni.

Nam. 133

Kuwasaidia Wananchi Wasiharibu Mazingira

Mhe. Shaib Said Ali - Aliuliza:-

Moja kati ya uchafuzi na uharibifu kwa mazingira ni uchimbaji wa mawe, mchanga na ukataji wa miti ovyo, suala ambalo limejitokeza sana katika ukanda wa pwani wa mashariki ya kisiwa cha Pemba.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hao ili wasiendelee kuchafua na kuharibu mazingira bila ya kuwaathiri wanachi hao kimaisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Shaib Said Ali wa Jimbo la Chonga swali lake Nam. 133 kama ifuatavyo:-

Kwanza kabla ya kumjibu naomba niungane na Mhe. Mwakilishi kuwa masuala ya uchimbaji wa mawe, mchanga na ukataji wa miti ovyo ni mambo ambayo yanapelekea uharibifu wa mazingira. Hata hivyo, maisha yetu ya kila siku yanahitaji matumizi ya maliasili zenye uhai kwa maana zile ambazo zinarejesheka na zisizokuwa na uhai ambazo hazirejesheki. Kwa mnasaba huo ni wazi kuwa ili tuendelee kuwa na maisha bora basi ni lazima tutumie maliasili hizo kwa ajili ya shughuli mbali mbali kama vile za kilimo, viwanda, usafiri na shughuli nyengine za kujikimu kimaisha.

Mhe. Mwenyekiti, jambo muhimu la kuzingatia ni kuwa tunapotumia maliasili hizo basi tufikirie pia kizazi kijacho nacho pia kinahitaji kutumia maliasili hizo hizo kwa maisha yao. Hivyo suala la matumizi bora na endelevu la maliasili hizo wenye kufuata utaratibu wa Kisheria uliopo wa matumizi ya maliasili hizo ni jambo ambalo linapaswa kuzingatiwa na kutekelezwa na kila mtu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mara zote imekuwa inachukua juhudi kubwa za kuwasaidia wananchi wake ili waweze kujikimu kimaisha na wasiendelee kuchafua na kuharibu mazingira. Kupitia sekta mbali mbali za kilimo, mifugo na uwezeshaji, Serikali imekuwa ikiwapatia vifaa mbadala vya uvuvi, mifugo na imekuwa ikiwahamasisha wananchi kujiunga kwenye vikundi vya ushirika ili kutumia fursa ziliopo za misaada ya kiuchumi.

Mhe. Spika, hivi karibuni Wizara yangu imesaidia miradi ya mbogamboga vikundi vya Maziwani, Wingwi, Kubulunzi, Maziwani kwa fumo, Mnyonyoni Wilaya ya Wete. Aidha, pia imetoa msaada wa mizinga ya nyuki kwa vikundi vya Tundauwa, Ole, Tumbe, Sizini, Vitongoji, Uwandani, Wambaa na Mwambe.

Aidha, Serikali itaendelea kutoa misaada ya kujikimu kimaisha kadri hali itakavyoruhusu ambayo haina athari ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira hasa katika ukanda wa Pwani wa Mashariki ya Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo tu la nyongeza. Je, Mhe. Waziri ana mpango gani wa kuyafukia mashimo yaliyoko ambayo sasa hivi imekuwa hatari kwa wanyama na binadamu katika ukanda huu wa mashariki ya kisiwa cha Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, suala alilosema ni zuri lakini kwanza tuyabaini yote na halafu huo mkakati wa kuendelea kuwafikia uendelee. Lakini nisisitize sana kwa pamoja tutafanikiwa. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti naelewa mazingira ni uhai wa kila kitu na bila ya kuwa na mazingira salama ni hatari kwa maisha ya binadamu wetu na wanyama na kadhalika. Kwa kuwa eneo la Kwarara kwa Ngulangwa kuna kadhia kama hii ya kuchimba mchanga usiku na mchana kweupe, lakini Idara ya Mazingira taarifa huwa wanazo baadhi ya wakati wakipigiwa simu na wananchi wema au raia wema huwa hawachukui hatua za kuwafuatilia watu hao. Je, Wizara kupitia maeneo haya ambayo yana nguzo zetu kuu za umeme mkuu kutoka nje ambao tunaoutegemea kwa nchi nzima, na nguzo hizo zishaanza kuchimbwa hivi sasa, Wizara ina mpango gani wa makusudi kufanya doria na kuwachukulia hatua wananchi hawa wako mchana bila kujificha.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Wizara kupitia Idara ya Mazingira inafanya doria ya kuwabaini na kuwakamata waharibifu hawa wa mazingira. Lakini kama ulivyosema kwamba mazingira yanatuhusu sote na hawa wahalifu wanatumia akili sana kuvisoma hivi vikosi vyetu kazi. Lakini sheria yetu ya nchi inaruhusu kwamba raia mwema pia kumkamata muhalifu, tunaomba sana mutusaidie kwa hili wakamatwe na taarifa tupeane ili sheria ichukue mkondo wake. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nami ninashukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu amesema kwamba wanafanya doria kupitia Idara ya Mazingira, lakini kila kukicha mazingira yanaharibiwa kwa makusudi, hususan mikoko. Hata juzi tulipokuwa na ziara ya Mhe. Balozi, tulikuta maeneo ya Tingatinga

mikoko mingi imekatwa na imekusanywa kwa kwenda kujenga. Je, ni watu wangapi katika hizo doria wamekamatwa na wamehukumiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa vile swali lake ni la takwimu hapa sinazo naomba nimjibu kwa maandishi lakini nakubaliana naye kwamba kuna waharibifu wa mazingira, hivyo nitoe wito tena sote waheshimiwa Wawakilishi na wananchi, raia wema, tuwaambie kwamba sote kwa pamoja tuwe walinzi wa mazingira yetu. Ahsante sana.

Nam. 52

Kuondoka kwa Mwekezaji Mpapindi *Holiday and Dibing Company*

(Mheshimiwa Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 120

Udhibiti wa Serikali katika Biashara

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Serikali imeamua kuwa biashara nyingi kuwapa wafanya biashara binafsi ili wawe ndio waendeshaji.

(a) Je, Serikali ilifanya utafiti wa kina kuangalia athari za maamuzi hayo kimapato na kiusalama.

(b) Je, kwa nini Serikali imekaa na kusubiri mapato kutoka kwa walipa kodi na kuacha vyanzo vya mapato ya kibiashara hasa kwa zile biashara ambazo zinawahusu wananchi moja kwa moja.

(c) Je, Serikali imejipanga vipi kuziba pengo hili kabla ya kutokea madhara.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan swali lake Nam. 120 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, ilihodhi biashara zote muhimu kwa nia ya kuhakikisha kuwa wananchi wa Zanzibar wanapata mahitaji yao muhimu bila ya matatizo yoyote. Hali hiyo iliendelea mpaka pale ilipoona kuwa wananchi wa Zanzibar wanaweza kuhimili kufanya kazi hizo za biashara ndipo ikaanza polepole kuiachia sekta binafsi kujihusisha na biashara. Serikali ilifanya utafiti wa kina na kuweka sera, sheria na kanuni za kusimamia uendeshaji wa biashara katika soko huria kwa kuruhusu ushindani halali pamoja na kumlinda mtumiaji wa bidhaa katika uwanja wa biashara huru, pia Serikali imeweka sheria na kanuni za kusimamia kodi na mapato ya serikali. Kwa hivyo ikaamua kuiachia sekta binafsi kujihusisha na biashara.

Kwa upande wake Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikukaa na kusubiri mapato tu, bali inaimarisha na kuyasimamia mazingira mazuri ya biashara pamoja na kukusanya mapato kwa ufanisi ili kuendeleza utoaji wa huduma mbali mbali kwa wananchi. Kwa juhudi hizo Serikali imejipanga na kufuatilia kwa umakini kabisa kusitokee madhara yoyote.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru Mhe. Waziri amenijibu vizuri isipokuwa kuna maswali ya nyongeza. Nafahamu Mhe. Mwenyekiti, waziri amesema kuwa Serikali ilifanya naweza kusema kwamba utafiti wa kina kuhusu masuala hayo ya biashara kwa kuweza kuwagaia sehemu wananchi wake ili kuendeleza biashara hizo. Lakini nataka nimwambie Waziri kwamba kwa mfumo huo ambao zamani ulikuwa unatumiaka na sasa hivi ni kwamba nchi yetu imeingiwa na utashi mkubwa wa kisiasa. Baadhi ya wafanyabiashara hasa wakubwa wengine wameingia na utashi ule ule wa kisiasa na wanajaribu kufanya kila hali kuwatonya wanachama baadhi yao wasiweze kupata vifaa ili wananchi wale waweze kuilaani Serikali kwamba vitu hivi hapana, kitu hichi hapana.

Sasa Serikali imeliangalia hilo kwamba bado ina dhima ya kuhakikisha wananchi wake wanapata kila kile ambacho wanahitaji na wakati huo Serikali imetegemea wafanya biashara hao pengine si waaminifu. Hilo ni swali (a).

Swali la pili pamoja na kunijibu kwamba Serikali imeachia hivyo, lakini nataka nimwambie Mhe. Waziri ni kwamba kukusanya kodi ni suala jengine lakini la pili pia kuna suala la mambo ya ulinzi. Nchi yetu kama tunavyoiona ina milango mingi ya ulinzi. Sasa baadhi ya nchi nyingi huwa kuna maeneo ambayo biashara zake haziruhusu kutiwa mkono na wafanyabiashara. Je, Wizara ya Biashara imeshafanya utafiti wa kwamba biashara gani inaweza ikawa ni tatizo kwa wafanyabiashara waliokuwa si waaminifu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kuhusu suala la wafanyabiashara waliokuwa si waaminifu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwa kusema kwamba kwa kipindi cha karibuni, kumeonekana wafanyabiashara ambao si waaminifu sio wazalendo. Kwa sababu walikuwa wanafanya biashara lakini vile vile walitumia masuala ya kisiasa kuwaadhibu wananchi ambao walikuwa hawana hatia. Na kipindi kilichotokea mambo haya tulichukua hatua zinazofaa.

Kwanza kuna wafanyabiashara leseni zao zilifungiwa na kuna wafanyabiashara wengine walipewa maonyo, kwa hivyo si jambo zuri kwa kweli kwamba mfanyabiashara kwa sababu umepewa leseni ya kufanya biashara ukaanza kutumia leseni ile kuwaadhibisha wananchi ambao hawana hatia, tumeyaona na serikali iliyachukulia hatua. Lakini niseme tu kwamba hatutarajii tena mambo haya kufanywa kipindi kinachokuja, serikali itarekebisha sheria kuona sheria gani nyengine mbadala tutazichukua kwa ajili ya kuwadhibiti hawa wafanyabiashara ambao wanahatarisha maisha ya wananchi wetu.

Kuhusu swali la pili ni biashara gani ambazo serikali inadhibiti kusema kwamba hizi ni biashara ambazo serikali inatakiwa izidhibiti.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wakati mwengine serikali inaangalia maeneo gani ambayo haya wakiachiwa wafanyabiashara ambao hawana uzalendo wanaweza kuleta athari kwa wananchi, na ndio maana ukaona biashara kama zile zina vivutio. Mpaka sasa hivi naweza nikasema mfano ambao biashara iliyodhibitiwa na serikali mpaka sasa hivi ni suala zima la umeme, bado umeme unadhibitiwa na serikali. Lakini tungefikiria kama umeme ungelikuwa umepewa kwa wafanyabiashara ambao sio wazalendo basi sehemu nyingi ya Zanzibar tungekuwa hatuna umeme, mfano tu natoa.

Pia biashara nyengine ambayo kwa upande mmoja ni huduma na biashara ni suala zima la usambazaji wa maji, unajua nchi nyengine maji ni biashara, kwa hiyo wanaachiwa watu binafsi tu wanaweka biashara zao, wanaweka visima vyao wanasambaza maji nchi ambazo soko la huria liko huria kweli kweli.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa Zanzibar maeneo hayo muhimu ni ya *strategic* ambayo mpaka sasa hivi hayajabinafsishwa wala hayajapelekwa katika soko huria. Kwa haya mengine Mhe. Mwenyekiti, ni kweli huku Zanzibar hasa Pemba kuna milango mingi, bandari bubu ziko nyingi nimeona mimi mwenyewe nilivyotembelea kipindi kile cha karafuu, niliona bandari bubu kweli ziko nyingi. Pamoja na hayo tumeona kitu kimoja tu kwamba mpaka sasa

hivi kuna magendo yalikuwa yanafanyika ya sukari, unga wa ngano wakati mwengine na mchele kutoka Pemba kupelekwa sehemu nyengine kama Tanga na Mombasa. Hili tumeliona na tunalifanyia kazi, lakini vitendo hivyo bado havijaathiri upatikanaji wa vyakula Pemba na upatikanaji wa vyakula Unguja, kwamba kuleta tishio kwa ajili ya wananchi kwa sababu kuna mambo mabaya yanafanywa kwani bandari bubu ziko nyingi.

Kwa hiyo, tuchukue tena sekta hii ya biashara kama ya mchele, sukari na unga wa ngano tukaichukua tena tukairudisha mashirika ya serikali jambo ambalo ni gumu na haliwezekani kuliendesha kirahisi. Lakini niseme kweli kuna maeneo ambayo serikali inaona bado idhibiti biashara zile, lakini kuna maeneo mengine kwa sababu tunao uwezo wa kuyadhibiti, kulinda na kuwatetea na kuwalinda wananchi tumeona bado tuendelee biashara hii ifanywe na watu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nawaombeni sana mnapouliza swali muutumie muda vizuri kama mnavyoona orodha ya shughuli za leo shughuli ni nyingi, kwa hivyo muuliza swali aende moja kwa moja pamoja na kupamba yake lakini asiende mbali sana. Kwa hivyo, jitahidini kuokoa muda. Ahsante sana.

Nam. 83

Umilikishwaji wa Jengo kwa Wizara ya Afya

Mhe. Mtumwa Suleiman Makame (Kny: Mhe. Masoud Abrahman Masoud) - Aliuliza:-

Sekta ya afya ni miongoni mwa sekta nyeti ambayo inahitaji uimarishaji wa hali ya juu. Hospitali iliyoko katika Shehia ya Mbuzini ni Hospitali ambayo jengo lake lilikuwa likimilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi kwa wakati huo ambapo kwa sasa ni Manispaa ya Magharibi "A". Jengo hilo lilimilikishwa kwa Wizara ya Afya kwa makubaliano ya kurejesha shilingi milioni 70 kwa Halmashauri husika.

(a) Je, fedha hizo zimeshalipwa na kama hazijalipwa zitalipwa lini.

(b) Hospitali hiyo katika awamu iliyopita ilitembelewa na Mhe. Rais ambapo aliahidi kuwa serikali itasimamia umalizaji wa jengo hilo ili kuifanya Hospitali hiyo kuwa ya Wilaya, Je, ahadi hiyo ya Mhe. Rais itatekelezwa lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 83 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Wizara ya Afya ilimilikishwa jengo la hospitali ya Mbuzini na kulipokea na makubaliano ya wazi ya ulipaji wa shilingi milioni 70 kwa Halmashauri hiyo. Hata hivyo, wizara yangu inafanya utafiti wa hali ya juu ili kuweza kupata taarifa sahihi juu ya deni hilo. Mara tu zitakapopatikana taarifa za kutosha kuhusu deni hilo wizara itaandaa utaratibu wa kulilipa kwa mujibu wa taratibu za kiserikali.

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar tayari jengo hilo limeshakabidhiwa kwa Wizara ya Afya na hatua mbali mbali za ujenzi zinaendelea kuchukuliwa. Ahsante.

Nam. 147

Gawio la Mafuta kwa *Ambulance* za Majimboni

Ali Suleiman Ali (Shihata) (Kny: Mhe. Yussuf Hassan Iddi) - Aliuliza:-

Kwa kuwa Wabunge na Wawakilishi tumejitahidi sana katika majimbo yetu kununua gari za Wagonjwa (*ambulance*).

Je, wizara ina mpango gani wa kuzigawia mafuta gari hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 147 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya inathamini sana michango mbali mbali inayotolewa na Wabunge, Wawakilishi na watu binafsi wa maeneo tofauti ya Unguja na Pemba ukiwemo huu mchango mkubwa wa utoaji wa *ambulance* katika maeneo ya Donge, Kiembesamaki, Chukwani, Fuoni, Pwani Mchangani na maeneo mengine ambayo yamewahi kutoa huduma hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivi sasa msaada mkubwa wa mafuta kwa gari zinazohudumia wagonjwa majimboni, nguvu ya wizara zimeelekezwa katika hospitali za Makunduchi na Kivunge. Kwa kuwa sera yetu ya afya inahimiza

ushirikishwaji kikamilifu kwa jamii katika kusaidia sekta hii, tunatoa wito kwa jamii au mfadhili yeyote kujitolea kusaidia huduma hii majimboni ili iweze kuwa ni huduma endelevu. Ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Waheshimiwa Viongozi; Wabunge, Wawakilishi pamoja na wananchi wema ambao wanasaidia suala la afya ni muhimu hasa tukizingatia kwamba afya inamgusa kila mtu. Lakini kwa bahati nzuri katika juhudi hizo huwa baada ya kutoa magari katika hospitali zetu au vituo vya afya, huwa kunahitajika madereva, kunahitajika na mafuta, na kwa kuzingatia hospitali ya Fuoni imekusanya majimbo kama matatu mpaka manne. Jimbo la Fuoni wenyewe, Pangawe, Kijitoupele mpaka watu wa Ndijani na kwengineko wanakuja huku.

Je, kwa kuwa gari lipo na zima kabisa lina matatizo ya mafuta na dereva, wizara ina mpango gani wa makusudi kuhakikisha kwamba gari hilo linafanya kazi, linapatiwa dereva, mafuta na mambo mengineyo ili kuwahudumia wagonjwa hasa akina mama wajawazito wanaostahiki kupelekwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja au Mwembeladu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, hili naomba nilichukue kama ni ushauri kwa vile kwenye wizara hatujawa na mpango huo. Naomba nilichukue ni jambo la maana, ni jambo ambalo litasaidia sana wagonjwa wetu waliomo majimboni na hasa kwa *ambulance* ilipo, lakini hakuna dereva hakuna mafuta. Sasa nakuomba sana uridhie nilichukue nilipeleke katika wizara lifanyiwe utafiti ikigundulikana kama ni tatizo na kweli uwezo hamna basi tutatafuta njia ya kusaidia. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru.

Nam. 55

Ukosefu wa Miundombinu ya Meli za Mizigo Pemba

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Serikali haijawa na mpango wa kuimarisha miundombinu ya bandari kwa upande wa Pemba ili meli za mizigo ziweze kufunga gati moja kwa moja katika

bandari ya Mkoani na kushusha mizigo ikiwemo vyakula badala ya kushusha Unguja na baadae kusafirisha mpaka Pemba na kusababisha mfumuko mkubwa wa bei za bidhaa kwa kufidia gharama za usafirishaji.

(a) Je, kwa kuwa tatizo hilo ni la muda mrefu na wanaoumia ni wananchi, serikali italipatia lini ufumbuzi tatizo hilo ili kuwapa unafuu wa bei na upatikanaji wa mahitaji kama wanavyonufaika watu waliopo Unguja.

(b) Kwa kuwa bandari ya Wete na Mkoani zinashindwa kufunga meli kubwa kuanzia tani 2000 za mizigo na kuendelea kutokana na kina chake cha maji kuwa kidogo, serikali ina mpango gani wa kuongezea kina cha maji na kufanya bandari ya kisasa kama ilivyofanyika bandari ya Malindi, Unguja.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 55 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa wizara yangu kupitia Shirika la Bandari inachukua hatua mbali mbali kuimarisha huduma za Bandari ya Mkoani na Wete kwa kuimarisha miundombinu ya bandari hizo pamoja na kuzipatia vifaa vya kubebea mizigo ili kuwavutia wenye meli za nje kupeleka meli zao huko Pemba.

a) Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari inaendelea kufanya jitihada za kuwashajihisha mawakala wa meli za nje (*shipping liners*) kuweza kupeleka meli moja kwa moja katika Bandari ya Mkoani ili kuwapa unafuu wananchi wa Pemba. Jitihada hizo ni pamoja na kupeleka tagi moja ndogo katika Bandari ya Mkoani na kujenga eneo la kuhifadhia mizigo ikiwemo makontena kule Mkoani.

   Aidha, Shirika limenunua vifaa mbali mbali vya kubebea mizigo ambapo kreni moja ya tani 25 inatarajiwa kupelekwa Pemba hivi karibuni baada ya madereva wake kuhitimu mafunzo ya uendeshaji wa chombo hicho.

   Baada ya hatua hizo kuchukuliwa wizara yangu ina imani kuwa mawakala wa meli za kigeni wataanza kupeleka meli zao kwa mujibu wa uwezo wa gati yetu.

b) Bandari ya Mkoani ina uwezo wa kupokea meli za zaidi ya tani 2000 (hadi tani 3000) ambapo meli hizo huwa na kina cha maji mita 6 pamoja na urefu wa mita 110. Kwa hivi sasa serikali haina mpango wa kuongeza kina cha maji katika Bandari hizo, hata hivyo wizara yangu kupitia Shirika la Bandari inaimarisha njia za meli kuingilia bandarini kwa kuweka maboya mapya ya *solar* pamoja na kuifanyia matengenezo minara yote ya Pemba.

Pamoja na hivyo, wizara inaendelea kufanya mazungumzo na wawekezaji katika kuwekeza bandari ya Wete. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 69

Wafanyakazi Bandarini Kugawiwa kwa Makundi

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)(Kny: Mhe. Shehe Hamad Mattar) - Aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Bandari lina wafanyakazi waliogawiwa katika makundi mawili ambayo ni kundi 'A' na kundi 'C' ambapo kundi 'A' ndio lenye wafanyakazi wa kudumu na wanapata stahiki zote kama vile mishahara, likizo na mafao mbali mbali na kundi 'C' ndio lenye wafanyakazi vibarua ambao wengine wanafika takriban miaka 20 na hawajaajiriwa rasmi.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kuwapatia ajira ya kudumu wafanyakazi hawa wa kundi 'C' ambapo wameshafanya kazi kwa muda mrefu ili kutoa motisha wa kazi kwa wafanyakazi wengine wa kundi hilo.

b) Je, wizara inafahamu kuwa wafanyakazi hawa wanafanya kazi katika mazingira ambapo hata vitendea kazi huwa hawapatiwi na wanapoumia katika kazi huwa wanajitibu wenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye vipengele (a) na **(**b) kama ifuatavyo:-

(a) Naomba kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa, Shirika la Bandari linakabiliwa na changamoto mbalimbali, miongoni mwa changamoto hizo ni suala la wafanyakazi wa Kundi C, kutokana na wingi wa

wafanyakazi hao ambao idadi yake ni 519. Shirika haliwezi kuwaajiri wote kwa pamoja na limekuwa likiwaajiri kwa awamu tofauti, tokea kuanzishwa kwake mwaka 1997 hadi kufikia 2009 limeshaajiri wafanyakazi 136. Baadhi ya wafanyakazi hao wameajiriwa katika taasisi nyengine, wapo waliojiunga na Ushirika wa Jitihada Njema na Makuli Saccos bandarini ambao ni wafanyakazi 58. Idadi halisi ya wafanyakazi wa kundi C kwa sasa ni 430, kati ya hao kuna wafanyakazi 93 ambao wamestaafu kutoka taasisi nyengine za serikali.

Wizara yangu kwa kupitia Shirika la Bandari iliandaa ripoti maalumu kuhusiana na wafanyakazi hao na kuiwasilisha mbele ya Baraza la Mapinduzi na hatimaye BLM lilimuagiza Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na Uchukuzi wa wakati huo kushirikiana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kulitafutia ufumbuzi suala hilo. Wizara hizo mbili ziliunda kamati maalumu ya kutathmini na kupendekeza utaratibu bora wa wafanyakazi kundi C.

Kamati hiyo ilifanya kazi iliyokabidhiwa na kuiwasilisha ripoti yake kwa mawaziri wa wizara hizo. Aidha, ripoti hiyo inatarajiwa kupelekwa Baraza la Mapinduzi karibuni kwa ajili ya kupitiwa, kujadiliwa na hatimaye kutolewa maamuzi yanayofaa.

(b) Wizara yangu inaomba kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa, wafanyakazi wote wa Shirika (wakiwemo kundi C) hupatiwa vitendea kazi pale vinapohitajika na kwa mujibu wa taratibu za shirika.

Aidha, wafanyakazi wote wakiwemo wa kundi C wanapopata ajali na kuumia wakiwa kazini hupatiwa huduma ya kwanza pamoja na fidia maalumu kwa mujibu wa taratibu na sheria.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa kuhakikisha kwamba bandari yetu ni uti wa mgongo na pia ni uhai katika nchi kwa kupata bidhaa kutoka nje na kusafirisha nje ya nchi. Pia kwa kuzingatia kwamba Shirika la Bandari hivi sasa limefanya jitihada kubwa sana katika *operation* maalumu ya kuhakikisha kwamba makontena yanapakuliwa kutoka asubuhi, mchana na usiku kwa masaa 24 bila ya kuchoka, na ukienda mandhari yake pia inaonesha kwamba inaridhisha.

Je, Mhe. Naibu Waziri watu wanasema *"mcheza kwao hutunzwa"*. Wizara kupitia Shirika la Bandari kwa wafanyakazi wetu hawa ambao wamewajibika vizuri na kuonesha ari ya kuleta ufanisi katika kazi zao imeandaa angalau zawadi gani au tunzo gani kuwasaidia wafanyakazi hawa ili waongeze ari katika kazi yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali kwamba ripoti hii tayari tushakabidhiwa na katika kipindi hiki kifupi Mhe. Waziri aliniagiza mimi kuwa Mwenyekiti wa ile Kamati. Na tumeshaandaa *package* nzuri tu, lakini hatuwezi kuisema sasa hivi mpaka ikapate maamuzi ya Baraza la Mapinduzi baadae asiwe na wasi wasi wafanyakazi wale watafurahi sana na watalishukuru sana Shirika na vile vile Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Namuomba avute subra *In shaa Allah* mambo mazuri hayataki haraka.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa kwa hatua zinazoendelea tujitayarishe kumpokea Naibu Spika kuendelea na kikao.

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)

UCHAGUZI WA NAFASI ZA UONGOZI KWENYE UMOJA WA MABUNGE YA NCHI ZA JUMUIYA YA MADOLA TAWI LA ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama Katibu alivyotangulia kusema naomba tubadilishe kwa sababu *quorum* yetu haijatimia kabisa, *quorum* yetu hata nusu ya wajumbe haijafika. Hivyo, nafikiria sio vizuri kufanya uchaguzi wakati baadhi ya Wajumbe hawapo na hata nusu ya Wajumbe haijafika. Hivyo, ningeshauri katika ratiba yetu ya leo kutakuwa na hoja ya Mjumbe, Mhe. Mohammed Said Mohammed, itatangulia shughuli hii halafu baadae iwapo *quorum* itatimia tutaendelea na suala zima la uchaguzi.

HOJA YA MJUMBE

KUHUSU MATOKEO HATARISHI KATIKA SEKTA YA UWEKEZAJI YA VIWANDA

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza kusoma hoja yangu binafsi ningeomba kuwatambua kuwepo kwa *management* ya Kiwanda cha Mahonda ambao nimewaalika wapo pale juu. Nimekuletea karatasi sijui kama umeiona.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe taarifa sinayo hapa kama ninayo wajibu wa ...

Wajumbe: Wameshatambulishwa.

Mhe. Naibu Spika: Wameshatambulishwa? Haya, ahsante endelea.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetufikisha tukiwa katika hali ya uzima na afya njema, lakini nikushukuru wewe binafsi kwa kukubali hoja yangu hii kuileta mbele ya Baraza hili tukufu.

Nimshukuru sana Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali Barazani, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kwa kukubali naye hoja yangu kuletwa mbele ya Baraza hili, lakini niwashukuru sana Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu kwa kunipa moyo kila ninapoleta hoja hizi.

Vile vile niendelee sana kuwashukuru wananchi wangu, wapiga kura wangu wa Jimbo la Mpendae kwa kuendelea kuniamini na mimi nawaambia nitawawakilishi vizuri katika Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, niendelee sana kukishukuru chama changu cha Mapinduzi kwa kunipa uwezo wa kupeperusha bendera katika jimbo langu lakini vile vile kuiendeleza na kuitetea Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hoja hii imeundwa chini ya Kanuni ya 27 fasili ya 1(n) na 27 fasili ya 3 na 49 fasili ya 1 na Kanuni ya 50 za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012.

Mhe. Naibu Spika, maelezo ya hoja.

KWA KUWA, uwekezaji wa viwanda ni njia moja muhimu sana katika kufikia maendeleo ya nchi ambapo nchi nyingi hutafuta wawekezaji ili kuimarisha sekta ya viwanda kwa ajili ya kuinua uchumi wake.

NA KWA KUWA, wawekezaji wanaotaka kuwekeza katika nchi huangalia mambo mbali mbali, zikiwemo sera za uwekezaji na matokeo mbali mbali yanayojitokeza katika nchi kabla ya kuanza uwekezaji kwenye nchi husika.

NA KWA KUWA, kumekuwa na vitendo mbali mbali vinavyofanywa kwa makusudi ndani ya Zanzibar ambavyo vinahatarisha kuimarisha uwekezaji wa viwanda nchini.

NA KWA KUWA, vitendo hivyo vimekuwa vikijitokeza mara kwa mara katika Kiwanda cha Sukari cha Mahonda kilichopo Zanzibar katika Mkoa wa Kaskazini, Wilaya ya Kaskazini 'B' - Unguja na vitendo hivyo ni matokeo ya uchomaji wa moto katika mashamba ya miwa yanayomilikiwa na kiwanda hicho.

NA KWA KUWA, dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuimarisha uchumi wake kupitia uwekezaji wa viwanda ndani ya Zanzibar, hii inatokana na ahadi aliyoitoa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein katika Hotuba yake ya Uzinduzi wa Baraza la Tisa la Wawakilishi kutafuta wawekezaji wenye mitaji mikubwa, uwezo na dhamira ya kweli ya kujenga viwanda nchini.

NA KWA KUWA, endapo serikali itashindwa kudhibiti matokeo kama haya ambayo yataendelea kufanyika siku hadi siku ni kuhatarisha uwekezaji wa viwanda ndani ya nchi yetu.

Matokeo hayo ya kuchomwa moto kwa mashamba ya miwa yanayomilikiwa na Kiwanda cha Sukari cha Mahonda pamoja na hasara iliyoipata kiwanda kwa matokeo hayo ni kama haya yafuatayo:

Hapo chini nimejaribu kuonesha jadweli hasara yake na tarehe zake.

SN	TAREHE YA TUKIO	JUMLA YA EKA	HASARA ILIYOPATA KIWANDA
1	16/04/2015	2.2	4,711,034/-
2	08/01/2015	9.11	6,455,516/-
3	15/10/2015	151.2	5,370,732/-
4	29/12/2015	150	1,832,160,000/-
5	03/01/2016	50	494,576,000/-
6	16/01/2016	100	1,221,440,000/-
7	02/02/2016	133	1,334,155,200/-
8	05/02/2016	41	396,260,800/-

9	06/02/2016	50	434,181,120/-
10	20/03/2016	303	3,669,849,450/-
11	20/04/2016	7	50,657,600/-
12	24/05/2016	7	44,850,400/-
13	17/07/2016	16	125,744,000/-
14	21/07/2016	20.38	110,950,400/-
15	24/07/2016	1	7,568,640/-
16	03/08/2016	7	52,980,480/-
	JUMLA	**902**	**9,791,911,372/-**

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa jadweli la hapo juu, ndani ya kipindi cha miezi kumi na sita (mwaka mmoja na miezi minane) kuna matokeo ya uchomaji moto kumi na sita (16) yaliyofanywa katika eka mia tisa na mbili (902) na yamesababisha hasara ya Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Saba na Tisini na Moja, Laki Tisa na Elfu Kumi na Moja, Mia Tatu na Sabini na Mbili (9,791,911,372/-).

NA KWA KUWA, hasara hiyo iliyotokea haiathiri shughuli za kiwanda tu, bali inaathiri nchi kwa ujumla, kwani imepunguza kiwango cha uzalishaji wa sukari, ajira za wananchi na mapato ya serikali.

NA KWA KUWA, pamoja na matokeo hayo, yaliyofanywa katika nyakati tofauti, bado hakuna mtu yeyote aliyekamatwa kufikishwa katika vyombo vya sheria dhidi ya vitendo hivyo vibovu vya uhujumu uchumi ambavyo vinaathiri shughuli ya uwekezaji hapa nchini hasa katika maeneo ya viwanda.

Mhe. Naibu Spika, sasa ningeliomba Baraza lako tukufu liazimie mambo yafuatayo:

1. Serikali kupitia vikosi vyake vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi

Zanzibar (*ZAECA*) ifanye upelelezi wa kutosha ili kubaini chanzo cha vitendo hivi na wote wanaohusika na vitendo hivi wafikishwe mara moja katika vyombo vya sheria.

2. Serikali ya Mkoa kupitia kamati zake za ulinzi na usalama ziweke mikakati madhubuti ili kuimarisha ulinzi katika Mikoa yao hasa katika maeneo ya uwekezaji.

3. Elimu ya ulinzi shirikishi baina ya Vikosi vya Ulinzi na Usalama pamoja na Jeshi la Polisi na wananchi iendelee kutolewa ili wananchi waelewe umuhimu wao katika kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo ya nchi kwa ujumla.

4. Masheha katika maeneo husika watoe ushirikiano wa kutosha kwa vikosi vya ulinzi na Jeshi la Polisi ili kutoa taarifa haraka iwezekanavyo kabla matokeo kama haya hayajafanyika na pia kutoa taarifa kwa wale wanaohusika ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo na maazimio niliyoyatoa, ningeomba Waheshimiwa Wawakilishi waweze kuchangia hoja hii ili tuone jinsi gani tunaweza kuishauri serikali kwa ujumla wake.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja iltolewa iamuliwe)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mjumbe ameleta hoja yake sasa mimi nafikiria kwamba tunaweza kuanza kuchangia. Waheshimiwa Wajumbe nina majina ya wachangiaji wanane na ningependa sana kwamba angalau kila mtu achangie kwa muda usiozidi dakika 15. Kwa hiyo, nitaanza na mchangiaji wa mwanzo ambaye ni Mhe. Ali Suleiman Ali atafuata Mhe. Nadir Abdul-latif na baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Abdalla Ali Kombo.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Naibu Spika ahsante sana, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuchangia hoja ya Mjumbe, Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Naibu Spika, hoja hii binafsi inahusu tokeo kubwa la uchumi katika nchi yetu, na hoja hii imekuja wakati ambao unastahiki kuangalia azma ya serikali yetu huko mbele tunakokwenda. Kwa sababu asilimia kubwa ya Wajumbe

waliokuweko hapa mimi nikiwa mmoja wao, naiomba serikali kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia njia zozote walizokuwa nazo kuwekeza au kuita taasisi na mashirika mbali mbali kuwekeza katika nchi yetu ili wananchi wetu wapate ajira. Lakini sio ajira tu, pia serikali yetu kuweza kupata fedha kwa ajili ya kuwaendeleza wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, mwekezaji nia yake ni njema ya kuwekeza ili kupata faida yeye, aliowaajiri na serikali. Sasa sisi kelele zetu huwa kila mara tunawaomba wawekezaji waje kutoka mashirika mbali mbali au makampuni kwa ajili ya kuweka kile wanachoona kinafaa kuleta maendeleo katika nchi yetu na kusaidia maendeleo kwa Mfuko wa Serikali Kuu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilibahatika kuishi Mahonda miaka ya 1960/70, nimeanza kusoma Skuli ya Mahonda, mwanafunzi wa mwanzo kabisa wakati ule inafunguliwa skuli ndiye niliyekuwa kiongozi wao, wakati huo unaitwa *chairman*, lakini ndiye kiongozi wa Skuli ya Mahonda. Pale Polisi nilipokuwa nalelewa upande wa pili wa kiwanda ilikuwa mikarafuu mitupu, lakini Mwenyezi Mungu ana rehema zake kila muda ukiendelea mbele mambo yanabadilika, pameweza kujengwa kiwanda kile kila fani ya maendeleo katika eneo hilo ipo.

Kwa hivyo, kiwanda hiki kilianza muda mrefu na hatima yake tuliona maendeleo yake, lakini baadae kilikufa kutokana na mazingira ya uendeshaji, akatokea ndugu yetu mwekezaji huyu tuliyekuwa naye kwa dhamira njema kabisa ya kuwekeza ili wananchi wapate sukari hapa hapa kwa urahisi, Pili wananchi wetu wapate ajira, serikali ijiongezee pato lake la maisha na wao wenye kiwanda wapate. Mimi nawapongeza sana wenye kiwanda hiki.

Mhe. Naibu Spika, lakini zuri zaidi niseme kwamba, sisi huwa tunatembelea maeneo ya biashara hata sukari, kutokana na ubora wa sukari ya Zanzibar ya kiwanda cha sukari ambapo kuna *packet* zimefungwa za kisiwa, hii sukari *made in Zanzibar* jamani, ni sukari nzuri iliyo na ubora kuliko sukari kutoka nje. Wenye biashara ndogo ndogo kama juisi wanakwambia sukari hii bora kuliko nyengine, kuwa ni tamu na inakidhi haja kwa malengo ya mtumiaji.

Sasa matokeo haya yaliyotokea wakati mwekezaji nia yake njema kabisa pana haja serikali kuwa makini lakini pia pana haja ya mwekezaji kuwa makini na wananchi pana nini, paangaliwe. Mimi ningeomba sana Mheshimiwa hakuna jambo zuri katika maisha kama kuishi karibu na jamii. Kwa hivyo, tutizame pana tatizo gani ikawa mara kwa mara matokeo 16 yametokea katika uchomaji

wa miwa kwenye maeneo haya, hii ni hatari. Hatari yenyewe isitoshe inarudisha nyuma wawekezaji wengine.

Mimi juzi katika kuchangia Mswada wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii nilimuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwamba tubadilike, tutoke kwenye ujenzi wa majumba kukodisha tuingie kwenye ujenzi wa viwanda mbali mbali. Nikatoa rai kwamba Zanzibar asilimia mia moja tumezungukwa na bahari, Zanzibar tunaweza kupata samaki wazuri kuliko samaki wanaovuliwa katika maji baridi kama Mwanza, lakini kwa nini samaki wa Mwanza wanaitwa Sato, wanapelekwa nchi za nje na wanasifiwa samaki wazuri, kumbe samaki wanaovuliwa katika bahari ya Zanzibar ni wazuri kuliko samaki wa maji baridi mara mia moja. Ladha yake nzuri na kila kitu, nikaiomba serikali tutafute wawekezaji waweke viwanda vya kusindika samaki. Kwa bahati katika majibu Mhe. Waziri alisema tu kwamba tuko mbioni na *In shaa Allah* kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu tutafanikiwa.

Sasa kitu ninachokiomba kwa serikali yetu tuzungumze na wana jamii wanaozunguka katika mazingira hayo ya kiwanda chetu, lakini labda tutafute kiini pana kitu gani kinachosababisha haya.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninaloliamini katika nafsi yangu choyo ni kitu hatari sana, ukiwa mchoyo Mheshimiwa utaharibikiwa, sisemi wenye kiwanda wachoyo, nasema labda kuna baadhi ya watu, mfano mimi nimetoka Mahonda hapa nilipozaliwa au nilipolelewa, imetokea ajira fulani nimekosa kapewa mfano tu aliyetoka Donge, Uroa, Kiwengwa kw anini sikuipata mimi. Pia inachangia, iangaliwe kitu gani kwa sababu kwenye sekta ya uwekezaji wananchi wanapiga kelele wale wazawa wa pale. Kwanza wapatiwe ajira wao ndio walinzi wako namba moja.

Kwa hivyo, hili mimi ningetoa wito kwenye kiwanda tuangalie wafanyakazi wetu. Najua mfanyakazi akiwa wa pale pale basi ana usalama mkubwa kuliko anayetoka nje, anayetoka pale atakuwa na imani ya kukulinda wewe kwa sababu ni kwao, lakini anayetoka nje anaweza kufanya hujuma kwa mambo yake anayoyajua yeye, sitegemei yatokee hayo kwa pande zote.

Ombi langu Mheshimiwa tukae tuangalie kitu gani kitatusaidia kuwasaidia wenzetu hawa wa kiwanda chetu cha sukari cha Mahonda, kwa sababu ni tegemeo pekee kwa Zanzibar, kiwanda kikubwa ambacho kina hadhi na kinaeleweka hata duniani sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, sukari ya kiwanda cha Mahonda inaweza kuuzwa popote katika nchi zote duniani kwa ubora wake. Kwa hiyo, hii ukienda katika maduka kuna wajasiriamali tunafuatana nao sisi, ukienda pale unakuta sukari kutoka Brazil na hii unaambiwa kisiwa kutoka Zanzibar, kwanza bei yake iko chini kwa wale waliokuwa hawajui. Kwa hiyo, niseme tu paketi ukiikuta inauzwa 84 huyu anauza 83 Zanzibar utaambiwa inauzwa 80. Kwa hiyo, hiyo ni faraja kwetu kwa walaji wetu. Naomba serikali hili tuliangalie juu ya hujuma hizi.

Mhe. Naibu Spika, tatizo jengine labda kutokuwa na elimu ya kuelewa kiwanda faida yake nini, mwekezaji anapata nini na wewe muajiriwa unapata nini. Mimi ningeomba taaluma najua inatolewa, lakini iongezwe zaidi kwa wananchi wanaoishi katika mazingira yale, kwa sababu kuhujumu uchumi ni uhalifu. Kwa hiyo, niiombe serikali juhudi itafutwe tuzingatie kwa muhujumu yeyote anayemtumia mtu ikiwa yeye katia moto kwa taratibu anazozijua yeye basi Jeshi la Polisi lifanye kazi zake kwa uwezo wake wote kama ilivyosema taarifa hii, ili watu hao wakamatwe iwe ni kielelezo kwamba kikundi hichi ndio wahujumu uchumi na sheria za kuhujumu uchumi tunajua ni uhaini katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, tunaamini kwamba kuna wawekezaji wetu wengi wana imami hiyo ya kuwekeza kama nilivyosema mwanzo, na kwa kuzingatia hiyo hatutegemei kuona kiwanda cha sukari peke yake. Mimi nasema kwa Zanzibar hii tunaweza kuwa na viwanda vya samaki hata vitatu au vinne, ukienda Msuka Pemba huko, ukienda Mkumbuu huko ukaja zako Wete mfano Mkoani au Chake Chake tunapokuwa Pemba tunaona samaki vya kufanywa hawana, baadhi ya wakati inakuwa wakati ule tunaita shuwari, sisi wavuvi tunajua.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, wakati ule samaki wale ndio wa kuhifadhiwa na kupata viwanda kufanyiwa kazi kwa rasilimali ya kusafirishwa nje na walaji pia watapatikana hapa.

Zamani nakumbuka kulikuwa na samaki wa vibati, samaki wale wanatoka nje wanaletwa hapa siku za kusi kachaga au kaskazi kachaga, samaki wale huwa ni soko kubwa katika nchi yetu. Turudishe viwanda vyetu tuwaombe wawekezaji waje ili viwanda vile vitusaidie panapo haja ili kuendelea na maisha yetu ya kila siku na vijana wetu kupata ajira.

Mhe. Naibu Spika, maendeleo ya nchi huletwa na wananchi wenyewe na tunaambiwa katika hatari ya maisha ya kila siku "mjenzi wa nchi atakuwa mwananchi na mvunja nchi atakuwa ni mwananchi aliyekuwa hajui utaratibu", Kwa hivyo, niseme tu kwamba wawekezaji wapewe taaluma yetu nzuri hawa wanaotaka kuja na wenzetu hawa naamini wako vizuri, kwa sababu

wamejitahidi sana wanaendelea kuishi na jamii, na jamii inajua kuwa wanaishi nao vizuri, lakini bado nasema pana kikundi ambacho haijaeleweka na kikundi hichi kimejificha au kinaeleweka kwa wengine, kitafutiwe busara pawe na mazungumzo pawe na taaluma.

Mhe. Naibu Spika, si vibaya unajua sisi wengine kama tulivyosema tulioishi kule hebu tukutane na jamii ya pale turuhusike kidogo tuzungumze na wale wananchi. Wananchi kuna tatizo gani tuelezeni undani, naamini Mheshimiwa mimi kama Shihata sijisifu kama nina uwezo zaidi, lakini niko karibu sana na jamii katika kila sehemu.

Mhe. Naibu Spika, mimi mpaka leo kuna wananchi wengi wanajua kuwa mimi kwetu Mahonda nilikozaliwa, lakini Mhe. Ussi Yahya anajua Kiwengwa ingawa kwetu Dunga nitazikwa Dunga. Lakini nimekulia Mahonda, nimejijua kila kitu Mahonda na kubwa zaidi napajua Mahonda kuliko huko kwengine. Kwa hivyo, Mheshimiwa ningeomba sana, mimi nitajitolea mmojawapo kwenye kiwanda tushirikiane twende pale tukazungumze na jamii kila pembe; Zingwezingwe, tunakwenda Donge Mnyimbi, Kinduni, Daraja la Mto Mchanga uko wapi, mote tutakwenda tukazungumze nao kwa sababu nia yetu kujenga, na nia yetu tupate ukweli. Mimi Mheshimiwa nakwambia lakini iwe ni kitu ambacho cha kwenda kutafuta kwa nia njema Mheshimiwa tutapata faida.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo niseme kwamba nawapongeza wenzetu wawekezaji wa kiwanda cha sukari, namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie awape imani hiyo hiyo waendelee na wawe wastahamilivu, lakini mimi nitajitolea na niko tayari Mheshimiwa kwenda kuzungumza na jamii ya Mahonda kwa sababu tunaweza kuitana wana Skuli na Skuli yetu wenyewe ile wanafunzi sote tuliosoma pale, na wazee wengine wanatuelewa tuzungumze kuna tatizo gani kwa manufaa ya wananchi wetu, kiwanda chetu na nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nawaomba wenzangu hoja hii binafsi tuichangie, tutoe rai na tutoe maelezo kwa sababu wenzetu hawa ustahamilivu wao neema yao tunaipata, wakisema kiwanda wao basi, neema ile itatuondoka itakuwa bei inapanda. Kwa hivyo, baada ya hayo naiunga mkono hoja hii na namshukuru au nampongeza sana mtoa hoja kwa sababu naye ni mtu ambaye mbunifu, kajua kero na matatizo na wajibu wake ndio hichi chombo cha kuleta kero ile tuizungumze kwa maslahi ya nchi yetu. Nashukuru Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe nilitaja majina ya watakaofuatia kwa ajili ya kuchangia, nawaomba radhi wale ambao nimewataja nitampa nafasi Mheshimiwa Waziri katika Afisi ya Rais achangie kwa kuwa ana majukumu mengine ameniomba achangie sasa hivi ili aweze kwenda kufanya majukumu yake mengine. Mheshimiwa Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Lakini pili kukushukuru wewe kwa kuweza kunipa nafasi na mimi kutoa mchango wangu katika hoja hii ambayo imewasilishwa mbele ya Baraza lako hili tukufu.

Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika, sina budi kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mpendae kwa kuweza kuguswa na jambo hili ambalo imani yangu kwamba matarajio yake yeye ni kutaka kuona serikali tunaweza kukaa vizuri zaidi katika kuhimiza na kushajihisha fursa hii ya uwekezaji nchini, ikiwa ni miongoni mwa kichocheo na miongoni mwa vyanzo vya mapato kwa serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niseme kwamba ni wajibu wetu serikali na ni wajibu wetu mkubwa sana kuwatumikia wananchi, na pili kwamba serikali hatuna tatizo na wawekezaji. Pia ni wajibu wetu sisi kama serikali kuhimiza, kuwalinda na kuwasaidia wawekezaji wetu wanapokuja hapa nchini ili kuweza kukuza sekta hizi pamoja na kukuza vile ambavyo wanakuja kuviwekeza kwa maslahi mapana ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, hoja iliopo hapa kwa namna moja au nyengine inahusisha masuala ya kihalifu katika nchi yetu. Tunaposema masuala ya kihalifu kwa maana ya kwamba ni masuala ambayo yanahujumu mali za wawekezaji zinazopelekea hasara kubwa kwa wawekezaji hao. Lakini pia na uharibifu mkubwa sio tu kwao wao na athari zake ni kama vile ambavyo Mheshimiwa Mjumbe ameweza kuziainisha. Lakini kama tunajua kwamba suala hili linahusiana na masuala ya uhalifu bila ya shaka yoyote mtu ambaye anaitwa muhalifu anakuwa ni mtu ambaye anajipa nafasi ya kufikiri vizuri zaidi, lakini pia kutazama pale panapo mapungufu ili aweze kufanikisha ile nia yake ovu ya kuona ile dhamira ya kutaka kufanya tendo lile inaweza kuwa ni vizuri kwa kukidhi ile haja ya matakwa, na nia mbovu kabisa ya kudhoofisha shughuli na maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ukitizama kwa makini utaona kwamba katika suala hili ambalo Mheshimiwa Mjumbe ameleta hoja yake inahusiana na wananchi wanaozunguka maeneo ya mashamba haya. Kwa mtazamo huu maana yake jamii husika kwa namna moja au nyengine inawezekana ikawa inawajua watu hawa na inaendelea kuwaficha. Kwa hiyo, mimi naomba tu nitoe wito kwa jamii inayozunguka eneo hili, wachukuwe fursa ya kupima na kuona faida na athari za uwekezaji ili kuweza kuchukua nafasi ya kuwabainisha, kuwataja na kwenda kuwakalia ushahidi pale ikibidi hawa watu ambao wanashiriki katika matendo haya maovu ambayo yanazuia jitihada za serikali katika kukuza na kustawisha sekta hii ya uwekezaji.

Mhe. Naibu Spika, lakini jambo la tatu nadhani kuna haja ya kujitizama upya kama kiwanda na kama mwekezaji, inaoenkana kwa namna moja au nyengine kuna pengo la mashirikiano baina ya muwekezaji na wananchi wanaozunguka katika eneo hili.

Imani yangu kama mwekezaji atachukua nafasi ya yeye ya kushawishi kama vile ambavyo sote tunajua katika ule msingi wanaouita ***good neighbourh****ood principle,* matarajio yangu kwamba kama mwekezaji huyu na yeye atachukua nafasi ya kuwaelimisha, kuwashajihisha lakini pia kuwa-*engage* majirani na watu wanaoishi katika maeneo haya, inawezekana katika sehemu moja au kwa namna moja au nyengine ikawa ni sehemu ya kupunguza kadhia na matokeo kama haya ambayo yamekuwa yakijirejea mara kwa mara.

Ikitokea hivyo atapata fursa hasa mwekezaji huyu ya kuweza kujua matatizo yao, changamoto zao lakini pia kuna fursa ya kuweza kuona namna gani ataweza kushirikiana katika kuona kiwanda kile, mashamba yale yote yanakuwa na faida kwa pande zote mbili. Kwa maana kwamba mwekezaji na pia wananchi wanaozunguka katika eneo lile.

Jambo la tatu Mhe. Naibu Spika, ningeomba tu kutoa nasaha zangu kwa kuona tu kwamba chombo hichi cha Baraza la Wawakilishi ni chombo kikubwa sana Mhe. Naibu Spika, na chombo hichi ndio matarajio na mategemeo ya Wazanzibari wote kwa ujumla katika msingi wa sera pamoja na usimamizi na uendeshaji wa shughuli zetu za kiserikali. Niombe tu kwamba si vibaya kuja na mawazo, maono na mtazamo kama huu, lakini tusije kufika pahali chombo hichi tukakifanya kwamba ndio chombo cha rufaa katika mambo kama haya. Kwa sababu ukisoma vizuri hii *paper* inaonesha kama vile serikali labda hakuna chochote ambacho imekichukua katika kuona namna gani tunaweza tukashiriki katika kunusuru mambo kama haya yasiweze kujirejea.

Kwa hivyo, imani yangu kwamba chombo hichi kitaendelea kubaki kama ndio ngome ya Wazanzibari lakini pia kuona kwamba kuna haja basi tutumie fursa zaidi nzuri za kuweza kwenda serikalini kuweza kukutana na wahusika, kubadilishana mawazo lakini pia kuwapa mitazamo yetu na kuona kwamba kwa kiasi gani serikali inaweza ikayachukua mapendekezo hayo au mtizamo wetu huo katika kuona tunaweza kutengeneza njia nzuri zaidi ya kuwasaidia wawekezaji wetu hawa ili waweze kujilinda na mali zao.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni wajibu wetu wa msingi wa kutambua tu kwamba mlinzi wa kwanza wa mali ni yule mmiliki wa mali yeye mwenyewe. Kwa hiyo, imani yangu kwamba wenzetu hawa wa kiwanda ni wajibu wao kushirikiana na watu wengine katika kuona wanaendeleza jitihada hizi za kuweza kulinda maeneo haya, lakini pia tutambue kwamba eneo hili ni kubwa na liko *very scattered*, sasa msingi mkubwa wa ulinzi wake unategemea ushiriki wa wenye kiwanda namna watakavyoweza kuwashirikisha majirani na wanaofaidika na maeneo yale ili na wao waweze kutanua wigo wa kuona kiasi gani wataweza kushiriki katika kulinda mali hii ambayo imeekezwa.

La mwisho tu Mhe. Naibu Spika, mimi nimeyaona mapendekezo na ninaamini karibu ya mapendekezo yote sioni kama yana matatizo kwa upande wa serikali, na ni msingi wa wajibu mkubwa sana wa serikali ambao haya Mheshimiwa Mjumbe anaweza kutukumbusha. Imani yangu kuona tu kwamba mambo haya ambayo amekuja kuyapendekeza ni jambo zuri katika kukumbushana kama serikali kuweza kuona tunaweza kusimamia vizuri zaidi ili tuweze kuendeleza ulinzi, ustawi na uwekezaji kwa faida yetu sisi na vizazi vinavyokuja.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache nasema nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza kama walivyotangulia wenzangu nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na kwa kufika hapa.

Mimi nitachangia kwa uchache vile vile kwa muda mfupi tu hoja ya Mhe. Mohammed Said Mohammed, hoja makini, hoja nzuri kwa niaba ya nchi na kabla ya kufika huko mwisho kuja kusahau mimi hoja hii naiunga mkono asilimia mia kwa mia.

Mhe. Naibu Spika, masuala ya viwanda ni masuala muhimu katika nchi yetu ni biashara ambayo inaongeza pato la nchi, inaleta sifa ndani ya nchi. Katika suala hili sisi Wawakilishi wajibu wetu ni kuiuliza serikali, kushauri na vile vile

kuisifu serikali sio kukaa kila siku tukawa tunazungumza mambo mengine, lakini ni wajibu wetu serikali yetu inapofanya mazuri basi tuizungumze kwa mujibu wa uzuri wake na inapokosea tuishauri kwamba imekosea.

Vile vile, hoja hii ya msingi zaidi kwa sababu Mhe. Mohammed Said Mohammed nahisi kaona suala hili kwamba litaleta athari kubwa hapo baadae katika nchi yetu, hasa katika suala la uchumi na viwanda na ndio maana yake ya kwamba akaleta humu ndani tulijadili.

Lakini ninachotaka kuwahakikishia Waheshimiwa wenzangu pamoja na wananchi wote wa Zanzibar serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Makamu wa Rais kwamba serikali yenyewe naamini kwa nafsi yangu kwamba haitaki wala haipendezekewi na mambo yote yanayofanyika ya kuhujumu uchumi wa nchi au matatizo yoyote yale ambayo yanasababisha nchi ionekane iko katika matatizo. Suala hili naamini linawakera, naamini linawasumbua na naamini wanalifuatilia, lakini ninachotaka kuwahakikishia wananchi kwa ujumla kwamba hakuna serikali hata moja duniani iliyokuwa kamilifu kwa sababu mkamilifu ndani ya dunia hii ni Mwenyezi Mungu peke yake, sisi sote ni binadamu ambao hatukukamilika hata kwa asilimia 60.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa ushauri wangu mimi wa mambo machache tu kwamba wananchi wenyewe kwanza wawe makini, hasa wa jimbo lile ambalo maeneo yale ya Kaskazini linalohusiana na eneo lile, na vile vile wafahamu kwamba wanapochoma moto kuwakomoa labda Kiwanda cha Sukari cha Zanzibar basi wajihesabu kwamba wamejikomoa wenyewe na sio wamekomoa serikali moja kwa moja, kwa sababu watakapochoma moto miwa kuhakikisha kwamba wanaona wenyewe kwamba ni furaha kwao kwamba serikali itatetereka labda kwenye uchumi, labda serikali itaathirika na mambo mengine basi mimi nahisi hawafanyi jambo la busara na huu mimi naweza nikasema kwamba sijui niwaambie kwamba akili zao hazitoshi au haziko vizuri.

Kwa sababu kwanza wafahamu wanachokichoma pale ni chakula, na pindipo kama ni chakula unakiendea kinyume iko siku na wewe utakuja kufa njaa itakusuta vile vile wakati unapochoma miwa. Miwa unapoichoma ni sawa sawa unakuwa una -*destory* chakula, na miwa vile vile wafahamu kwamba madawa yanatumika kwa sukari, chakula kinatumika kwa sukari, na vitu vyengine vingi vinatumika kwenye sukari. Na ili nchi yetu iendelee basi wananchi wote tunatakiwa tuwe watu wenye busara, hekma na tusifuate mambo ambayo hayana maana, tukafika hatua ya kuchoma vitu au kutaka kuikomoa nchi. Matokeo yake tunajikomoa wenyewe.

Nchi hii kama hatujailinda wenyewe, hatujawa na akili wenyewe za kukaa tukatatua matatizo haya basi hatutofika popote. Serikali kwa hili mimi ninawatetea kwamba hawapo pamoja nalo suala hili linawakera sana na mimi nimeshaona. Kama Serikali ingekuwa suala hili ambalo hawajalifuatilia au haliwaumi mimi ningekuwa wa mwanzo humu kupiga kelele kulizungumza. Lakini mimi Mhe. Mohammed Said Mohammed ninampongeza sana kwa kulileta hili, lakini ninachotaka kuwaambia Wajumbe wenzangu kwamba suala hili linasababishwa na wananchi ambao hawaitakii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar jambo zuri, jambo lenye kheri, wanataka kurudisha uchumi nyuma.

Na vile vile ningeshauri sana kwamba hawa wamiliki wa kiwanda wakakae na Mhe. Mbunge na Mwakilishi wa maeneo ikiwa labda Jimbo la Mahonda na Jimbo la Donge, Wabunge washiriki pamoja na Wawakilishi, pamoja na ulinzi na usalama wa maeneo yale kwa pamoja ili wakakae na wananchi waangalie nini kuna tatizo au kitu gani ambacho kinachosababisha kuchomwa miwa hii, na matokeo yake kiwanda kile kisiweze kufanya kazi kama ilivyotakikana.

Sababu hizi zinatokana zaidi kwamba inawezekana kwenye mambo haya tofauti. Pengine wananchi wametumwa kwa mambo ya siasa kuikomoa Serikali, pengine wafanyabiashara wanakomoana, wanachomeana ili wamuulie mwenzao biashara, pengine suala hili linafanyika kwa mtu kwamba mmoja au wawili ndani ya kijiji wamekerwa.

Sasa ningeomba sana kama walivyoeleza wenzangu kwanza *investor* yeyote anapofika nchini awe na busara na hekma ya kukaa na wanajamii vizuri, kuwasikiliza, kuangalia kuna matatizo gani. La sivyo basi kutakuwa kuna mtihani.

Na ninachotaka kuhakikishia kwamba suala hili kwa ufahamu wangu kiwanda kilichopata matatizo ndani ya nchi hii mimi ninahisi kwa nguvu zote ni Kiwanda cha Sukari. Ningeomba sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikashirikiana zaidi, ninajua wanashirikiana, lakini ikashirikiana zaidi pamoja na wenye kiwanda hichi ili kwenda kutatua matatizo haya kwa wananchi na kuangalia vipi kuna tatizo gani ili walitatue.

Vile vile ningeomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ingewasaidia Jeshi la Polisi kuwapatia fedha binafsi, wawe na mfuko maalumu Polisi kunapotokezea uhalifu wa kutangaza mapato ambayo atakapomtaja mtu aliyefanya tukio lile, basi atapata shilingi milioni tano zawadi yake.

Lakini kwenye Serikali yetu mpaka hivi leo mimi suala hilo sijawahi kuliona, inawezekana labda lilitokea sijaliona lakini mimi kwa muda mrefu sijalisikia. Ningeomba sana Serikali iwa-*support* Jeshi la Polisi pia kwa fedha siyo kwa mdomo mtupu, ambapo wakafanye kazi kwa sababu dunia ya sasa hivi mtu anaweza kuwa anamjua aliyefanya uhalifu lakini hatoi ushahidi kama hajapata kitu. Kwa sababu watu wengi wanafahamu kwamba atakayetoa ushahidi ni mtu mhalifu vile vile, ataandamwa. Lakini mimi ninaamini kama kitatajwa kima atakayemtaja aliyeunguza miwa sehemu fulani, atakayeleta ripoti kwa uhakika kabisa basi tunampa fungu la shilingi milioni tano au shilingi milioni tatu, lakini litasaidia, na hili suala litakwisha.

Lakini tukienda hivi hivi kila siku kunachomwa moto kumeshafikia hatua ya bilioni tisa. Leo wawekezaji hawa wakija kufunga kiwanda, wakija wakienda wakawaeleza na wenzao nchi za nje basi tuhakikishe kwamba kwenye suala la viwanda vya sukari katika nchi yetu tutaathirika na hatutegemei kama atakuja kufungua mtu, kwa sababu itakuwa tayari rekodi mbaya ipo kwamba kumechomwa.

Kwa sababu kuna watu wa aina mbili. Kuna watu wataweza kuondoka hapa wakaenda kuzungumza mambo mazuri huko nje ya nchi na kuna watu wanaweza wakaondoka hapa wakaenda kuyazungumzia mambo mabaya ambayo hayapo. Sasa ninachotaka kuomba mimi kwamba wenye kiwanda wafahamu tupo nao pamoja, hata sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hili jambo hatufurahiki nalo na tutasaidiana nao kwa njia yoyote. Lakini vile vile wawe karibu sana na wananchi pamoja na kushirikiana na Waheshimiwa, wakakae kule waangalie matatizo haya vipi wataweza kuyatatua. Na ninaamini kwamba haya mambo yatakwisha kwa kuwashirikisha wananchi kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa kuwa hili suala limegusa sana Kiwanda cha Sukari na mimi nimeona nilizungumzie suala hili, zaidi kwa sababu viwanda vyengine naona vipo katika *safe side* sijasikia matatizo matatizo, ndiyo maana sitoweza kugusia huko ili niwaachie na wenzangu.

Mhe. Naibu Spika, kwa hili ninamshukuru Mhe. Mohammed Said Mohammed, Mwakilishi makini, kwa kuleta hoja yake, na ninaiunga tena mkono asilimia mia kwa mia.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Nadir kwa mchango wako mzuri kabisa. Sasa Mhe. Abdalla Ali Kombo.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchangia hoja hii ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Mpendae Mhe. Mohammed Said Mohammed.Kwanza ninaiunga mkono asilimia mia kwa mia.

Mhe. Naibu Spika, hii ni moja katika aibu kubwa sana katika nchi yetu inayotokea Mkoa wa Kaskazini Unguja. Aibu ambayo hizi bilioni tisa ni pesa kidogo sana ukilinganisha na aibu ambayo inatokea. Aibu hii hatuwezi kuiwekea thamani ya pesa yoyote katika nchi. Kwa sababu hii *message* si ya Unguja na Pemba, hii ni *message* ambayo sasa hivi ipo dunia nzima.

La kwanza Mhe. Naibu Spika, mchango wangu wa mwanzo ni kwamba ninashauri uongozi wa kiwanda pamoja na watu wa Kaskazini yote "A" na "B" wananchi kukaa pamoja na hasa wazee wa Kaskazini, akina Mzee Nyange, Machano, Foum, Mbwiga kule Kandwi, wakae pamoja wazungumzie suala hili. Na hili siyo suala la siasa ni suala la kijamii. Kwa hivyo wakae pamoja, wazungumzie chanzo ni nini cha mambo haya.

Na wawekezaji bahati mbaya mimi siwajui kwa muda mrefu katika mazungumzo yao basi wapewe wazee wa Kaskazini. Hata kazi ya kutafuta chanzo ni nini wapewe watu wa Kaskazini, kuanzia Mfenesini mpaka Nungwi. Na isiwe maoni ya siku moja, iwe maoni ya karibu wiki halafu wao walete jibu tufanye nini kuondosha aibu hii katika nchi. Hilo la kwanza.

Mhe. Naibu Spika, tumeshuhudia mwaka mmoja uliopita hasa Tanzania Bara kulikuwa na matukio mengi mabaya, machafu, ubadhirifu, heshima katika nchi ilikuwa hakuna. Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli la mwanzo alilolifanya alimuondoshea Dkt. Hosea. Yeye ndiye aliyekuwa dhamana wa rushwa, mabaya mengine ya wizi yalikuwa yanakuwa makubwa kuliko yeye. Kwa hivyo cha mwanzo akaanza kumuondosha yeye.

Mhe. Naibu Spika, ninachofahamu mimi kwenye Mkoa wa Kaskazini aidha Mkoa ama Wilaya zake, muna Kamati za Ulinzi na Usalama. Vibaka hawa wamekichoma kiwanda mara kumi na sita, lakini Kamati hizi za Ulinzi na Usalama bado zipo na hazina taarifa yoyote ya maana ya kufuta kitu hichi.

Kwa hivyo mimi napendekeza katika hoja hii Kamati hizi hazifai ziondoshwe. Kama mara kumi na sita kunatiwa moto katika eneo la Mtendaji Mkuu wa Serikali wetu katika nchi na Baraza, mara kumi na sita unaambiwa kuna Kamati za Ulinzi na Usalama, ina maana yake hawafai. Kwa hivyo tumfuate

Dkt. Magufuli awaondoshe waje watu ambao wanafaa, tuondoshe kadhia hii na aibu hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hapa hakuna mambo ya halibadiri kama yaliyosomwa Pemba. Maana nilikuwa na Mheshimiwa mmoja wa Pemba kasoma halibadiri anasema watu wametawanyika. Sasa hakuna kutawanyika kwa halibadiri. Hapa Serikali ifanye kazi kuwaondosha watu ambao hawafai. (*Makofi*)

Lakini la tatu Mhe. Naibu Spika, samahani kidogo jirani zangu wa Kizimkazi, kulikuwa na mnyama asubuhi kaamka anakuja miguuni tu, huyu vipi, vipi huyu. Pana mzee mmoja akasema mmh! sisi watu wazima si mnyama huyu. Haiwezekani aingie miguuni namna hii. Huyu mwekezaji kumi na sita anatiliwa moto lakini bado wanaendelea na kazi.

Sasa kidogo na hii nayo inanitisha, kwamba mara kumi na sita umeshafikia bilioni tisa wanakutilia moto na wewe unaendelea na kazi tu. Sasa isijekuwa mnyama wa Kizimkazi anakuja miguuni tu huyu. Sasa nayo kidogo Mhe. Naibu Spika, tuwe makini hawa watu siku hizi dunia imeharibika hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Abdalla Ali Kombo. Mchangiaji wetu anayefuata sasa hivi ni Mhe. Suleiman Makame Ali atafuatiwa na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja hii.

Mhe. Naibu Spika, haitokuwa vyema kama sitomshukuru Mhe. Mohammed Said Mohammed aliyeleta hoja hii mbele yetu. Mhe. Naibu Spika, ninamshukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, nende kwenye suala la elimu ya ulinzi shirikishi.

Mhe. Naibu Spika, suala la elimu ya ulinzi shirikishi ni suala muhimu sana katika jamii zetu. Leo hii Mhe. Naibu Spika, kumejitokeza watu hawa wasiotakia mema Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar na kufanya hujuma hizi.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia vijana wengi wanalilia kuhusu suala la ajira. Leo Kiwanda kile cha Sukari Mahonda, kinaajiri zaidi ya vijana si chini ya mia tatu

naa. Leo wanajitokeza watu hawa wanafanya uharibifu makusudi ili kuirudisha nyuma Serikali pamoja na wawekezaji.

Mhe. Naibu Spika, pia Serikali ina nia njema kwa wananchi wake kwa kuwatafuta wawekezaji wa viwanda vikubwa na viwanda vya kati. Lakini leo Mhe. Naibu Spika, kumejitokeza wahujumu wa uchumi hawa wanafanya makusudi ili kuwarudisha nyuma wawekezaji ambao wana nia njema ya kuwekeza.

Mhe. Naibu Spika, mimi niwaombe wananchi wa Zanzibar, vijana, wazee waone angalau uchoyo kwa kule wenzetu Tanzania Bara wanavyopiga hatua hivi sasa kwenye maendeleo ya viwanda. Sisi hapa Zanzibar viwanda vilikuwepo na kama nia ya Serikali hiyo hapo inataka kuanzisha viwanda upya, lakini leo Mhe. Naibu Spika, kumejitokeza wimbi hili la watu hawa wasiotakia mema nchi yetu, wasiotakia mema vijana wetu. Pia vile vile niwaombe vijana wawe mstari wa mbele, kwa sababu vijana ndiyo tunaolilia sana kuhusu masuala haya ya ajira kuwafichua hawa waliokuwa hawana lengo jema kwetu sisi vijana.

Mhe. Naibu Spika, pia niombe Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye viwanda na wakulima *(Zanzibar National Chambers of Commerce, Industry and Agriculture)* kwamba hawa nao wahusike kwenye kutoa taaluma kwa wananchi. Pengine wakienda wao kwa jamii kutoa taaluma ile itakuwa labda itafika kwa wale wananchi hususan kwamba wajue kwamba hili nalo linawagusa.

Mhe. Naibu Spika, sitaki niseme mengi sana isipokuwa naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia na pia niwaombe wenzangu wote kwamba tuunge mkono hoja hii iliyoletwa mbele yetu.

Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Suleiman. Mchangiaji mwengine ni Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini baadae atakuja Mhe. Rashid Makame Shamsi na baadae atafuata Mhe. Mussa Ali Mussa.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Naibu Spika, na mimi ninakushukuru sana kunipatia wasaa huu wa kuchangia mawili matatu katika hoja hii ya Mhe. Mjumbe makini kabisa Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli jambo la kuhujumu uchumi halikubaliki, na sisi kama Waheshimiwa Wawakilishi hatuna budi kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Kiwanda cha Sukari kimewekeza nchini mwetu na sisi kwa vyovyote tunafaidika na tutaendelea kufaidika. Kwanza kwa watu wetu kupata ajira. Pili uchumi wa nchi tunapata zao moja hilo la *cash crop*, la kuuza, hili ni tija kubwa sana, zao la fedha hilo.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nimejaribu sana kuangalia maazimio aliyotoa Mhe. Mohammed Said na niseme kwa kweli yanahitaji kuyatafakari kwa kina sana.

Mimi nina mtizamo wangu mwengine kidogo, kwa sababu nimeangalia sana maazimio yake yamejikita kwenye ulinzi na usalama lakini naomba twende zaidi.

Suala la kwanza ninataka tujiulize nimefikiri Waheshimiwa nimewasikia wengine wakichangia, nini hasa chanzo cha haya. Kwa sababu Kiwanda hichi kilikuwepo siku za nyuma, miaka ya sabini, thamanini.

Mhe. Naibu Spika, kuna Mkoa wa Kaskazini wakati huo Kiwanda kilichokuwa na Mchina ilikuwa kama Serikali kamili Mahonda pale, magari, watu wanavyoshughulika, nyumba za kukodisha, matrekta yanavyokwenda, malori mpaka Mkwajuni watu wanakuja wanakwenda, shughuli zilikuwa kwa nguvu kabisa. Mwenyewe utatikisika hasa utaona kwamba huku uchumi kumeamka Mkoa wa Kaskazini. (*Makofi*)

Sasa hakukuwa na *sabotages* hizi. Kama zilikuwepo kidogo tu na zilianza kweli kidogo. Zilianza kidogo na hiyo ndiyo sehemu ya pili ninataka niigusie kwamba hili suala hili limegawika sehemu mbili; Kiwandani kwenyewe (*management*) uongozi nao uangaliwe sana. Ninaamini kuna matatizo madogo madogo upande wao. Juu ya *management* ya shamba na Kiwanda. Lakini pili *management* ya *staff* wao. Kweli wanawa-*treat* inavyopaswa? Ninasikia wenyewe uongozi wanafika pahala hawapatani, wanagombana wenyewe kwa wenyewe, wanagombana na wafanyakazi, hawawapi stahiki ipasavyo. Kwa hivyo pengine hawa hawa nao wanashiriki katika kufanya hujuma hizi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ichunguzwe kwa makini. Kwanza Mhe. Naibu Spika, kwanza nijikite hapo hapo, mua ukishaupanda *life span* yake mwaka mmoja ndiyo unauvuna, unauvuna kwenda sasa kuifanya hiyo sukari. Lakini sasa ule mua *mother crop*, ile ya mwanzo ukishapanda kile kigongoro cha mua, ukipanda kile baada ya mwaka tayari. Sasa unakuja unakata. Halafu

subsequently, yaani kila mwaka unachipua ule unakata tena, tunaita *ratoon crop*. Zile *ratoon crops* mwisho ziwe kumi. Wenyewe wanaziweka mpaka kumi na tano, kumi na mbili. Ule mua tena unatoa majani mengi mtu akipita tu moto mdogo na joto la Kaskazi lile unaripuka tu au mwengine ana sigara kidogo unaripuka tu.

Kwa hivyo *management* wenyewe kwanza wayatunze mashamba yao, yawe masafi. Kwa kitaalamu unasema wafuate *full agronomic practices.* Lakini wenyewe *management* ya kiwanda hawafanyi. Mashamba machafu, kuna majoka, machatu mule Mhe. Naibu Spika. Huwezi hata kupita, ni hatari, hao wafanyakazi wanaogopa. Matokeo yake wanachoma moto, ile ni kawaida kabla ya kuvuna unachoma moto lakini siyo moto mkubwa, lakini usipochoma kule huwezi kuingia kwenda kuvuna. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Naibu Spika, tunaomba sana Kiwanda chenyewe au *management* wafuate *appropriate agronomic practices* za mua, kwa kweli hawazifuati. Hilo ndiyo tatizo mojawapo linalosababisha hii mioto, samahani Mhe. Haroun Ali Suleiman hayupo, siyo mioto, huu moto usitokee. (*Makofi*)

Jengine Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema inaelekea kuna wafanyakazi hawawapi stahiki zao, wanawakera, wanagombana nao na wao wana-*retaliate*, aah! kama unanifanyia hivyo basi na mimi nitawaonesheni na *incidences* hizo zipo tumepata salamu.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo kubwa kama kiwanda, *management* lazima wakae vizuri na wananchi wanaowazunguka, majirani zao, uhusiano huo kweli upo.

Wakati ule niliposema kama miaka ya 70 au 80 ilikuwa kama ile serikali nzima ya pale, kiwanda kile kila mmoja anakiendesha mwenyewe, anaona hasa *he is part and parcel* ya kiwanda kile. Lakini leo kila mmoja anaona mmh! hawa wamekuja kuwekeza hapa au wamekuja kutunyima haki zetu, ile *mentality* haikuweko nyuma huko.

Sasa *management* ya kiwanda haina budi kukaa na uongozi wa wananchi wale, wananchi waulize ni nini tatizo. Kweli tunakubali ardhi ile waliazimwa wananchi walime mpunga tena kwa mikataba, baada ya muda warejeshe, ukikaa nao ukiwafahamisha na mkafanya mpango, aah! na nyinyi mtapatiwa mpango mtalima miwa mtapata tija, hawakatai. Lakini tukienda kwa malumbano, basi kwa wananchi itakuwa ni vigumu sana.

Jengine Mhe. Naibu Spika, lazima kiwanda nao wawe na *social responsibility*, watizame tija za wananchi pale kuna matatizo gani. Kuna njia zao, kuna maduka wanataka kukopa, labda barabara, kituo cha afya wasaidie dawa, wakae nao kwa *harmony*, kwa makubaliano mazuri, waishi vizuri. Naamini ukifanya hivyo Mhe. Naibu Spika, matatizo yataondoka.

Mhe. Naibu Spika, kubwa zaidi nataka kusema kwamba kiwanda kile nacho kiende kwa taratibu za kiwanda. Najua *environmental impact assessment* imefanywa, kwa sababu sio cha leo ni cha zamani, kama nilivyosema athari ya mazingira, athari ya watu wakae vipi, waende vipi, tija nayo imeshaonekana sukari tayari tunazalisha. Lakini suala la msingi narudia tena Mhe. Naibu Spika, sababu hasa chanzo tukitafute.

Mhe Mohammed Said Dimwa kaeleza vizuri sana, lakini zaidi kajikita kwenye ulinzi. Kasema vikosi, mikoa, ulinzi shirikishi, masheha, lakini mimi nataka kushauri na kiwanda chenyewe nacho kiwe na walinzi wake, wala wasiwape *SMG*, wala wasiwape bastola. Yale mabunduki ya zamani yanaitwaje yale

Waheshimiwa Wajumbe: Magobore.

Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame Mwadini: Magobore, wakae na yale tu. Si mashamba, wengine wanakaa na yale, walinzi wetu wengine wanakaa nayo yale, hapiti mtu, na yale kama wanakaa mule *block* moja. Mfano kama chumba chetu hiki zaidi ya mara tatu au nne, wanakaa mule, anaangalia *point* kwa *point*, na zile *trace passing* watu wanaopitapita mule wasiruhusiwe au waruhusiwe lakini waangaliwe hawafanyi hujuma. Kwa hivyo, wakibaini tu moto umetokea upesiupesi hatua inachukuliwa. Lakini inafika moto unawaka mpaka shamba linateketea. Kwa kweli inaelekea ulinzi mule mashambani haumo.

Lakini zaidi Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba sana *management*. Ukitizama hizi *figures* za hapa za hujuma zilizotokezea, ukiangalia hizi tarehe nyingi hujuma zimetokea wakati wa kiangazi ambapo jua ni kali. Ukiangalia Disemba kama ukurasa wa 2 chini pale tarehe 15 Oktoba, kabla ya vuli. Ndio vuli maana yake Oktoba ndio vuli ndio inaanza, lakini bado hapa. Ukija namba 4 kwenye ukurasa wa 3 juu pale tarehe 29 Disemba tayari tuko kwenye kiangazi hapa heka 150 zimeteketea, njoo tarehe 16 Januari heka 100 zimeteketea kwenye kiangazi hicho. Njoo tena namba 9 au namba 7 tarehe 2 Februari heka 133, wakati wa kiangazi huo. Njoo tena namba 9 tarehe 6 Februari heka 50 zimeteketea. Njoo tena namba 10 tarehe 20 Machi heka 303, tarehe 20 Machi kiangazi ndio kikali. Halafu njoo tarehe 21 Julai heka 20.38. Sasa utakuta zaidi

ni wakati wa kiangazi, sasa lazima kiwanda wa-*realize* kwamba hizi hujuma zinafanywa wakati gani. Kwa hivyo, wao wachukue *appropriate steps* za kuhakikisha wakati ule wana-*beef up* ulinzi wao na juhudi zao, wao ndio mali yao hii. Kutegemea kwamba serikali iwasaidie ulinzi, aah! sisi wenyewe haututoshi. Kwa hivyo, sisi tutawasaidia lakini na wao wajibebe wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuunga mkono hoja, kweli kama hujuma ya uchumi haikubaliki na sote wajibu wetu kuipiga vita ipasavyo, tuone sukari inazalishwa na tuna-*export* baada ya *surplus* kupatikana nchini.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwinyihaji Makame. Waheshimiwa Wajumbe, bado nina wachangiaji kama 9 na nitajaribu kupunguza muda. Nashukuru kwamba wengi hawatumii muda wote dakika 15, lakini nitajaribu sana kupunguza muda ili basi wale wote ambao wameomba kuchangia wapate kuchangia.

Kwa hivyo, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Rashid Makame, baadae anafuata Mhe. Mussa Ali na ajitayarishe Mhe. Simai Mohamed Said.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hoja binafsi ilioko mbele yetu ya Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa).

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kwanza kumpongeza sana Mhe. Mohammed Said Dimwa, kwa kuweza kuileta hoja hii muhimu, kwa maendeleo ya viwanda na uchumi katika taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, tunatarajia au lengo letu ni kwamba nchi yetu iwe ni nchi ya viwanda, na ili tuwe ni nchi ya viwanda tunahitaji usalama wa kutosha wa nchi yetu, lakini vile vile tuwe na ubora wa miundombinu yetu, pamoja na rasilimali watu ambayo itatumika katika kufanya kazi katika viwanda hivi.

Mhe. Naibu Spika, ni faraja kuona kwamba wenzetu wanajitokeza katika kuwekeza katika sekta hii ya viwanda. Lakini ni masikitiko makubwa kuweza kuona kwamba kuna hujuma katika sekta hii na hususan hoja iliyoko mbele yetu ya Kiwanda hiki cha Sukari cha Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina mambo mbali mbali ya kuchangia. Lakini la kwanza ni la kujiuliza kwamba Zanzibar ina viwanda mbali mbali, hiki cha

sukari ni sehemu ya viwanda hivyo. Lakini kwa nini hujuma zielekee zaidi katika Kiwanda hiki cha Sukari na sio viwanda vingine.

Hapa kuna swali lazima serikali na sisi wananchi na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tujiulize, kulikoni, kwa nini hujuma hizi zielekee zaidi katika Kiwanda cha Sukari cha Zanzibar, na isiwe katika viwanda vyengine.

Mhe. Naibu Spika, yumkini kuna jambo maalumu au kuna chanzo maalumu. Wenzangu waliotangulia niwashukuru sana, na naweza kusema kwamba wamechukua mawazo yangu mengi katika kulichangia suala hili. Hapa nimpongeze sana Mhe. Mwinyihaji Makame kwa mchango wake mzuri juu ya hili.

Mhe. Naibu Spika, lazima tutafute chanzo cha tatizo. Suala la uendeshaji wa Kiwanda cha Sukari, ili tuweze kuona chanzo hasa cha tatizo, lazima kwanza tutazame historia ya kiwanda.

Kiwanda hiki kilikuwepo na kilikuwa kinaendesha shughuli zake, tokea utawala wa Mhe. Marehemu Mwenyezi Mungu amlaze pahala pema, Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi. Kiwanda hiki kilikuwa kinaendesha shughuli zake.

Mhe. Naibu Spika, kihistoria inasemekana kulitokea uhujumu wa kiwanda hiki, kwa hivyo kikashindwa kufanya kazi mpaka alipojitokeza mwekezaji. Sasa ni vyema tuanzie tokea kule katika kuchunguza, ilianza vipi ikafanyika hujuma katika miaka ile, nini chanzo cha hujuma katika miaka ile, kwa sababu inawezekana walihujumu kwa misingi wanayoifahamu miaka ile, pengine ndio hawa hawa, sasa wamegeuza tu upande wa shilingi wanaingia sasa katika miwa. Kwa hivyo, hili ni la kutizamwa na wapo wenzetu wenye historia nzuri ambao wanaweza kutupa.

Mhe. Naibu Spika, lakini chengine cha kutazama ili kuweza kuona chanzo cha tatizo, ni kuwachunguza wawekezaji hawa waliowekeza. Kwa sababu haya masuala ya kuwekeza yana mbinu na taratibu nyingi. Wenzetu wanaowekeza wakati mwengine wanakopa mikopo mikubwa na wakati mwengine wanashindwa kuilipa kwa wakati kutokana na uanzaji wa miradi yao. Inawezekana mwekezaji akabuni mbinu za kuweza kuchoma kwa makusudi ili aweze kupata *relief* katika mikopo aliyochukua katika mabenki. Suala hili lazima tulichunguze. Ingawa kwa ghafla unaweza kusema kwamba mtu aliyekalia tawi hawezi kulikata mwenyewe, lakini inaweza ikatokea.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna mtu mmoja, yeye alikuwa hutembea wakati wa jua kali na baiskeli yake, akifika katikati ya uwanda basi huwa anatoa mipira yote pumzi baiskeli ile, na wanapopita watu wenye vipando huwasimamisha na kuwaomba msaada wa kwenda kuziba pechi kumbe ilikuwa ndio *system* yake ya kuweza kupata mapato. Sasa lazima tuwachunguze vizuri wawekezaji wetu, wasije wakawa wana mbinu hiyo ya mpanda baiskeli huyo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, tuchunguze kwa upande wa waajiriwa wa kiwanda wanaweza na wao wakatoa ripoti, wananchi wa maeneo ya jirani na wao tukiwachunguza tunaweza kupata mawazo yao. Lakini vile vile tuna wafanyabiashara wakubwa wa sukari nchini.

Mhe. Naibu Spika, unajua masuala ya ushindani haya ya kibiashara, wakati mwengine wafanyabiashara wanakatana shingo. Kwa hivyo, na hayo tunapaswa kuyaangalia, kwa sababu kama utakuwa na mwekezaji anazalisha sukari, lakini na mimi ni mfanyabiashara mkubwa wa sukari, maana yake naingiza nchini, kiwanda hiki kikiimarika maana yake soko langu mimi la biashara hii litakuwa chini. Kwa hivyo, wakati mwengine kuna mbinu za wafanyabiashara, kunahitaji uchunguzi mkubwa sana katika kuweza kujua chanzo cha tatizo letu, tusitazame juu juu tu.

Mhe. Naibu Spika, suala hili la tatizo la hujuma za Kiwanda hiki cha Sukari halikuanza leo, limeanza tokea tarehe 16/4/2015, huu ni mwaka mzima. Ninaelewa kwamba serikali haikukaa kimya, nimeziona ziara mbali mbali za Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kutembelea kiwanda hiki na kuweza kufuatilia matatizo, pia kuzungumza na wananchi katika eneo hili.

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu ina utaratibu, kuna kamati za usalama katika wilaya, kuna kamati za usalama za mikoa na kuna kamati za usalama za taifa au ya taifa. Kwa hivyo, nina imani kwamba vyombo hivi havijakaa kimpya juu ya suala hili. Ningefurahi sana katika tatizo hili vile vile tukasikia maelezo ya mtendaji mkuu wa serikali, juu ya jinsi serikali ilivyolishughulikia tatizo hili, ili kuweza na sisi kujiridhisha kwa kuona juhudi za serikali zilizochukuliwa na huku tukilijadili suala hili, nitafurahi sana. Nasema kwamba mimi hapa nitaunga mkono kwa asilimia 50 tu, lakini na asilimia 50 mpaka nitakapopata maelezo sahihi ya juhudi za serikali katika kulifuatilia suala hili na ufumbuzi wake. Nikipata maelezo ya serikali yakiniridhisha, kwa hivyo nitamalizia asilimia zangu 50 kuunga mkono hoja ya Mhe. Mohammed Said Dimwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, suala la moto ni suala ambalo hivi sasa wakati mwengine unaweza ukawa na ulinzi mkubwa, lakini siku hizi kuna teknolojia ya moto kuweza kuripuka bila hata kutiwa na binadamu katika mazingira ya kawaida.

Nafikiri Mhe. Makamo wa Pili wa Rais anaweza kuniamini alipotembelea siku moja kwenye suala la moto kule Kibondemaji. Kuna moto unaweza kuripuka bila hata kuwepo kibiriti. Kwa hivyo, tuweze kuangalia hilo. Tunaweza kuwa na walinzi wanakesha pale, lakini na moto ukaweza kuunguza.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, tuwe na uchunguzi wa kisayansi kwa nini moto unaweza kuzuka, hii ni miwa halafu jua kali, kuna majani makavu, historia za kuvumbuka kwa moto tunaambiwa ilikuwa ni kuchekecha vijiti vikavu au majani makavu. Kwa hivyo, vile vile utafiti unahitajika kuweza kuona hasa chanzo cha moto katika shamba hili, kuna vitu vingi vya kuweza kuangalia.

Mhe. Naibu Spika, nije sasa katika suala la hizi takwimu.

Ningependa Mhe. Mohammed Said Dimwa atakapokuja kufanya majumuisho, basi aweze kuleta hasa *justification* ya hizi takwimu. Mimi hizi takwimu zinanishangaza sana.

Mhe. Naibu Spika, tukitazama tukio la kwanza la heka 2.2 ambalo lilitia hasara kiwanda ya milioni 4,711,034, halafu tukitazama tukio la tarehe 8 heka 9, hapa pana milioni zaidi ya 6. Mimi kwa mahesabu yangu ya haraka haraka ni kwamba tukio la pili, maana yake iwe ni karibu mara tatu ya hasara ya tukio la mwanzo. Lakini ukiifuatilia hii takwimu. Kwa mfano, tukio la tarehe 24/07/2016 tukio la 15, ilikuwa ni heka moja, lakini gharama zake ni milioni 7. Sasa hizi takwimu nahisi hazina uwiano wa heka na uwiano wa gharama. Sasa ningependa Mhe. Mohammed Said Dimwa akija aweze kuleta *justification,* kwa nini huu uwiano hatuuoni.

Kuna heka nyengine miwa ilikuwa mipevu sana, mingine ilikuwa michanga, au kuna mbegu ilikuwa ni nzuri zaidi na gharama kubwa kuliko mbegu nyengine. Nafikiri tungeweza kupata hasa hizi takwimu na tuweze kujiridhisha, kwa sababu isiwe takwimu zenyewe ni za kupika, kwa sababu kuna takwimu zinaweza zikapikwa

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, nakupa dakika moja malizia.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana na nimalizie tu kwa kuweza kushukuru kwa kuja hoja hii muhimu kwa maendeleo

ya nchi yetu. Kwa hivyo, naiomba serikali katika hili kuwa makini zaidi, kwa wawekezaji ambao tunawapa maeneo ya kuwekeza, ili kuweza kuepuka matatizo mbali mbali.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono kwa asilimia 50 katika hoja hii, na asilimia 50 nitakapopata maelezo ya serikali juu ya hatua zilizochukuliwa katika kadhia hii. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mjumbe. Hii hoja lakini haipigiwi buti. Mhe. Rashid, hupigi buti kwenye hoja hii. Tunaendelea Mhe. Mussa Ali.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Ahsante, Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja hii aliyoileta Mtoto wangu Mhe. Dimwa. Bado namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu* W*ataala* kwa kutujaalia kuwa wazima katika Baraza hili tukufu, lakini pia nina masikitiko makubwa sana kuona kwamba kiwanda hichi kimetiwa moto, shamba hili limetiwa moto kwa mujibu wa takwimu hizi na tarehe hizi zilizotajwa hapa na hakuna mtu yeyote aliyekamatwa basi hata *suspect* hakuna, yaani mtu anayeshukiwa pia imeshindikana.

Huyu mtu au kikundi ambacho kinafanya mambo haya basi hichi kikundi kiwe cha malaika, kwa sababu kule kwetu Pemba vitendo kama hivi vya hujuma kama hizi vilikuwa vikifanywa kwa kuchoma mikarafuu, lakini bahati nzuri tuliopoanza kujipanga na jeshi la polisi likajipanga wakapatikana *suspected*, wakawekwa korokoroni basi moja kwa moja vitendo hivi vimekoma na havipo tena wala hivisikii tena, haidhuru hawakupatikana na hatia, lakini ile mshike mshike tu imewafanya wafyate mkia.

Sasa mimi hofu yangu imenijia hapa kwamba wenzetu wa Mahonda wamefanikiwa kupata kiwanda hichi, kiwanda hichi si cha watu wa Mahonda tu, kiwanda hichi ni cha Wazanzibari wote, leo wakaweza kuandaa hujuma kwa kukihujumu kiwanda hichi kwa kweli mashamba haya yaliyohujumiwa na hasara hii iliyoingizwa nia aibu kuitangaza hata hapa kwenye Baraza wenzetu wakaisikia, nchi za wenzetu watatuona watu wa maajabu, tena watu tusiotabirika, tena watu ambao hatutaki maendeleo katika nchi yetu, hichi ni kilio kikubwa sana. Mimi nasikitika sana pamoja na watu wa jimbo langu la Ole wakisikia kwamba leo Mahonda kuna watu wamechoma moto kwa tarehe kadhaa na kadhaa zaidi ya miezi sita na hakuna hata *suspect* waliokamatwa wataona huko Unguja kuna mambo ya maajabu.

Ushauri wangu kwanza iundwe Tume iende ikachunguze tume hii Mwenyekiti wake awe Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda, waende wakachunguze kwa ndani kabisa ni nani au kikundi gani kinachofanya huduma hizi na kinafanya kwa sababu zipi, kwa sababu naona bado nina wasi wasi kuwa sababu hizi sio sababu za kisiasa, ama kutakuwa kuna watu wana madai yao ama ya mashamba yao yanawezekana yamechukuliwa wao wamekosa huduma za kupata kutumia ardhi hii kwa ajili ya mazao yao na hawakulipwa chochote ndio labda wanafanya hujuma hizo.

Na ikiwa hivyo ndivyo, basi ni bora tupate tume nzuri ya watu wasiopungua 22 na mimi mwenyewe nikiwemo kwa sababu nina uzoefu mkubwa wa upelelezi, nipelekwe Mahonda na mimi nitahamia Mahonda nijaribu kuliangalia suala hili, kwa nini litokee kuna sababu gani ya kutokea suala hili, hichi ni kilio cha taifa, hichi ni kilio cha Wazanzibari. Hili ni jambo la ajabu kwa Wazanzibari, kusikia leo Wazanzibari wanachoma mashamba ya miwa. Hii ni hatari kabisa, hata kama hii ni siasa ni siasa ya Abunuasi, sio siasa ya watu, hii ni siasa ya Abunuasi.

Mhe. Naibu Spika, sasa nasema hali hii inataka itizamwe kwa umakini sana sana, pia watu wa Mahonda wapatiwe ajira asilimia 50%, inawezekana ikawa kiwanda kipo Mahonda, mashamba yapo Mahonda, lakini ukienda kuangalia watu wa Mahonda waliopata ajira hawafiki 10, ikawa nayo hii ni sababu. Sasa mimi napendekeza asilimia 50% ya wafanyakazi wa mashamba haya wawe watu wa Mahonda.

Pia, namuomba ndugu yangu Waziri wa Vikosi afungue kituo cha ulinzi pale na askari wa pale asiwavishe ma-*uniform* awaache kama askari wa usalama na waajiriwe katika kiwanda kile, wakae pale kwa kazi maalum ili tuangalie jambo hili halitapatiwa ufumbuzi. Hii ni ajabu kubwa, huu ni mtihani mkubwa, hata hayo madola ya wenzetu wakisikia kwamba sisi tunafanya hujuma katika misaada tunayoipata nadhani watakimbia, hii ni hatari kubwa sana. Hilo ni jambo la pili ni lazima Waziri wa Vikosi aweke kikosi kazi kikae pale ili kifanye hiyo kazi.

Jambo jengine wazee wa Mahonda wote wazawa, mashekhe wote tuwapate tuzungumze nao katika jambo hili, jambo hili si la kukaliwa kimnya, jambo hili si la kuachwa ovyo ovyo, jambo hili si la kupewa muda, ni jambo la hatari sana. Pamoja na hayo maelezo yangu mafupi, naunga mkono hoja na namtakia utendaji mwema mtoto wangu Mhe. Dimwa, ili aje na maelezo zaidi na naunga mkono hoja asilimia mia moja.*(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsamte Mhe. Naibu Spika, kwa fursa hii na mimi nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa), Mwakilishi makini wa Jimbo la Mpendae kwa kuweza kuja kuungana na sisi ili tuweze kushauri na kusaidia Serikali na waweze kutimiza majukumu yao ya kila siku.

Lakini nichukue nafasi hii pia kuwapongeza ma-*back benchers* wenzangu wote waliochangia hii hoja, lakini shukurani za pekee pia ziende kwa Mhe. Mussa, kwa sauti aliyokuwa anazungumza akinguruma na pia kuomba katika hiyo tume itakayoundwa basi na yeye ahamishwe Mahonda, kwa kweli huu ni ujasiri mkubwa anaonyesha mapenzi yake jinsi gani nchi inavyomuuma na pale hujuma kama hizi zinavyofanyika basi yuko tayari na yeye pia kuingia kazini kwenda kuwatetea Wazanzibari kwa maslahi ya nchi yake, kwa kweli nampongeza sana.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kabla ya kutoa mawazo yangu na kuendelea kumpa pole Mwakilishi mwenzetu Mhe. Saidi, kwa kufiliwa na mwanawe, *In shaa Allah* Mwenyezi Mungu atampa nguvu katika kipindi hichi kigumu na Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahala pema, *amin.*

Mhe. Naibu Spika, kwa upeo ninaoufahamu mimi nakumbuka mwaka 2010 wakati Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alikuwa anafanya ziara za mikoa ya Tanzania, kwa bahati nzuri palikuwa panafunguliwa kituo cha Polisi Bumbwini na yeye ndiye aliyekuwa mgeni rasmi, na pale kipindi kile alisimamishwa Sheha wa lile eneo husika akaitwa mbele ili azungumze matatizo yaliyokuwepo katika maeneo yale. Siku ile ilikuwa ni siku ya kihistoria kwangu kwanza nikapata hofu yule Sheha anapotoa yale malalamiko yake yanakwenda kwa Rais wa Muungano yatafikaje Zanzibar, nikajiuliza kwenye akili yangu, lakini zaidi nikasema kwamba yule Sheha aliposimama pale akaitwa akasema kwamba kuna muhindi kwenye hili shamba hataki sisi tulime, inaelekea sasa baada ya miaka sita utawala sasa umebadilika kwa pande zote mbili za Muungano, lakini bado tatizo hili linaendelea.

Mhe. Naibu Spika, ukitaka kupiga makofi unahitaji mikono miwili, kwa hivyo, hili jambo tatizo ni dogo sana, kwanza niseme kwamba mapendekezo aliyoyatoa Mhe. Dimwa, sijui Serikali leo kama watakubali kutusikiliza? Lakini haya, tutafanya kazi yetu sisi ya ushauri, ukiangalia mapendekezo haya ni ya kujenga nchi yetu. Namshukuru Mhe. Waziri wa Fedha, ananisikiliza kwa makini na ananiangalia tayari anaanza kuwaza anaunga mkono hii hoja na mawazo yetu.

Lakini hofu mimi napata kwa Mwanasheria Mkuu pia, yeye ndiye ambae anaongoza kutupinga sisi mawazo yetu wakati mwengine japokuwa kwa nia njema, anatumia yale mapungufu ya kisheria kuishauri Serikali ili washinde na kuifanya hapa kuwa ni simba na yanga, ndio maana ukakuta hata nguvu za wajumbe katika hili Baraza imepungua, kwa sababu tayari kuna simba na yanga. Lakini sisi kama *back benchers* kwa hoja za wananchi tutaendelea kusimama, tumemuona leo Mhe. Mussa, yaani Simba alivyonguruma humu ndani yuko tayari atakwenda, lakini na sisi tutakapokwenda tutapita kileni katika kipindi hichi kigumu lakini katika mwezi wa Machi na mwezi wa saba wa bajeti tutakutana na tutashikana humu ndani. (*Makofi*)

Sasa nini kifanyike Mhe. Naibu Spika, katika hili, mimi nashauri haya maoni yote yachukuliwe na yafanyiwe kazi, waende kule wananchi kama wao tayari wana hoja zao za kusikilizwa tuwasikilize, waende watu waliokuwa makini wenye upeo wa kufahamu masuala ya kilimo na mimi ningeshauri sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji, aingie na pia Mhe. Dimwa, mwenye hoja nae pia wachukuliwe kwenda kufanya ile kazi na kutatua kwa sababu hapa kinachohitajika ni busara, wawekezaji wenye kiwanda cha Mahonda wakubali kupoteza kitu fulani na wale wananchi wakubali kupoteza pande fulani ili tufikie katikati na kulimaliza tatizo hili. Kwa sababu wanachokitaka wao haiwezekani kwa miaka yote hichi kiwanda hawa wakakiwachia na Serikali kwa sababu wawekezaji wanakuja hapa kuendeleza nchi watalipa kodi, watalima, wata-*create* hizo ajira, lakini pia wanaipatia sifa nchi ili kusema kwamba Zanzibar ukienda kuna viwanda hivi na hivi na kuna haya, lakini leo mwananchi kuchukua hatua za kisheria ni aibu na Mhe. Naibu Spika, natoa mfano lakini wa ukweli kabisa.

Siku ya uchaguzi hapa Zanzibar tukifika wakati panapokuwa na matatizo haki ya Mungu pale Forodhani kama utatoka baada ya saa mbili ya usiku utakuwa unatembea mikono mfukoni unatetemeka, maana yake ulinzi unakuwa mkali kuwalinda Wazanzibari na mali zao, lakini wakati mwengine matatizo kama haya kwa nini huyu muwekezaji tatizo lake halitatuliwi, ili nchi ikapata amani na wao wenyewe wakaendesha shughuli zao. Kwa nini muwekezaji aonewe mara kumi na sita mtu anaonewa, hivi leo binaadamu Mhe. Naibu Spika, wewe kwako mtu aje leo ampige mwanao bakora mara ya kwanza skuli, mara ya pili, hadi mara kumi na sita mtoto anakuja kajaa alama za bakoro ameshacharazwa na mwalimu, utakubali! Huyo mwalimu mbona tutashikana mashati, atachezea mitama na yeye pia pengine.

Kwa hivyo, mimi ninachosema ni kwamba hili shamba kwa kweli Serikali za Mkoa wa Kaskazini, Wizara zote zinazohusika wamewaachia mkono ndio

maana haya yote yamefikia hapa, na ukiingia katika maeneo sisi sote Wazanzibari tunajuana, ukifika tu hilo eneo ukitaka kumuangalia mtu yeyote kwamba nani kafanya katika kijiji pale ulichoingia wakorofi tu, pengine wapo wawili, watatu tu wanatembea kifua mbele na wanazungumza kabisa tutamfanyizia, hizi ndio tabia zetu, tunawalinda hawa wahalifu. Mimi nashauri kazi ianze mara moja wawekezaji waendelee kulindwa na kupendwa, Wizara zinazohusika zichukue nafasi yake tunamuona Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, anasafiri anakwenda Marekani, anakwenda sijui *South Africa* kuleta watu waje kuwekeza.

Sasa huyo muliyekuwa nae ndani mnashindwa mkulinda, ataweza kuwafanyia kazi zake kuwaleta wengine, hao wanaoshughulikia ulinzi fanyeni wajibu wenu ili mumlinde muwekezaji isifike hapa leo anakuja Mhe. Dimwa, Mhe. Dimwa, sio Waziri au Katibu Mkuu, amekuja hapa kuleta wawekezaji wametukalia mbele yetu pale wanatuonea huruma tuwafanyie nini. Maana yake kuna watu wameshindwa kutumiza wajibu wao, hebu niseme Waheshimiwa Mawaziri muliokuwepo hapa nendeni huko, mfano Mhe. Mohammed Aboud, wewe ni Waziri makini kabisa nenda Kaskazini na watu muwafanyie kazi watu, wewe umekuwa Waziri wetu wa Utalii huko miaka ya nyuma, tumeona mambo yalivyotokezea kuwa magumu, hapa palitokezea ulinzi kwa sababu wizi waliwaibia wawekezaji, wizi ulikuwa katika kila maeneo, hata rafiki yetu yule Msumari akapigwa risasi ya mkono, lakini mliingia kazini ulikuwa Naibu Waziri wa Usalama wa Rais na mkaweza kuwatokomeza wote hawa majambazi, leo kwa nini mnashindwa kumlinda mtu mwenye kiwanda chake. Amewekeza pesa zake anataka kulima na mmempa nyinyi kama hamumtaki mwambieni bwana, ahsante kwaheri, hiyo ndio lugha nyepesi.

Sasa mimi nashauri tafuteni utaratibu hii hoja leo tunakuombeni sana kama wasikifu mtuunge mkono, tusiende kwenye kura msimame kwa lugha nyepesi, tumepokea mawazo, tutayafanyia kazi na tutarudi.

Mhe. Naibu Spika, ahsanteni sana kwa kunisikiliza, nimemaliza maneno. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia hoja ya Mheshimiwa makini kabisa Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa), hoja yake hii ya kadhia ya uchomaji wa moto wa mara kwa mara katika kiwanda cha Mahonda Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mhe.Naibu Spika, kama alivyoumwa Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa), kuumwa homa ya maendeleo, kwa kweli na mimi homa hii imenipata sana, kwa sababu leo hichi kitendo kinachofanyika mimi nataka niseme ni aibu kubwa sana sana kwa wananchi wetu hasa wa Mkoa wetu wa Kaskazini, Kiwanda cha Sukari cha Mahonda hakikuanza leo kama walivyosema wenzangu kiwanda hichi kina historia kubwa, huko miaka ya nyuma kilikuwa kinaendeshwa na Serikali, na watu wengi wa Mkoa wa Kaskazini wakiwemo wazee wangu wa Chaani walipata ajira kubwa sana katika kiwanda hichi cha Mahonda. Nilipokuwa mdogo nina kumbukumbu kuna magari makubwa yale yalikuwa yanaitwa magari ya Mchina yanapita na yanakuja kuwabeba wazee wetu wanakwenda katika kiwanda cha Sukari cha Mahonda kwenda kufanya kazi.

Kiwanda cha Mahonda kilikuwa ni kielelezo kwa Mkoa wa Kaskazini, watu wa Kaskazini walikuwa wakifurahia sana kiwanda kile kwa sababu ilikuwa ni sehemu ya watu kupata riski zao na kuendesa maisha yao, kwa bahati mbaya sana katika miaka ya katikati hapo kiwanda kile tulipata taarifa kilikuja kupata hujuma kubwa sana, matokeo yake kiwanda kikafariki, maana yake kilifika pahala kikawa hakifanyi kazi. Baada ya hapo yale mashamba ya miwa baada ya kuona muda mrefu yamekaa wananchi wakaomba walime na Serikali kwa kuwa kitu kikubwa ni kuwajali wananchi wake, mashamba yale walipewa wananchi kwa muda ili walime mpaka pale kiwanda kitakapokuja kufanya kazi mashamba yale yarudi kwa ajili ya kiwanda.

Sasa Mhe. Naibu Spika, Baada ya miaka hiyo kupita tumshukuru sana muwekezaji huyu kwa kuonyesha moyo wa kutaka kusaidia uchumi wa Zanzibar na akaja kuwekeza katika kiwanda cha Sukari cha Mahonda. Kulikuwa kuna changamoto za hapa na pale, serikali iliingilia kati zikarekebishwa. Hivi sasa kiwanda tayari kimeshaanza uzalishaji wa sukari, sasa tayari yameanza kujitokeza matatizo ya hapa na pale. Matokeo 16 kwa kiwanda kimoja kuchomwa moto, jambo ambalo ni lazima sisi kama wasemaji wa wananchi, Wawakilishi wa wananchi na wasimamizi wa shughuli za serikali lazima tufike pahala tujiulize kuna nini? Kama hatukujiuliza kiwanda hichi kitaendelea kuchomwa, miwa itaanza kuchomwa na mwisho kitakuja kuingiliwa kiwanda chenyewe kichomwe kabisa kiwe hakipo.

Mhe. Naibu Spika, zipo sababu nyingi, Mhe. Muhammed Said (Dimwa) yeye katika mapendekezo yake alieza zaidi katika masuala ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, hili kwa kweli ni jambo la muhimu. Mradi wowote unapofanyika kwanza kunatakiwa ifanyike *EIA* na hii inaeleza yote mpaka matatizo ya wananchi, changamoto za wananchi na nini kifanyike ili mradi

wende vizuri. Sasa hapa sijui hii *EIA* kama itaangaliwa, kama iliwahi kueleza kuna changamoto zishughulikiwe na kama zimeweza kushughulikiwa kwa wakati. Inawezekana tukawa tunaangalia tulipoangukia, lakini tukashindwa kuangalia pale ambapo tulipojikwaa.

Mhe. Naibu Spika, kuna watu wa Mahonda niliwahi kukaa nao wanasema kwamba, zamani kilipokuwa kiwanda kile kilikuwa kinashughulikiwa na watu wa China, walikuwa wanasema kwamba Wachina walikuwa nakwenda mpaka vijijini kwao mitaani, wanakaa kitako wanakula viazi kwa mboga, Wachina wa kiwanda kile cha Sukari cha Mahonda. Kwa maana hiyo inaonyesha kulikuwa kuna mashirikiano makubwa baina ya wananchi wa maeneo yale, lakini na vile vile na wawekezaji wenyewe. Sasa inawezekana na ndio maana hapa hiyo Kamati ya Ulinzi na Usalama kwanza wajaribu kuangalia ile *EIA* kabla ya mwekezaji kupewa kiwanda, halafu aweze kushauri nini cha kufanya.

Mhe. Naibu Spika, chengine labda kwa kuwa serikali ipo hapa watwambie, je, katika ule mkataba wa kiwanda cha sukari cha Mahonda unasemaje yanapotokea matatizo kama haya. Je, inapotokezea kiwanda au mashamba ya miwa kuungua moto nani pale anatakiwa kuwajibika ni Bima au serikali. Inawezekana pengine mtu akaona mambo yamekwenda vibaya akaona atengeneze utaratibu ili aweze kupata fedha kwa ajili ya kuendesha au kiimarisha kile kiwanda chake. Mikataba hii wakati mwengine inatoa *loophole* pengine kwa muwekezaji kuweza kufanya mambo ambayo yakaibebesha mzigo serikali.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani ni suala muhimu kabisa liweze kuangaliwa nini hasa tatizo. Ndio maana nikasema mwanzo hebu uiangalie *EIA* inasemaje halafu tuuangalie na mkataba wa Kiwanda cha Sukari cha Mahonda unasemaje.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala la kushauri. Mimi nashauri Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa lakini vile vile kama alivyosema Mhe. Simai, kupitia Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kama haipo Tume au kamati basi iundwe kamati maalum akiwemo Mwakilishi wa jimbo hilo husika. Mwakilishi anakuwa anaguswa na mambo mengi, anapata taarifa nyingi kutoka kwa wananchi. Nadhani na yeye kwa kuwa ataona ile kile kiwanda kile faida kwa wananchi wake naamini ataweza kutoa ushirikiano mkubwa katika hilo.

Lakini chengine Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna suala la malalamiko la wananchi wale ambao mwanzo walipewa yale mashamba baada ya kwamba miwa halimwi na mashamba yale sasa hivi wamenyang'anywa yamerudi tena serikalini na kurejeshewe muwekezaji wa kiwanda cha Sukari cha Mahonda.

Sasa je, hawa yale malalamiko yao zile changamoto zao zimewahi kushughulikiwa kwa sababu vyenginevyo unaweza ukaja ukampiga ng'ombe wa nyuma kumbe anayechelewa kwenda ni ng'ombe wa mbele. Sasa kama kilio hichi cha wananchi hakijasikilizwa na kushughulikiwa, basi mimi naamini pengine moja katika *source* ya haya matatizo inawezekana na wao wakawa wameguswa vile vile.

Mhe. Naibu Spika, chengine nataka nizungumzie kuna malalamiko vile vile ya wananchi kuhusu maji ambayo yanayotiririka kutoka kiwanda kile Mahonda inaonesha kuna *polution* ambayo inasababisha maji ya mto hasa ule mto uliokuwepo Mahonda, pengine ni moja katika hicho chanzo cha hayo matatizo. Ndio maana nikasema yajaribu kuangaliwa mambo kwa upeo mkubwa ili lisiangaliwe tu suala moja la kuchomwa miwa kwa shamba la Kiwanda cha Sukari cha Mahonda, lakini vile vile lishughulikiwe na hilo tatizo jengine la uharibifu wa maji ambayo wanayotumiwa wananchi vile vile.

Kwa kumalizia mimi naunga mkono yale mapendekezo ambayo ametoa Mhe. Muhammed Said (Dimwa). Lakini vile vile na sisi kwa upande wetu na hasa serikali wajaribu kuangalia ni namna gani tunaweza kuvilinda hivi viwanda vyetu kama alivyosema mwenzangu Mhe. Simai. Leo viongozi wetu tunawaona wanahangaika dunia nzima hawalali makwao wanakwenda kuhangaika kutafuta wawekezaji hasa waje wawekeze katika sekta ya viwanda. Sasa kama kuna watu wamejitokeza wamekubali wito wetu, wamekuja leo kila siku yanajitokeza matatio kama haya, je, hao wangine watakuwa na moyo wa kuja. Hilo mimi nafikiri ni jambo muhimu sana ni lazima tulizingatie na tuliangalie.

Mhe. Naibu Spika, kibaya zaidi Zanzibar katika miaka ya kati kati miaka ya 70 na 80 tulikuwa tuna viwanda vingi hapa, lakini kila kimoja kilianza kufa kifo cha kiofisa na *tie* shingoni kidogo kidogo, tulikuwa tuna kiwanda cha kutengeneza vitambaa Karakana, tulikuwa tuna kiwanda cha kutengeneza magodoro, kiwanda cha Soda Maruhubi, kiwanda cha sigara, kiwanda cha kutengeneza sabuni (Manukato), kiwanda cha viatu, vimekufa kidogo kidogo. Leo watu wanakuja kufufua viwanda sisi viwanda vile tunavitengenezea mazingira ya kufa.

Mimi nadhani Wazanzibari lazima ifike pahala kama kushiba siasa basi Wazanzibari tumeshavimbiwa bado kupasuka tumbo tu, sasa hivi twende kwenye uchumi, twende katika viwanda, hakuna uchumi uliokuwa imara, uchumi ambao huwezi ukatetemeshwa na mtu yeyote kama utaimarisha viwanda katika nchi yako, vijana watapata ajira kutakuwa hakuna

manung'uniko. Lakini leo kama tutakuwa tunauwa viwanda, tutaendelea kula siasa mpaka ifike pahala siasa itupasuwe tumboni, tufe sote moja kwa moja.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na namshukuru sana Mhe. Muhammed Said (Dimwa), endelea kuumiza kichwa chako, endelea kuangalia changamoto, lete hoja sisi tutazichangia na kwa kweli tutaunga mkiono na tunaomba sana serikali yetu iwe sikivu kwa Waheshimiwa wanavyojituma wanapoleta mawazo yao na nyinyi muweze kuyafanyia kazi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nami niungane na wenzangu baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nimshukuru sana Mhe. Muhammed Said, kwa kueleta hoja hii muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Lakini pili niwashukuru sana wawekezaji walikuja kuwekeza katika nchi yetu na hasa kama tunavyofahamu sasa hivi viwanda vikubwa tulivyonavyo ni Kiwanda cha Maziwa na Kiwanda cha Sukari ni miongoni mwa viwanda vikubwa sana tulivyonavyo katika nchi yetu, kwa hivyo, nataka niwapongeze sana.

Mhe. Naibu Spika, nilitaka kwanza niseme ya jumla, kwanza ni vizuri tukafahamu wajibu wa serikali na wajibu wa muwekezaji. Wajibu wa serikali kwanza ni kutengeneza Sera za uwekezaji na ndio maana tunacho chombo chetu kinaitwa *ZIPA* chenyewe ndicho kinaratibu uwekezaji wote unaokuja nchini. Sasa mtu akishapitia *ZIPA* pale basi yapo mambo ambayo anaelekezwa na anatekeleza kwa mujibu wa sheria iliyopo ya uwekezaji.

Moja ambalo nataka niliseme nikwamba muwekezaji mwenyewe ndiye mwenye wajibu wa kulinda rasilimali yake yeye mwenyewe kwanza anayoiwekeza, ukenda kwa wachimbaji madini kule kwenye makampuni makubwa ya madini yana kampuni zao za ulinzi, wana kila kitu na wanafanya utaratibu wa ulinzi wao wenyewe, wanakichomoza hesabu zao ni wao wenyewe. Serikali wajibu wake ni kutoa ulinzi wa jumla huwo ndio wajibu wa serikali yoyote duniani. Katika maeneo ya uwekezaji yoyote ni muwekezaji mwenyewe ndiye anayetakiwa a-*provide* ulinzi wa eneo lake na ndio maana serikali katika kushughulikia matatiza ya Kiwanda cha Sukari.

Kwanza nataka niseme kama kuna chombo ambacho kimepewa fursa kuja serikalini kila wakati na kupewa msaada wa hali na mali ni kiwanda cha Sukari. Jana Waheshimiwa walikuwa Ofisini kwangu mimi, kaondoka kwangu akenda kwa Katibu Mkuu na matatizo mengine ambayo tunayo tuna-*deal* nayo. Sasa niseme kama ni msaada, kama ni ushirikiano ni mkubwa kabisa hawajapata

hata siku moja kuwa hawakupata fursa ya kuonana ama na Makamo wa Rais au Waziri yeyote, Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko sijui mara ngapi keshafika, kipa pahala na barua zao kila wakati zipo zinakuja, yapo maelekezo tunayatoa kwao na wao wanawajibu wa kuyatekeleza ambayo tunawapa.

Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo moja ambalo nataka niliseme kwamba, yapo maelekezo tumewapa, kwa mfano Wajumbe wengine hapa wamesema suala la *management* ya shamba lenyewe. Shamba la miwa au shamba lolote lina utaratibu wake wa kuliendesha, ukiangalia mashamba yale hayana utaratibu mzuri, zamani kulikuwa na vibanda virefuu vya walinzi, leo vipo kwa sababu muwa ni sehemu kubwa sana, kwa hivyo, zamani wamejenga vibanda wakati wa Wachina na hata ukenda mashamba ya miwa kuna mlinzi kule juu anaangalia mtu anaepita huku na huku, leo kaangalie shamba zima humkuti mtu yeyote pale.

Walitakiwa katika kila sehemu ya shamba kuwe na sehemu ya kuweka moto unapotokea kuna kitu cha kuzuia *Fire brackets* kwa zoezi zile hakuna. Sasa haya ni mambo ambayo tumewaelekeza kufanya na wao wenyewe hawafanyi. Sasa lazima tutizame *role* ya muwekezaji ni ipi na *role* ya serikali ni ipi, hili ndio jambo moja ambalo mimi naliona lina kasoro.

Mimi nawashukuru sana kwamba wamefanya *investment* kubwa sana kwenye kiwanda chenyewe, *no doubt about it*, katika kiwanda wamefanya kazi kubwa na kila mmoja ana *appreciate*, lakini tumewaelekeza na kwenye mashamba na wao wafanye *management*, mto umekauka, tukawaambia fanyeni *irrigation system* hapa ili muzalishe angalau mara mbili, tatu, haifanyiki, matokeo yake linatokea jua kali, maji hayapo, moto utatokea tu utaunguza. Tunasema hapo yapo mambo ambayo tumewaelekeza wenzetu wafanye, mimi ningewaomba kabisa na wenyewe wafanye.

Mhe. Naibu Spika, jengine Kamati za Ulinzi na Usalama zimekutana sana za Mkoa za Wilaya na wametoa maelekezo. Mimi ningeshauri sana Mhe. Muhammed Said, ungesaidia, yale maelekezo ambayo yametolewa kwenye Kamati za Ulinzi na Usalama tungetegemea kwenye waraka wako na wewe yawepo, kama umetafiti vizuri, yapo maelekezo yametolewa kwenye Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na za Mkoa na Taifa lenyewe, maana hata kama ya Kitaifa iliundwa katika jambo hili, lakini maelekezo hayo hayapo. Sasa huu waraka una mapungufum hilo la kwanza, hili ni pungufu kubwa sana kwa sababu huwezi ukafanya jambo ambalo ukafanya nusu na nusu ukaliacha. Umesema moja ni zuri tu na wala hatuna ubishi nalo ni jambo jema tuhakikishe ulinzi, lakini na wao *role* yao ni ipi?

Mhe. Naibu Spika, *role* ya kwanza tumekaa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, moja waliyoelekezwa ni mashirikiano yao na watu waliokuwepo pale, suala la ajira la watu wa pale, je, watu wanaajiriwa kama tulivyotaka, mikataba iko wazi, wameleta mikataba kwetu tumewarudishia ina matatizo, tumewambia kairekebisheni, hayajarekebishwa, mnafanyaje?

Kwa hivyo, nasema matatizo haya yapo pande zote mbili, mimi nakubali kabisa lakini wao wanayo *role* kama wawekezaji kuwekeza katika suala zima la ulinzi. Takwimu hizi Mhe. Mwenyekiti, zilizotolewa hapa, ukifanya hesabu haraka haraka maana yake ni kwamba hekta moja imegharimu moto si chini ya bilioni moja, haiwezekani! Hakuna hesabu hiyo hata kidogo na mimi ninayo a,b,c,d, kidogo ya hesabu. Haziwezi zika-*differ* kiasi hicho, kwa hivyo, hapa kuna matatizo ya kimsingi yanahitaji kutatuliwa. Kuna suala zima la Bima watuulize hawana Bima kama wanabima, je, Bima imewalipa haikuwalipa. Hizo ni *areas* nyingi tu ambazo nilitaka maswali ambayo yaulizwe na yapatiwe majibu.

Kwa hivyo, mimi nasema Mhe. Naibu, moja ambalo nalisema ni kwamba, suala la serikali la kutaka wawekezaji wawekeze kabisa kabisa tunawakaribisha, masharti yapo, sheria zipo na kanuni zipo na *role* ya serikali ya jumla ya ulinzi nakubali kabisa lazima tuifanye. Lakini nadhani nikubaliane na Waheshimiwa Wajumbe kwamba kunahitajika kwenda kwa kina zaidi kama serikali. Baada ya kupata hii hoja tuliyoipata sasa hivi tukakae na twende kwa kina zaidi ili tuliarifu Baraza hii tukufu maeneo ambayo serikali imeshughulikia na maeneo ambayo muwekezaji mwenyewe hajayashughulikia, tuliarifu Baraza rasmi. Vyenginevyo, tutaondokana na habari nusu nusu, ili kuondoa habari nusu nusu, sisi tukae kitako na tuje na habari zote za serikali ambazo tumezifanya na yote ambayo muwekezaji kaelekezwa kufanya na hajafanya. Mimi nafikiri hapo tutakapofika ndio tutaweza kupima nani anasema jambo sahihi, hili ni jambo moja ambalo nataka nalo tuliseme.

Mhe. Naibu Spika, nataka nikubali jambo moja siasa ya sukari Tanzania ipo, Bara kule miaka yote wameshindwa kuzalisha zaidi ya tani laki nne kwa sababu wanaagizia sukari wasingependa kuviona hivi viwanda vya sukari vinakua, tunavijua vita hivyo vipo na vya kweli kabisa kabisa.Tunahitaji kuwasaidia wenzetu hawa wawekeze, wazalishe na waingie kwenye soko vizuri. Na sisi tunasema kama ni viwanda vya serikali tupo tayari. Lakini nasema shilingi ina pande mbili, sisi kwa wajibu wetu tutatekeleza na wao watekeleze wajibu wao. Wafanye *investment* waliofanya kwenye kiwanda, wafanye *similar investment* kwenye mashamba yenyewe waone kama serikali haitashiriki.

Mhe. Naibu Spika, nitakupa mfano mmoja, sisi tumewaelekeza waweke umwagiliaji maji ambao utasaidia kuzalisha kutoa angalau tani 78 mpaka 79 kwa hekta, hawajafanya, kwa hivyo, wanangojea mvua tu, kwa hivyo, ikifika msimu wa mvua hawakulima ni tatizo kwao. Sasa kwenye *Sugar Industry* kama hii huwezi ukangoja mvua, *that's no way* ukaendesha kilimo kwa kutegemea mvua, kilimo kinaendeshwa kwa kutegemea *irrigation system*, ndio zaidi hawataki kuifanya hii. Sasa hili ni tatizo la msingi, kwa maana hiyo sasa watadai ardhi zaidi na ardhi watakayokwenda kudai pengine watakwenda kuomba mkopo ili kusaidia kwamba una ardhi.

Lakini sisi tunataka ardhi itumike na ndio tatizo tulilonalo la wakulima kule. Wakulima wanataka waingie kwenye *contract* lakini wanasema basi tuondokane na kilimo tunacholima sasa hivi, tuingie kwenye kilimo cha kisasa, chenyewe nacho ni tatizo. Kwa hivyo, nasema haya ni mambo ya msingi tunahiji tukae kitako kwa pamoja sote tuone nani ana kasoro gani, lipi tulisahihishe kwa pamoja, lakini serikali nakuhakikishieni kabisa kama kuna watu tumekutana nao mara mia zaidi ni watu wa uzalishaji wa sukari mpaka *main top management* yake nimeshakutana nayo, kila siku tanakutana nao, lakini kuna mambo tunawaambia hili kalitekelezeni, tuambiwe wamelitekeleza, hakuna, hili mmelitekeleza, hakuna.

Mhe. Naibu Spika, unafika pahala unakwama. Lakini nasema tena suala la ulinzi kwa ujumla wa kiwanda na shamba lenyewe ni suala la kampuni yenyewe. Ulinzi wa jumla ya nchi ni suala la nchi, hakuna hata serikali moja duniani inakwambia kwamba walinzi hawa wakakulindie kiwanda chako, *you provide them, you pay them*, na ndio maana serikali ikawaambia kashirikianeni na vikosi vyetu vya Ulinzi na Usalama walipeni fedha kidogo waweze kuwalindia, hawajafanya mpaka leo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, serikali inawaambia vikosi vipo vya SMZ kachukueni vijana pale, walipeni pesa kidogo, tena hawakuwambiwa wwalipe mshahara, walipeni pesa kidogo tu kwa kuwasaidia mafuta na kadhalika ya kuweza kufika kazini kwao ili waweze kuwahudumia pale, hawajafanya. Hivi serikali ingefanya nini zaidi ya hilo. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, na mimi pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Muhammed Said (Dimwa), kwa hoja yake aliyoileta binafsi inayohusu kiwanda hiki cha sukari Mahonda. Lakini pia naomba nitambue michango ya wenzangu wote waliochangia katika hoja hii.

Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inathamini sana mchango wa wawekezaji wa Kiwanda hiki cha Sukari cha Mahonda, tunathamini sana na Serikali tumejitahidi kama Serikali kwa uwezo wetu kulishughulikia suala hili sio tu la hujuma hizi zakuchoma moto, lakini pia kuona kwamba kiwanda hiki kinasimama na kinatoa huduma na kinafanya mchango ambao unatakiwa ufanye kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia katika orodha hii ya moto iliyotokea, huu wa mwisho uliofanyika mwezi wa Agosti ulitushtuwa sisi wote kwa sababu hakuna anaependa katika Serikali kuona mali za wawekezaji zinaharibiwa kama hivi kwa sababu sio nia kabisa na madhumuni ya kuwaita wawekezaji na kuwataka wawekeze katika visiwa vyetu vya Zanzibar. Baada ya moto ule kikao kiliitwa na kilisimamiwa na mwenyewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Kama walivyosema wenzangu hasa Waziri wa Kilimo. Kikao kile Mhe. Naibu Spika, mambo mengi yalikubaliwa na yaliamuliwa kwamba pande zote mbili mambo yale wayafanye. Kwa bahati mpaka sasa hivi kwamba hakujatokea hujuma nyengine, hiyo inaonesha kwamba kuna mambo ya msingi yalifanyiwa kazi na kuna mengine ambayo hayajafanyiwa kazi. Nilikubaliana tu na Mhe. Waziri wa Kilimo kwamba, kuna majukumu ambayo yanatakiwa wenye kiwanda hiki wayafanye na kuna majukumu ambayo wakitakiwa Serikali kwa kushirikiana nao tuyafanye.

Serikali kama tulivyokuwa tumetia katika Sheria yetu ya *ZIPA* tunatoa ulinzi wa jumla kwa sababu ni miongoni mwa ahadi tunayotoa kumwambia muekezaji, ukija ukiekeza Zanzibar, Serikali itakuhudumia mambo yafuatayo, ambayo yakiwemo na mambo vile vile ya kuwapatia ulinzi wa mali zao na ulinzi wa wao wenyewe kwa usalama wao.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna mambo ambayo muekezaji anatakiwa na yeye afanye kwa sababu sio tu ya Kiwanda hiki cha Sukari, lakini hata wenye mahoteli pia katika masuala ya ulinzi wanajihudumia wenyewe. Kwa sababu ulinzi sasa hivi umekuwa ni rahisi na umekuwa ni kazi, unaweza kupata kazi ya ulinzi kwenda kwa kampuni binafsi na kadhalika. Tuliwaelekeza hawa mengi tu lakini wawekezaji hawa hawajakamilisha. Kamati za ulinzi za Mkoa, za Wilaya, tulikaa nao kikao wakatufahamisha yote na wakaeleza matatizo yote yaliyopo pale na ndio maana wakawa wanawasubiri wawekezaji hawa ili waende wakamalizane ili hii kazi iendelee vizuri.

Kuna ulinzi wa muda mfupi na ulinzi wa muda mrefu ambao pamoja na wao kujenga hizo *towers* za kuwaweka walinzi, kujenga maeneo ya kuwaweka

walinzi kuweza kukaa, wakaweza kubadilishana zamu na kadhalika. Haya yote Mhe. Naibu Spika, nayasema kwamba yalizungumzwa na yakakubaliwa pande zote mbili, kwa hivyo, ni vizuri tu wajumbe wakaelewa kwamba Serikali hatujakaa kwamba tumeliachia hili suala, lakini hatua tumezichukua na utekelezaji wake umeanza lakini nyengine ilikuwa pande hii ya wawekezaji walitakiwa wafanye.

Mhe. Naibu Spika, katika mjadala huu yalizungumzwa mambo mengi kuhusu viwanda. Naomba niwahakikishie wajumbe, Mhe. Naibu Spika, na wananchi wote, wananchi wetu wanaotusikiliza kwamba Serikali inajiandaa vizuri sana katika suala zima la viwanda. Sasa hivi hata katika mpango unaotayarishwa, mpango wetu tumetoka na MKUZA II, tunaingia mpango mwengine ambao utakuja katika bajeti inayokuja, tunajipanga kwa kuwa na viwanda ambavyo muhimu katika dhana nzima ya mnyororo wa thamani.

Kiwanda hiki cha Sukari ni kiwanda kimojawapo ambacho kinaingia katika viwanda kwenye dhana ya mnyororo wa thamani. Kwa sababu Kiwanda cha Sukari Mhe. Naibu Spika, faida yake inapatikana katika maeneo mbali mbali. Kwa mfano suala la ajira, Kiwanda cha Sukari katika kipindi cha kutengeneza sukari wakati wanavuna miwa na sukari wanaajiri wafanyakazi zaidi ya 700 ambao wanafaidika sio tu wa Kaskazini na wanafaidika na watu wengine ambao wanatoka maeneo yale.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, kiwanda hiki kina uwezo wa kusaidia hata nishati ya umeme kwa sababu wao wenyewe wanatengeneza nishati ya umeme kinaweza kuwasaidia wananchi wa pale. Pia, kiwanda mwaka huu peke yake ndio wameanza kuanza uzalishaji wamezalisha sukari zaidi ya tani elfu nne. Mhe. Naibu Spika, hiyo peke yake inatuwezesha wananchi kwa kipindi fulani kuwa na sukari ya uhakika na sukari iliyokuwa safi. Kiwanda kimewarahisishia, mimi mwenyewe binafsi nimekwenda kuwapa hati wafanyabiashara wa eneo lile na maeneo ya Kaskazini na maeneo mengine ya Kati ambao wameweza kununua sukari kutoka kiwanda kile na wakawa wanauza biashara hii ya sukari katika maeneo yao, kimewapatia faida wananchi wetu.

Kiwanda hiki vile vile Mhe. Naibu Spika, wana utaratibu wa kutaka kuuza sukari ya kilo ndogo ndogo, hiyo pia inawasaidia hata wafanya biashara walioko majumbani hasa akina mama wanauza bidhaa, maduka madogo madogo majumbani. Kiwanda hiki Mhe. Naibu Spika, kinaweza pia kutoa vyakula vya wanyama, zamani ndio tulinunua *molasses* kutoka Bara sasa hivi

kuna *molasses* ya kutosha pale ambayo inatuwezesha kuimarisha tena kiwanda chetu cha vyakula vya wanyama.

Kiwanda hiki Mhe. Naibu Spika, kuna lita zaidi ya 250 ya *spirit* ambayo kuna mradi ulikuwepo huko nyuma wa kufanya majiko ya kisasa ya kinamama, tumezungumza na muekezaji huyu aliyeko kule anataka kuja kufufua tena mradi huu wa kutengeneza majiko ambayo yanawafaa sana akina mama kwa sababu majiko ambayo hayatoi *gas* za hatari kama majiko ya *gas* wala hakuna mashindikizo mengine. Tatizo lililokuweko huku nyuma kwamba watu walikuwa wakitumia hii *spirit* kwa kunywa, lakini sasa hivi utafiti umefanyika hii *spirit* tena hainywiki kwa sababu imetiwa sumu ambayo inamfanya mtu akinywa asiweze kuimeza.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, kiwanda hiki kinatoa mafuta mazuri ambayo walikuwa wakifanya zamani. Sasa hivi tunazungumza na wawekezaji kuanzisha tena mradi mwengine wa mafuta mazuri. Pia, Mhe. Naibu Spika, nilisikia hoja kwamba kuna wakulima ambao walikuwa wakikaa wakilima katika maeneo ya Kiwanda cha Sukari. Natilia mkazo na Wizara ya Kilimo kuwa na utaratibu wa kilimo cha miwa ili wakulima hawa waweze kulima miwa wapate tija. Nimetoa mimi nilipokwenda kutembelea kiwanda cha sukari, fedha ambazo zilikuwa wamelipwa wakulima wa mwanzo, lakini pia wamepewa Shahada kwamba wamefanya kazi nzuri.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ninachohisi mimi labda elimu ni ndogo kwa wenzetu wanaoishi Kaskazini, lakini elimu ni ndogo hata kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa nini nasema hivyo, kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kama niliposema pale mwanzo viwanda hivi ambavyo vimo katika dhana mnyororo wa thamani huko mbele ndio ambako tunakoelekea. Kwa mfano Kiwanda cha Makonyo Pemba, kiwanda kile kitaweza kuwahudumia vile vile wakulima, wafanyabiashara wadogo wadogo na kadhalika, na hiyo hiyo tutajifunza kutokana na tunavyoendeleza kiwanda hiki cha sukari.

Mhe.Naibu Spika, Kiwanda cha Maziwa cha Bakharesa ambacho nacho kinatakiwa kiwe ni kiwanda cha thamani kwa ajili ya wakulima wetu na wafugaji wetu na wale ambao sasa hivi wanajifundisha kutengeneza siagi, kutengeneza maziwa mgando, kutengeneza maziwa, *ice- cream* na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, Kiwanda cha Mwani huko mbele tunataka tutengeneze viwanda vya mwani, tumeshapata viwanda viwili vya mwani ambavyo navyo vitasaidia kufungua milango kwa wananchi wengine. Kama nilivyosema hizi dhana na hii tunabidi sasa kama Serikali tuwaelimishe wenzetu, wananchi wetu

wajue kwamba hivi viwanda vya wawekezaji na wao wana tija na vile vile na wao ni walengwa. Lakini pia na wao wanatakiwa wajue kwamba hii ni mali yao kwa sababu inawafaa wao na inawafaa watoto wao na inatufaa kwa taifa zima. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tuna maslahi makubwa sana na viwanda hivi na kuvilinda viwanda kama hivi tunatakiwa sisi wananchi wote wa Zanzibar tuweze kuvilinda viwanda kama hivi.

Mhe. Naibu Spika, hii hoja imekuja...

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa hoja hii hatujamaliza na lengo ni tuimalize mchana huu sasa ningemuomba Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atengue kanuni ya muda ili tuweze kumaliza hii hoja na baada ya hapo wengi wameniuliza hapa wanaleta vikaratasi uchaguzi kama utafanyika, uchaguzi utafanyika na baada ya kufanyika uchaguzi tutaahirisha kwa ajili ya kwenda kwenye semina. Mhe. Waziri karibu.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa katika orodha ya shughuli za leo bado tunaendelea nazo hususan hoja hii ya Mhe. Dimwa, ambayo iko mbele yetu na kwa kuwa muda uko mbele yetu, kwa hivyo, naomba niliombe Baraza lako tukufu tuweke kanuni ya muda kando ili tuweze kumaliza shughuli zilizo mbele yetu kama tulivyozipanga.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Sasa nitawahoji wale ambao wanakubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, nilikuwa karibu ninamalizia hoja yangu niseme tu kwamba Mheshimiwa, hii hoja iliyoletwa sasa hivi, ukiitizama kwa upana wake na wale ambao wanatusikiliza nje na kwa sababu Serikali tumo mbioni kuwashajihisha wawekezaji kwa sababu Sheria za viwanda tunataka tuzirekebishe, Sheria za Viwanda Vidogo Vidogo zitarekebishwa na vile vile kupanga vizuri viwanda vya aina gani na vipi ndio tunamalizia. Kwa hivyo, hili suala kwa sababu linazungumzwa halituletei sifa nzuri Mhe. Naibu Spika, kwa sababu

wawekezaji wanatizama kiwanda hiki kwa kiasi gani Serikali tutamaliza matatizo yao haya na wataweza na wao kuendelea waweze kufanya vizuri vile ambavyo wamejipangia.

Mhe. Naibu Spika, kwa misingi hiyo ni vizuri hili suala la moto ni suala dogo lililokuja hivi la juu, lakini tuangalie masuala yote yanayohusu kiwanda hiki, kama alivyosema Waziri wa Kilimo, kwa sababu kiwanda hiki kinazalisha sukari mara moja tu kwa mwaka. Kuandaa kiwanda hiki kizalishe sukari mwaka mzima nini kifanyike. Kwa hivyo, tuna wajibu wa sisi kama Serikali kuwahimiza na kuwasimamia lakini na wenyewe wawekezaji wana wajibu vile vile kufanya kazi yao na kujipanga vizuri kwa mujibu wa utamaduni na utaalamu na hali halisi tunaotakiwa. Tukifanya hivyo Mhe. Naibu Spika, kiwanda hiki kitakuwa ndio kiwanda cha mfano na viwanda vyengine ambavyo nimevitaja na vyengine ambavyo viko njiani kuja vitawaangalia hawa jinsi wanavyoendeleza vizuri.

Mimi Mhe. Naibu Spika, ningewaomba *management* hii wawe na imani kwamba Serikali tumejitahidi na tuko nao pamoja, tunazungumza nao saa zote wanapokuwa na matatizo yao. Lakini na wao watusikilize kama Serikali, kwamba tunapokuwa tunawashauri na wao ushauri wetu watusikilize ili tuweze kufika mahali ambapo kiwanda hiki kitakuwa kiwanda cha mfano na kitaweza kuchangia sehemu kubwa ya taifa letu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kusema kwamba huu ni mfano ambao itabidi tuufanyie kazi ili mwakani kiwanda hiki nacho kiweze kuingia katika *list* ya viwanda ambavyo vinatuletea mapato makubwa nchini petu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na majadiliano, nilimuomba Mhe. Said Soud, lakini nimeshamuomba radhi kwa sababu ya muda, kwa hivyo, sasa nitamkaribisha Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Khalid, na mchangiaji wa mwisho atakuwa Mhe. Mohammed Aboud Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini la pili, nimshukuru Mhe. Dimwa kwa kuleta hoja hii. Lakini vile vile niungane na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali waliochangia na hasa Mhe. Waziri wa Kilimo, Mhe. Waziri wa Biashara, Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame na Mhe. Rashid Makame Shamsi. Mazungumzo yangu hayatokwenda mbali na yale waliyoyazungumza

wao kwa hivyo, nitakuwa *very brief* Mhe. Naibu Spika, na nitakwenda moja kwa moja kwenye *points* ambazo nilikusudia kuzichangia.

Ya kwanza kabisa Mheshimiwa, nina hoja ya hii *title* ya hoja yenyewe, kwa sababu ilivyoandikwa hapa ni hoja binafsi kuhusu matokeo hatarishi katika sekta ya uwekezaji ya viwanda. Ningemuomba sana Mhe. Mjumbe, akaiangalia hii *title* yake kwa sababu ni pana, wakati suala tunalolijadili ni hoja ya moto katika mashamba ya miwa. Mhe. Shamsi, alisema vipo viwanda ambavyo havijawahi kupata hujuma hizi, wala hawajawahi kudai ulinzi wa Serikali. Sasa ni suala ambalo liko *specific* kwa Kiwanda cha Mahonda, yaani Kiwanda cha Sukari, lakini *specific* kwa suala la mashamba.

Naungana sana na Waheshimiwa wote Wajumbe waliozungumza kuhusiana na suala la kutafuta kiini cha tatizo hilo. Lakini niseme tu Mhe. Naibu Spika, Serikali iliiliona hili na iliundwa Kamati Maalum ya watu wazito sana ndani ya Serikali, kukaa na wenzetu hawa, lakini pia kufanya tathmini ya kujua nini hasa kiini cha matatizo hayo. Kamati ilifanya kazi ya kuonana nao, ilifanya kazi ya kutembelea kiwanda kile, ilifanya kazi ya kuonana na Kamati za Ulinzi na Usalama na yako mapendekezo mengi yaliyotolewa. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, kayazungumza hapa, yalitolewa mengi, ikiwemo suala moja la kwamba wao wenyewe wana wajibu wa kuimarisha ulinzi wa mashamba yao.

Mimi niwapongeze sana wamefanya kazi kubwa sana katika kiwanda kwa maana ya kukifufua, kuweka mashine mpya, mimi mwenyewe nimepata nafasi ya kutembelea na nimeona *investments* walioifanya. Lakini kwenye upande wa mashamba Mhe. Naibu Spika, na hili tumeshawaeleza mara nyingi sana. Mimi nimeshakutana nao mara nyingi kwamba bado wanahitaji kufanya kazi zaidi kwenye mashamba. La mwanzo ambalo mimi mwenyewe niliwashauri, kwamba wahakikishe pia hata zile mbegu wanazotumia basi ziwe mbegu ambazo zina uzalishaji mkubwa. Tuna mifano mingi, bahati nzuri niliwahi kutembelea mashamba ya miwa ya Swaziland na Kiwanda cha Swaziland, miwa yao sio miwa unayoikuta Mahonda, kwa maana ya *thickness* ya muwa wenyewe, lakini na *quality* ya sukari iliyomo mule ndani. Hapa sisi *variety* tunazotumia sijui kama wao wenyewe wataalam zaidi, lakini miwa membamba sana inaonekana kwamba zile *practices* za kwenye miwa haifatwi.

Mhe. Hamad, hapa alizungumza masuala ya *irrigation*, masuala ya mbolea, masuala ya kupalilia hata hayo mashamba yenyewe, mashamba mengine yako kwenye mwitu mwingi sana na imekuwa kama kichaka cha miwa, ukiwa na kichaka cha miwa ni *source* kubwa ya kuingia moto, hiyo ndio hali ilivyo. Sasa

kiwanda wamefanya kazi kubwa sana, lakini kwenye mashamba bado kuna haja ya kufanya kazi hiyo, lakini pia tuliwashauri. Mhe. Amina, kasema wajenge minara ya ulinzi.

Lakini jengine tuliwashauri waweke zile njia ambazo zitazuia moto kuvuka kutoka eneo moja kwenda kwenye eneo jengine, yaani *fire breakers*, hayo yote wameelezwa, lakini pia tumewashauri kwamba waweke ikiwezekana *camera* za *CCTV*, zote wameshaambiwa. Lakini jengine pia waliambiwa wafanye na mawasiliano na watu wa vikosi ili wawe na makubaliano ya kuwasaidia katika masuala ya ulinzi. Sasa Mhe. Naibu Spika, haya yote hayajafanyika kwa upande wa wenzetu hawa.

Hoja hii iliyoletwa na Mhe. Dimwa, Mhe. Waziri wa Kilimo kasema kwamba, pamoja na kusikiliza upande mmoja ilikuwa pia wapite kuja kusikiliza upande wa pili wa Serikali na haya ambayo tunaeleza hapa pengine tungekwisha mueleza Mheshimiwa aliyeleta hoja hii napengine angefikiria vizuri zaidi ya jinsi ya kuiweka hoja yake. Lakini Mheshimiwa pamoja na hayo sheria ipo, Sheria ya vitega uchumi ya mwaka 2004 ipo na inaelezea utaratibu mzima na *insentive packages* ambazo wawekezaji wanapatiwa.

Lakini hata wanapokuwa na matatizo basi ziko taratibu za kufuatwa kwa wawekezaji hao hao. Utaratibu huu sina hakika kama utatusaidia sana lakini ndani ya sheria kuna utaratibu maalum, wenzetu hawa wangeliufuata na Serikali inakihitaji kiwanda hiki na viwanda vyengine, mimi naweza kusema hata kuliko wanavyokihitaji wao wenyewe. Kwa sababu sisi kama Serikali tuna dhima ya wananchi na ndio maana Serikali ikaamua kukitoa kiwanda kile na mashamba ambayo yalikuwa yakitumiwa na wananchi

Mhe. Naibu Spika, lakini pia serikali inatoa *incentive* maalum kwa kiwanda hiki, na inatoa kwa mujibu wa Sheria ya uwekezaji. Wao wenyewe wanajua tunatoa *exemption* kwa vifaa wanavyoviingiza ambavyo vina-*qualify* kupewa *exemption*, hii yote ni kwa ajili tunasamehe kodi kubwa sana, kwa ajili ya kuwawezesha wenzetu hawa waweze kufanya kazi zao vizuri lakini kwa matarajio kwamba wananchi wetu watapata ajira, lakini vile vile kukua kwao kibiashara basi na mapato ya serikali nayo yataongezeka. Kwa hiyo, inafanyiwa kazi vizuri sana, lakini na yale ambayo sisi tumewapa kama huo ni ushauri kutoka serikalini tunawaomba sana wenzetu hawa wauchukue ushauri huo.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo wenzangu wameshalizungumza suala la takwimu hizi zilizoletwa hapa Mhe. Naibu Spika, hizi takwimu zina utata, tena utata mkubwa sana, siamini kabisa kabisa kwamba hali iko hivi. Kwanza

nilikuwa najiuliza ni nani hasa aliyefanya tathmini hii, kwa sababu viko vyombo vinavyokubalika vinavyofanya tathmini majanga kama haya yanapotokea. Sasa kama wamejitathmini wenyewe wakaona ekari hizi na thamani yake ni hii, hilo ni suala jengine lakini wapo watu maalum chombo cha serikali pia kipo ambacho kina taaluma ya kufanya tathmini ya mazao wangekitumia kufanya *verification* ili tunapoziweka takwimu hizi basi kweli takwimu ziwe zinaleta maana. Kwa sababu hapa Mhe. Rashid, alizungumza unazungumzia ekari 9.11 zina thamani ya shilingi milioni 6,455,000.

Lakini kuna ekari 152.2 zina thamani ya shilingi milioni 5,370,000, lakini huku kuna ekari 150 zina thamani ya bilioni 1,830,000,000. Hizi takwimu zenyewe zinatupa utatanishi, zina haja ya kufanyiwa *verification* Mhe. Naibu Spika, zikizungumzwa hapa kwa kweli si jambo zuri sana kabla hatujazi-*verify* takwimu za namna hii kwa sababu zinatisha. Ukizungumzia suala la kwamba kuna ekari 902 zimepata hujuma hiyo. Sawa kwa nyakati tofauti na kwa maeneo tofauti. Katika ekari ngapi ambao wenzetu hawa wanazo, lakini unazungumzia suala la bilioni 9.8, ni tatizo kidogo, watu watakaotusikia wataona kwamba kuna hujuma nzito sana pengine imepotoshwa kutokana na takwimu hizi.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwenye *role* ya ulinzi, wenzangu wameshazungumza vizuri sana kwamba, *role* ya ulinzi serikali ina *role* hiyo kwa ulinzi ule wa jumla, lakini *role* ya mtu na *asset* yake bado inabaki kwa mmiliki. Tukianza kuzungumzia kwamba ulinzi sasa utolewe kwenye viwanda vyote vilivyopo hapa au *investments* zote zilizopo hapa ina maana na wenye mahoteli nao wakalindwe, wakatunziwe mali zao, Mhe. Bakhera, pale ana kiwanda cha maziwa nacho twende tukalinde huko kwenye Kiwanda cha Maziwa, kuna watu wana mashamba makubwa sasa hivi ya mpunga yakalindwe, haiwezekani, maduka yakalindwe haiwezekani. Hii bado inabaki ni jukumu lao kama wawekezaji, ule ulinzi wa jumla serikali inaendelea kuutoa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, vile vile, kuna mashirikiano makubwa sana yanayofanywa na wawekezaji, jeshi la polisi linafanya kazi hiyo, lakini pia na wananchi kwa ujumla wao ulinzi upo na upo wa uhakika na ndio maana nchi yetu mpaka sasa iko katika hali ya amani, utulivu na usalama na tunamuomba Mwenyezi Mungu iendelee hali hiyo. Ulinzi wa *assets* zetu wa mali zetu bado ni jukumu letu na tusiepuke hilo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakumbuka wenzetu hawa wana vitu karibu 16 waliviomba vifanyiwe kazi katika serikali, na vyoto hivyo tumewaelekeza

namna yakufanya. Wamekuwa wakija ofisini kwangu, wanakwenda ofisini kwa Waziri wa Biashara, wanakwenda kwa Mhe. Waziri wa Kilimo na sote sisi tushatembelea na tushazungumza nao. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mohammed, hii hoja sawa tumeiona, maelezo yake tumeyaona lakini bado kulikuwa na taarifa nyengine zilikuwa ziingizwe humu ili ikamilike na wajumbe waweze sasa kufanya maamuzi kutokana na mapendekezo hayo.

Mhe. Naibu Spika, ukiyatizama mapendekezo yaliyotolewa humu wala hayana matatizo kwa sisi kuyakubali, lakini bado unayakuta kwamba lile jukumu lote limewekwa kwa serikali, hilo la ulinzi wao wenyewe hawajaonesha watafanya kitu gani kwenye mapendekezo haya, yote Kamati za Ulinzi na Usalama, serikali, jeshi la polisi, lakini kama wao wana *role* gani kwenye hili. Kwa hiyo, mapendekezo yanaweza kuwa mazuri lakini bado yana mapungufu. Mhe. Naibu Spika, naomba kuchangia. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini pia nimshukuru mtoa hoja kwa maelezo yake, lakini niwashukuru zaidi Waheshimiwa Mawaziri kwa kulieleza jambo hili kwa upana wake na Waheshimiwa Wajumbe, kutoa michango yao.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwa kusema kwamba dhamira ya serikali ni kubwa sana katika kuimarisha viwanda na kuimarisha uwekezaji nchini. Mhe. Naibu Spika na Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Rais mwenyewe amekwenda kutembelea kiwanda kile, akaona, akayasikia, akayafahamu yaliyopo. Pia, akamuagiza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuchukua kila hatua kusaidia kila tatizo linalojitokeza pale ili wawekezaji wetu hawa wapate fursa nzuri ya kuendeleza uwekezaji. Maana serikali imeamua na imekubali kuimarisha uwekezaji nchini na kwa kiwanda kile ni uwekezaji maalum unaopewa kipaumbele maalum.

Kama walivyotangulia kusema Waheshimiwa Mawaziri hapa kwamba mawaziri mbali mbali wamekwenda pale. Mhe. Rais amekwenda pale, Mhe. Makamu wa Pili, amekwenda pale mara nyingi, mawaziri mbali mbali wamekwenda pale, hata mimi mwenyewe nimekwenda pale. Serikali iliunda kamati maalum ya mawaziri kwenda kuona matukio yale, kutafuta chanzo na matatizo yenyewe. Kwa bahati nzuri mawaziri wote wameeleza kwamba tayari ile kazi iliyoundwa na kamati imetayarisha ripoti, imeona kuna hatua za muda mfupi, hatua za kati na za muda mrefu zichukuliwe katika uendelezaji wake. Yako mambo ambayo wenzetu hawa walishauriwa kwa msingi wa kuimarisha kiwanda na mashamba.

Mhe. Naibu Spika, sasa dhamira yetu ni njema na mara nyingi Waheshimiwa Wajumbe hapa walisema serikali sio sikivu. Waheshimiwa Wajumbe, sisi kila lenye maslahi kwa wananchi hatuwezi kulikataa, nyie mna wajibu wa kutushauri na lile ambalo tunaona hili liko na maslahi na maendeleo ya nchi yetu hatulikatai, kwa sababu tunafanya kazi moja ya kuwatumia wananchi wetu. Lakini tukubali kwamba na serikali ina *missionary* kubwa zaidi ya kuona mambo mbali mbali. Kwa hiyo, pale ambapo tunaona aah, hili ndio mliotushauri lina kasoro hii tulifanye kwa utaratibu huu, si kwamba tunakataa, lakini watutafutie utaratibu ulio mzuri zaidi wa kufanya ili mambo yaende vizuri.

Sasa suala la moto pale limejitokeza likiwa na sura mbali mbali, kwa hiyo, kuna waliosema habari ya hujuma, kuna waliosema na utaratibu wenyewe wa kuyasimamia mashamba yanaweza kuwa tatizo. Moja ni hili la barabara zile za mashamba na majani tumewashauri sana wenzetu kwamba barabara zile zisafishwe ili isaidie moto unapotoka upande mmoja usirukie upande wa pili.

Mhe. Naibu Spika, lakini na mapendekezo mengi ambayo wenzangu wametangulia wameyaeleza nayo yalitakiwa yasikilizwe kuepuka kurudia kasoro ambayo kila mara zinajitokeza. Sisi serikali tumewaagiza wenzetu wa Kikosi cha *Fire* kama mnavyojua wana kituo chao pale jirani, lakini wameagizwa waimarishe shughuli za uzimaji moto kwa msingi wa kusaidia wenzetu pale. Na wenzetu pia wakashauriwa jamani shirikianeni na vikosi vyetu vya SMZ ili kama kuna jambo lolote la kiulinzi mshirikiane na nyinyi nyote ni mashahidi Waheshimiwa Wajumbe hapa.

Serikali imeanzisha taasisi maalum ya ulinzi, ukitaka ulinzi basi upo pale unakwenda, unajieleza unavyotaka na kwa kiwanda hiki sisi ni kipaumbele namba moja. Kwa hiyo, ni wenzetu hawa lazima waamue maana upo ulinzi wa jumla tunaufanya, lakini kwa *specific areas* hatuwezi kwa kila mwekezaji ukasema una-*deploy* ulinzi uupeleke pale. Sivyo kiutaratibu ulivyo ila serikali ina taratibu zake, lakini yale ambayo sisi tunaweza kuyafanya tunayafanya na ndio maana tunafanya kila jitihada kutoa *incentive* mbali mbali kwenda pale, kushauriana msingi wake tuwe na kiwanda bora kinachozalisha sukari kwa wingi. Na mengine mengi ambayo wao wameyataka kwa serikali yanafikiriwa kwa msingi wa kuimarisha kiwanda chetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nikubaliane sana na hoja aliyomalizia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwamba maazimio haya ukiyatazama ni kazi za kila siku za serikali. Kwa hivyo, hayana shida yoyote maana yake ndio mambo tunayoyafanya kila siku, lakini ilikuwa vizuri na upande wa pili wa shilingi nao

uangaliwe ili na wenzetu kama tuna tatizo nao walione ili ule uwekezaji uzidi kupata nguvu. Sisi tumekitoa kiwanda, tumeyatoa mashamba mjue tumepata kazi kweli kweli namna ya kushauriana na wananchi wetu pale kukubali kuyaachia mashamba yale yaendelee kulima kilimo cha miwa. Tumefanya kazi kubwa, kwa hiyo, wao walidhani wangeyatumia zaidi kwa kilimo cha mpunga, lakini baada ya mashauriano ya muda mrefu wenzetu wakakubali.

Sasa tatizo jengine lilojitokeza ambalo hatuwezi kuwalaumu wenzetu ni muda ule wa ukarabati kiwanda chenyewe ulichukua muda mrefu kufikia hatua ya uzalishaji, wananchi wetu wale wakaanza kuvunjika moyo kwa sababu baadhi yao nao waliacha kulima mpunga kama kawaida yao wakaanza kulima miwa. Sasa kutokununuliwa kwa miwa yao nao wakaona kiwanda hiki hakina maslahi makubwa kwetu kutokana na ile shughuli za ukarabati na ufungaji wa mashine, lakini ndio matatizo ya kiufundi yanatokea. Kwa hiyo, hili tunalielewa na wananchi wetu tumewaeleza na kwa kiasi fulani wananchi wanakubaliana na hali halisi ilivyo. Sasa hili ni jambo letu pamoja hakuna hata mmoja wa kumlaumu mwenzake, nia yetu ni kuendelea kuimarisha kiwanda kile, kuendelea kuimarisha mashamba yale ili yawe faida kwetu pamoja.

Sasa cha msingi hapa maelezo mengi yametolewa na serikali kupitia mawaziri mbali mbali, nadhani wenzetu hawa nao wayasikilize na bado warudi serikalini, Wizara ya Kilimo milango yake iko wazi, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko milango yake iko wazi, Waziri wa Fedha na Mipango milango yake iko wazi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais milango yake iko wazi, tushauriane tatizo lolote ambalo ni kikwazo liondoke, kwa kiasi fulani tumeona unafuu fulani. Yako yenye hujuma zaidi kwa kiwanda kile tunayafanyia kazi zaidi, yako yaliyosemwa hapa, namuheshimu sana Mhe. Rashid, amesema wako pia wasiopenda mafanikio ya kiwanda kile, kwa sababu kinatoa ushindani mkubwa katika sekta ya uzalishaji wa sukari. Sisi tunataka sukari itutosheleze ndani na tuuze nje.

Kwa hivyo, kwa vyovyote wapo ambao kwa njia moja au nyengine watachukia hoja hiyo, kwa sababu wapo wanaopata maslahi makubwa kwa kuuza sukari. Sasa kiwanda hiki kikizalisha vizuri kikatoa sukari itakayokidhi haja kwa uzalishaji wa ndani wapo watakaoathirika katika uletaji wa sukari kutoka nje. Lakini sisi tunataka kiwanda kiendelee kwa msingi wa wananchi wetu kupata kazi, uzalishaji wa ndani unaongezeka kwa msingi huo tunaimarisha uchumi wetu sasa kila hatua ya serikali inafanya ili kulinda uwekezaji huu.

Kwa hiyo, napenda tukubaliane na wananchi wetu watuelewe na kila mmoja atuelewe kwamba dhamira njema ya awali ya kukitoa kiwanda hiki kwa

wawekezaji iko pale pale na ndio nia na madhumuni ya serikali. Kwa maazimio haya ambayo yametolewa hapa ni shughuli za kawaida za serikali tumezifanya na tunaendelea kuzifanya. Kwa hivyo, kwetu hatuoni kama kuna hoja ya kupinga haya, haya ni mambo siku zote serikali inafanya; kama kuimarisha ulinzi serikali inafanya, kushirikiana na wananchi serikali inafanya, kutaka kuimarisha uwekezaji serikali inafanya, kutoa elimu kwa wananchi kuelewa umuhimu wa uwekezaji serikali inafanya. Kwa hiyo, yote haya ambayo yamo katika maazimio ni kazi za kila siku za serikali.

Kwa hiyo, Mheshimiwa, ameona atukumbushie lakini shughuli hizi zinafanywa na mimi namtakia kheri na hoja yake hii. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, kwanza niendelee sana kukushukuru kwa muda huo, lakini vile vile niwashukuru wajumbe wote waliochangia na wale wasiochangia na leo wajibu wao wote ilikuwa ni kuchangia, lakini nafasi ilikuwa ndogo. Lakini niwatambue sasa wale wajumbe ambao walichangie. Wajumbe wote waliochangia hoja yangu walikuwa ni wajumbe 20.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, hii ina maana hata miswada ile anayoletwa *AG* wachangiaji wangu walikuwa wengi kwenye hoja yangu. Waliochangia moja kwa moja walikuwa ni wachangiaji 14, lakini wachangiaji 6 walichangia kwa maandishi, niwashukuru wote sana. Naomba niwataje Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako.

Waliochangia moja kwa moja ni:

1. Ali Suleiman Ali
2. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
3. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
4. Mhe. Abdalla Ali Kombo
5. Mhe. Suleiman Makame Ali
6. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
7. Mhe. Rashid Makame Shamsi
8. Mhe. Mussa Ali Mussa
9. Mhe. Simai Mohammed Said
10. Mhe. Hamza Hassan Juma
11. Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi
12. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko

13. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, mwisho lakini sio kwa umuhimu wake
14. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Wachangiaji ambao wamechangia kwa maandishi ni sita:

1. Mhe. Khadija Omar Kibano
2. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
3. Mhe. Maryam Thani Juma
4. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
5.Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
6. Mhe. Waziri wa Habati, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, mambo mengi wamezungumza, lakini sitaweza kujumuisha kwa kila Mjumbe mmoja mmoja aliyosema, mbali ya kuwa tuna muda mdogo, lakini mambo ni mengi na nilitangulia kusema hoja yangu hii Wajumbe wengi sana wameichangia. Ninawashukuru sana wote kwa sababu kila mtu anajua umuhimu wa swala, lakini kabla ya kuswali tunatakiwa tusome adhana na adhana hii tumeisoma. Nimeona vizuri sana kuwa serikali ime-*respond* vizuri juu ya hoja hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa upande wa mawaziri ambao wamechangia hoja hii sana. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango; Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais; Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi; wote walichangia kwa upana wake. Lakini kitu cha ajabu sana nataka kusema kama tusingeleta hoja hii wananchi wasingepata ufafanuzi ambao serikali imeutoa na haya ndio majukumu yetu kuweza kuleta hoja, serikali tukaiambia wakaleta ufafanuzi hadharani. Leo siwezi mimi kama Mwakilishi kukaa chemba na serikali kutaka hiki na hiki, wananchi wetu watajua nini? Lazima serikali ilete ufafanuzi *publicaly* tuweze kujua. Nadhani *AG* atanisaidia sana kifungu cha 88 cha Katiba yetu kinazungumza kazi zetu sisi Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, iko dhana kubwa sana ya kuwa baadhi ya mawaziri inasemekana wanawatisha hata Wajumbe wetu wa *backbencher* wakati tukileta hoja kama hizi kuziunga mkono, sio haki. Kuna njia tatu za Wajumbe waliokuja humu ndani, kuna waliokuja kutoka kwenye majimbo nao wana sifa ya kuwa viongozi, lakini kuna walioteuliwa na Mhe. Rais nao ndio wana sifa ya kuwa viongozi na wale waliotoka kwenye viti maalum nao wana sifa ya kuwa viongozi. Kwa umoja wetu sasa tunatakiwa tujenge nchi yetu kuwa *backbencher* na *front* ni vitu viwili tofauti, wengine wanaongoza serikali,

wengine wako nyuma wanaisimamia serikali, lakini lengo letu ni kuidumisha na kuisimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka nitumie fursa hii na wanisikilize sana wananchi ninaozungumza nao na hasa Wajumbe wa Kamati Kuu wa Halmashauri Kuu ya CCM, Kamati Maalum ya Zanzibar, wafike pahali nao waisimamie serikali, watusaidie kuisimamia serikali, wakifika waiulize kwa ujumla wake nini mmefanya na hilo ndio limo kwenye Ilani yetu na chama chetu ndicho kinachoongoza Ilani ya Chama hiki.

Mhe. Naibu Spika, nilisema nakipongeza chama changu kwa kuwa kimenipa nafasi ya kusimamia Ilani ya Chama na kupeperusha bendera yake. Kumeelezwa sana tu mambo ya takwimu hayakukaa sawa, lakini nimeona kwa upana wake.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, yeye amezungumza, mimi niliona kila katika takwimu hizi ambazo wenyewe kiwanda ndio nilizozichukua kule. Kwa kila hekta haizidi shilingi milioni kumi. Sasa huyu mwenzangu Mhe. Waziri wa Kilimo, shilingi bilioni moja kwa kila hekta sijui yeye kaipata wapi na mimi naangalia kuwa isingekuwa shilingi bilioni tisa, milioni mia saba; labda yeye ingekuwa ni shilingi bilioni tisini na saba, sijui hapa pana mapungufu ya hesabu! Tukae vizuri labda tuweze kuyatizama kwa vizuri ili tuone na tuifanyie utafiti.

Mimi nimeileta hapa kuiambia serikali tufanye utafiti wa kutosha katika mambo yote ya uwekezaji ili tuone tunakaa sawa. Nimezungumza na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Mwakilishi wangu wa kijijini kwangu Donge, nimeeleza kwa kuwa alisema hiyo *title* haikukaa sana. Lakini nataka nimwambie afuate katika ukurasa wangu wa pili, kifungu cha mwisho kabisa ndipo nilipoeleza makusudio hasa ya hoja yangu. Kwa kuwa vitendo hivyo vimekuwa vikijitokeza mara kwa mara katika Kiwanda cha Sukari cha Mahonda Zanzibar katika Mkoa wa Kaskazini, Wilaya ya Kaskazini 'B'.

Mimi nadhani anajua Kijaninge na mimi nazungumza lugha moja, ni vyema kuifuatilia vizuri sana tukaweza kuona, lakini Waheshimiwa wote waliochangia wamechangia kwa upana wake.Nimshukuru sana Mhe. Mussa Ali Mussa, leo amenguruma kwa upana wake na serikali imemsikia. Mimi ningeomba jambo moja kubwa, ninayo mengi lakini sitaweza kuyajumuisha yote kwa pamoja kwa sababu naona muda umekwenda sana. Naomba tu niwape na yaingie kwenye *Hansard* kama nilivyoyajumuisha.

Mhe. Naibu Spika, nataka kusema mipango mizuri yote ya serikali katika sekta ya viwanda na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, tumpe hongera sana kwa kazi yake kubwa anayoifanya. Anajaribu kukimbia huku na huku lakini anataka kuhakikisha kwamba viwanda vimekuja nchini. Sasa tuwalinde hawa wawekezaji tuliokuwanao, lakini hao wengine hatujui Zanzibar watakuja lini, niiombe sana serikali yangu na niishauri kudumisha hivi viwanda vyetu vya ndani ambavyo vipo hapa.

Juzi nilipokuwa nikichangia hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, nilisema, sote tumekuwa kama tuna njaa ya Ramadhani, kila kitu tumekuwa tukikitaka kwa pamoja, haiwi vitu vyote kwa pamoja. Niombe sana serikali yangu tukufu na sikivu, *Senate* ayachukue haya yote akayafanyie kazi wala Mhe. Naibu Spika, hapa leo hatutatoa hoja kwa upana wake. Mimi nataka waichukue wakaifanyie kazi halafu watwambie basi tumefanya moja, mbili, tatu, nne; wala sisi hatuwezi kusema tukae na pande zote mbili, tutakaaje sisi na upande wa serikali, ila tukae na hawa wenye matatizo ili tuweze kujua wana matatizo gani, tulete hapa, lakini serikali itujibu.

Mhe. Naibu Spika, leo imekuwa vyema sana, nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, ametujibu kwa upana wake vizuri tu, lakini nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, ametujibu vizuri, lakini je, leo tusingekaa pamoja tukajua wawekezaji wana tabu gani, tusingelileta hapa nani angejua? Hatuwezi kupiga adhana ndani ya vibuyu wakati ule sasa umekwisha, tutasema waziwazi ili watu waone na nyinyi serikali mtujibu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nadhani Mheshimiwa, aliyetoa hoja ameweza kufanya majumuisho vizuri sana, sote tunajenga nyumba moja, kila mmoja kakamata fito kwa upande wake na ninaamini kabisa kwamba nyumba hii tutaijenga kwa salama na amani na Mwenyezi Mungu atatupa uwezo huo wa kuijenga nyumba hii.

Waheshimiwa Wajumbe, mimi niwashukuru sana wale wote ambao wamechangia na niwapongeze sana serikali kwa majibu yao mazuri, siwahoji kwa sababu najua serikali inajua majukumu yake na haya mengine ambayo yamezungumzwa ni kwamba, serikali tayari wanayafanyia kazi. Kwa hiyo, Waheshimiwa, haina haja ya kuhoji, mjadala ulikuwa mzuri na tumefikia pahala pazuri sana sote kwa pamoja. Mimi nafikiri kwa hili tujipongeze Waheshimiwa, tumekuja na hoja makini, hoja imezungumzwa kabisa kwa

heshima kubwa na kabisa tumefikia muwafaka mzuri, Mwenyezi Mungu atujaalie tuendelee hivi hivi nawashukuru sana. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea kama nilivyosema mwanzo kwamba baada ya hoja hii tutakuwa na uchaguzi. Kwa hivyo, sasa niwaachie makatibu watoe utaratibu wa uchaguzi.

Ndugu Mussa Kombo Bakari (Katibu Mezani): Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kama ambavyo mlitangaziwa awali kutakuwa na uchaguzi wa Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Nadhani Mhe. Naibu Spika, alitoa maelekezo kwamba mbali ya uchaguzi huo lakini pia ufanyike sambamba na uchaguzi wa Umoja wa Wajumbe Wanawake katika Mabunge ya Jumuiya ya Madola Tawi la Zanzibar. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, mtapewa kura zinazohusu chaguzi zote mbili, uchaguzi wa Umoja wa Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola Tawi la Zanzibar, lakini pia na uchaguzi wa Umoja wa Wanawake wa Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa uchaguzi utakuwa kama ifuatavyo: Baada ya kuthibitisha idadi ya Wajumbe waliomo ndani ya ukumbi wa Baraza, wagombea tutaanza na uchaguzi wa *CPA* na tutaanza kwa nafasi ya mwenyekiti.

Wagombea watajieleza kwa muda wa dakika tatu na wanaweza kuulizwa maswali yasiozidi mawili kwa sababu ya muda na watayajibu maswali hayo na wagombea wakati wa kujieleza wako huru kutumia lugha ama ya Kiswahili ama ya Kiingereza kadri watakavyohitaji. Baada ya hapo tutagawa kura na ili kuokoa muda tutawasikiliza Wajumbe wote wanaogombea halafu tutagawa kura zote za *CPA* na baada ya hapo kura zitakusanywa na zitakwenda kuhesabiwa.

Waheshimiwa Wajumbe, baadaye mtaingia katika uchaguzi wa *CWP* (Umoja wa Wajumbe Wanawake wa Jumuiya ya Madola) na baada ya kupiga kura, kura zitahesabiwa. Kwa maelekezo ya Mhe. Naibu Spika, kadri mtakavyokubaliana ama tunaweza tukaakhirisha mpaka baadae na matokeo yakatolewa leo leo au mkiona inafaa kadri ya maelezo ya Mhe. Naibu Spika, maelezo yanaweza yakatolewa kesho. Hayo yatategemea maelekezo ya kiti, lakini kwa ufupi huo utakuwa ndio utaratibu wa uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, tutakuomba sasa utoe maelekezo ya kuhesabiwa kwa Wajumbe ili tuweze kujua tuna Wajumbe wangapi ndani ya ukumbi.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza kama ilivyoelezwa na Katibu Mezani kutakuwa na uchaguzi wa *CPA* na baada ya hapo utafuata uchaguzi wa *CWP*, lakini kuna hoja ambayo imezungumzwa hapa suala la kwamba tuakhirishe baada ya uchaguzi ili tukaendelee na shughuli nyengine na matokeo yatafuata kesho asubuhi. Sasa hilo naomba niliulize kwa pamoja kama tunakubaliana hivyo kwa sababu ya muda hautoshi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa, nawauliza wanaokubaliana na hili wanyooshe mikono, kwamba tunapiga kura na tunaondoka, matokeo yatakuwa kesho, wanaokubaliana na hilo wanyooshe mikono.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hapa Wajumbe hawakukubaliana na hoja hii na hivyo hawakunyoosha mikono)

Mhe. Naibu Spika: Ina maana tutasubiri matokeo hapa?

Wajumbe: Ndiyo!

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sawa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe wote ni 56, hivyo, kura zitakuwa 56, sawa?

Wajumbe: Sawa.

Mhe. Naibu Spika: Kwanza tunaanza na uchaguzi wa *CPA*, naomba sasa niwataje wagombea. Mgombea wa kwanza ni Mhe. Simai Mohammed Said, karibu ambaye anagombea nafasi ya Uenyekiti. Mhe. Simai, tafadhali.

Waheshimiwa Wajumbe, mmepewa dakika tatu kwa ajili ya kumuuliza maswali, ajitambulishe lakini kama kuna swali lolote tutamuomba Mheshimiwa, ajibu. Mhe. Simai, karibu.

Mhe. Simai Mohammed Said, naomba ujitambulishe jina lako ili Wajumbe waweze kukufahamu, lakini pamoja na mengine ambayo utahitaji kujielezea wewe mwenyewe binafsi, maelezo ya binafsi, karibu.

Mhe.Simai Mohammed, kwa lugha yoyote ikiwa uko *comfortable* kwa Kiingereza zungumza Kiingereza, ikiwa kwa Kiswahili zungumza Kiswahili.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Naibu Spika, ahsante nakushukuru sana kwa nafasi hii. Waheshimiwa Mawaziri, Mhe. Mwanasheria Mkuu, Waheshimiwa Manaibu Waziri, Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Kamati za Baraza; Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati zetu; Waheshimiwa Ma-*back benchers* wenzangu, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, *Assalamu Alaikum.*

Nimesimama mbele yenu kwa jina naitwa Simai Mohammed Said (Mpakabasi), Mwakilishi wa Jimbo la Wananchi Tunguu. Nimesimama hapa leo kwa unyenyekevu mkubwa sana, ni mara yangu ya kwanza katika maisha yangu kugombea nafasi ambayo pia hakuna mtu mwengine ambaye anagombea. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lakini nafasi hii ninayogombania ndio maana nikatanguliza maneno ya unyenyekevu ni kwamba, hao wanaotaka kunipigia kura ni watu ambao mko makini sana. Sasa kwa lugha nyepesi kabisa na kwa umoja wetu tuliokaanao pamoja humu ndani, mmenizowea mimi ni mcheshi, nafasi nitakayosimamia hapa ni kwenda kuisaidia Ofisi ya Spika wetu na Naibu Spika katika kuanzisha tawi letu la Zanzibar la *Commonwealth.* Mimi niko tayari kushirikiana na wenzangu wote hapa Zanzibar na kamati yetu tendaji pamoja na Ofisi ya Spika na Katibu wake na Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa umoja wetu wote kuhakikisha kwamba hili tawi letu la Zanzibar linasimama linakuwa imara. Mimi katika maisha yangu jambo lolote nililolianzisha basi hadi leo limeweza kusimama.

Uzoefu huo ninao kabla sijaingia Barazani nawaahidi nyote nitatekeleza kwa ushirikino, hamu ninayo, uwezo ninao na namshukuru Mhe. Spika, mwezi wa 8 tuliambatana pamoja kwenda kushiriki katika mkutamo wa haya Mabunge yetu ya *Commonwealth Parliamentary Association* kwa ajili ya Kanda ya Afrika na kule pia nilipata fursa na nikaongea kwa dakika 19 kwa lugha hiyo ya Kiengereza na nika-*present* mada kuhusiana na masuala ya umeme jinsi gani Mabunge yetu yanaweza kuishauri na kuisaidia serikali na katika kule pia baada ya kumaliza karibu nchi 8 zilichangia ile hoja na ilibidi nirudi kwao kujibu ikiwemo *South Africa,* Nigeria, Ethiopia, Namibia. Kwa kweli inabidi nijisifu au nijipongeze lakini hiyo nyote mnastahiki siku ile Jamhuri ya Muungano Tanzania nilipeperusha bendera na watu walishukuru sana walifurahi na kwa kweli sikuwaangusha wananchi, nyinyi Wajumbe wezangu Barazani na Watanzania wenzangu.

Mimi ninachoomba leo nyote kwa unyenyekevu mkubwa...

Mhe. Naibu Spika: Omba kura Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Ndugu zangu Waheshimiwa Mawaziri, viongozi wote mliokuwemo humu ndani leo naombeni sana ile kalamu itakapoteleza kwenye ile karatasi basi mnione pale kwa huruma, mnipe ile kura ya ndio, nitafurahi na kufanyakazi. Baada ya machache nashukuru sana na kama ule yeyote nimemkosea jambo basi namtaka radhi bwana....

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia. Waheshimiwa Maswali.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi nina swali langu moja kidogo. Labda ningependa kujua mgombea wetu anaongea lugha ngapi. Ahsante.

Mhe. Simai Mohammed Said: *Thank you very much honourable deputy speaker,* kwa ruhusa yako nitapenda sana kuongea lugha ya Kiengereza kidogo.

"To respond to the Deputy Minister, I am fluent with three languages which is English, Kiswahili and Hindi but I cannot read or write in Hindi language but I can speak and hear and communicate very well. My English is extremely are well polished, I can read and write and you have no reason to worry when come to communications. Thank you very much"

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa swali jengine. Mhe. Said Soud Said.

Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara (Mhe. Said Soud Said): Mhe. Naibu Spika, mimi nina maswali mawili (a) na (b).

(a) Mheshimiwa mgombea, sisi kama mawaziri hatuna ruhusa ya kuchaguliwa, kwa nini unataka kura zetu na sie hatuchaguliwi. Maana ukiwa huchaguliwi, huchaguwi, kwa mujibu wa hii sheria, ama huchaguliwi huchaguwi la kwanza hilo.

(b) Mhe. Naibu Spika...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Waziri la kwanza sio kazi yake kujibu kwa sababu hizo ndio Kanuni za *Commonwealth* kwamba. waziri hatoshiriki katika C*PA*, lakini atapiga kura. Kwa hiyo, Mheshimiwa, hilo swali sio lake, hilo swali ni kutokana na Kanuni za C*PA*.

Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara (Mhe. Said Soud Said): Mhe. Naibu Spika, nataka kujua elimu yake huyo ana elimu ya darasa la ngapi. Maana inawezekana kwamba kizungu chake kaokota okota tu na wako watu namna hii. Mhe. Naibu Spika, watu kama hawa wapo wanao uwezo huo...

Mhe. Naibu Spika: Sawa Mheshimiwa, tumekufahamu umemaliza kaa, umekwisha.

Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara (Mhe. Said Soud Said): Mhe. Naibu Spika, namuhoji mie kwa vile uhuru wa kuhoji uwepo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Said Soud Said, basi imetosha ushauliza. Mheshimiwa, jibu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri, rafiki yangu kwa swala zuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimepata *Trainings* tafauti, lakini kwa elimu ambayo niliyokuwa nayo nina *Advanced Diploma* ya kwenye masuala ya usafiri na usafirishaji na nimechukuwa Uingereza. Lakini pia nimechukuwa *Advanced International Training* katika mambo ya *Strategic Business Plan* mwaka 2009 Sweden ambayo ilikuwa ni *intensive course* kama *cash course* ya *NBA* ambayo ita- *follow up* semina *South Africa*.

Kwa hiyo, naamini Kiengereza changu si dhani kama nina wasi wasi nacho, maana yake malezi niliyokulia nayo mimi hata nyumbani nimekulia katika malezi ya lugha mbili. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Swali la mwisho Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza mgombea swali moja.

Kwa kuwa Mheshimiwa mgombea nafasi ambayo anayoiomba ni kubwa Mwenyekiti wa *Sub Branch* ya C*PA* Zanzibar. Baraza lililopita tulijaribu kutaka ku-*launch* hii *Sub Branch,* lakini tukawa hatujafanikiwa. Je, mgombea anatuhakikishiaje kwamba hapa tulipokaa hatupotezi muda wetu na kwamba *Branch* hii itafunguliwa rasmi na itakuwa *active*.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi ningependa nimjibu Mhe. Wanu Hafidh Ameir, kwenye suala hili.

Kwanza niseme kwamba kuanzisha katika hii *Branch* kwa upande wa tawi sio juu yetu sisi peke yetu, ni utaratibu ambao itabidi tushirikiane na Afisi ya Spika pamoja na *Branch* ya Jamhuri ya Muungano kutoka Afisi ya Bunge. Kwa hiyo, sisi tutafanya kwa kamati kwa kushirikiana na Afisi ya Spika na kuhakikisha kwamba haya yote ambayo yaliazimiwa katika kikao kilichopita au Baraza lililopita tuyaendeleze pale walipoyaacha. Lakini tutafanya kazi kwa nguvu zaidi na Mhe. Naibu Spika, nikuahidi kwamba baada ya matokeo yatakapotangazwa nitakuomba sana uitishe kikao cha haraka ili tuanze kazi mara moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa kakae.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mgombea wa pili Makamu Mwenyekiti ni Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf. Mheshimiwa anza kujielezea.

Mhe. Nadir Abdul- Latif Yussuf: Tayari.

Mhe. Naibu Spika: Anza kujielezea, halafu wengine ambao watafuata wajitayarishe Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwenye Kamati tendaji Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Hamida Abdalla Issa, Mhe. Dkt Makame Ali Ussi, Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame na Mhe. Yussuf Hassan Iddi, wajitayarishe. Sasa Mheshimiwa, anza kujielezea.

Mhe. Nadir Abdul- Latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kunijaalia leo hii kufika hapa kuzungumza na Waheshimiwa wenzangu ndani ya Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, nimesimama hapa sio kwamba labda mimi mkamilifu au mimi najua kila kitu. Lakini nawashukuru sana wale wote viongozi wote waliotaka kuchukuwa nafasi yangu wakaniachilia kibinadamu kwamba na mimi nikajifunze.

Madhamuni ya kuomba nafasi hii pindipo Waheshimiwa Wajumbe *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu watanipa nafasi hii wakanichagua kwa ridhaa zao basi nawahakikishia kwamba nitafanyakazi kwa kushirikiana na Mhe. Rais wangu wa tawi, Mwenyekiti wangu mimi mwenyewe na wajumbe kwa ujumla

ili kuhakikisha kwamba tutaiwakilisha vizuri Zanzibar nchi yetu, serikali yetu Bunge langu, Baraza la Wawakilishi pamoja na kazi zote ambazo tutazijadili tutazipendekeza ili tukazizungumze kule ili Zanzibar ifanikiwe na *inshaallah* kwa Wajumbe wote ambao wanatarajia mambo mazuri basi tukaa nao pamoja kushirikiana nao watupe mawazo yao ili tukayari-*present* kule tutakapofika.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitakuwa na mengi kwa sababu hapa nimekuja kuomba na sijaja kujisifu, kila mmoja humu hodari kuliko mwenzake hakuna mbora aliekuwa mbora kuliko mwenzake. Ninachoomba kwamba Waheshimiwa wenzanu wanipe ridhaa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, nitajitahidi wa nafasi hii japo kuwa ndio mara ya kwanza lakini ndio naenda kuchukuwa uzoefu, lakini kwa elimu niliyojaaliwa nayo na Mwenyezi Mungu nitaweza kufanyakazi kwa kushirikiana na viongozi wangu. Mhe. Naibu Spika,...

Mhe. Naibu Spika: Malizia, Mheshimiwa, omba kura.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, naomba kura kwa Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, naomba kura vile vile kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wenzangu wa *back bencher* wanifikirie na wanijaalie kura ili niweze kwenda kufanya kazi na mimi kwenda kujifunza huko tutakapokwenda. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Haya, maswali?

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Aaah, lipo.

Mhe. Naibu Spika: Haya Mhe. Abdalla Ali Kombo.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika, nataka kumuuliza ndugu yangu rafiki yangu Mwakilishi wa Chaani tuna uzoefu wa kutosha hasa sisi wa *back bencher* huku, kuna watu waliomba Ubunge na tukawapa kuchwa kutwa mchana usiku tulikuwa nao. Sasa ukiacha Mhe. Jaku Hashim Ayoub, peke yake ndie anaesemesha watu huku nyuma na wewe ni maarufu huku nyuma, unatuhakikishiaje ukipata hii tutakuwa wenzako? (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Majibu Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, lile neno la mwisho sijalikamata vizuri, nitakapopata hii nafasi nitafanya nini, naomba kidogo, samahani.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Nasemaje, wewe mtu wa Kae, tulikuwa na wenzako wamegombania Ubunge kutoka *back bencher* huku, baada ya kwisha kupata hamna salamu yoyote. Ukiacha Mhe. Jaku Hashim Ayoub, na wewe ndie mwenye ufunguo wa *back bencher*. Je, ukishakupata unatuhakikishiaje na wewe utatusemesha au utatuacha.(*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, nitaomba kuomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi mwenzangu makini Mheshimiwa mwezangu wa *backbencher* mwenzangu, mzee wangu.

Mhe. Naibu Spika, nikuhakikishie kwamba kila Bunge lina utaratibu wake na sehemu tunayokwenda ni sehemu kama hii, lakini kiupande fulani imezidi *status* na ndio maana tukaamua kwa mara hii kwamba tutakapofanya kazi tutahakikisha kwamba Baraza letu hili tunaliwakilisha vizuri na tutakuwa *up to date* hapa na kule. Lakini ninachotaka kukuhakikishia kwamba tunapokwenda kuzungumza kule basi ni nchi 52 ambazo ziko pale na tunachotakiwa kuzungumza pale kile ambacho tulichokubaliana na kamati au na viongozi wenzangu.

Ninacho kukuhakikishia Mheshimiwa Mwakilishi kwamba, nitazungumza sehemu yoyote na tutawakilisheni vizuri na nchi yetu kwa ujumla. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Baada ya kuwa tumeshatoa karatasi za kura na tushapiga tutakuwa tunazikusanya, huyu bado, hiyo ya Mwenyekiti kwanza tutazikusanya halafu akimaliza huyu pia tutakusanya, sawa? Tutakwenda mtiririko huo. Kuna swali jengine. Jamani muda tuna semina mkae mkijua.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa ruhusa yako napenda kumuuliza Mheshimiwa mgombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti. Amekiri kwamba si mzoefu katika mambo haya, sasa nataka kumuuliza.

Je, yuko tayari kujifunza kwa wenzake na yuko tayari kufuata taratibu za Mabunge ya *Commonwealth* kwa sababu kuna taratibu zake kule. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, Ahsante sana kwa kuulizwa swali na Mhe. Jussa wa Mji Mkongwe, naomba nimjibu swali lake. Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima...

MUONGOZO

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, naona hajalitaja jina langu na yeye anaenda kwenye nafasi ambayo...

Mhe. Naibu Spika: Hebu taja jina lake.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, mimi nimetumia...

MUONGOZO

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa muongozo kwamba, unapouliza maswali na watu wakasema "maarufu" hiyo nafasi moja imeshapita. Maswali "Maarufu" anapouliza wa tatu, nafasi tatu zishakuwa tayari, muda tuna semina Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Sawa ni nyie wenyewe mnaofanya hivyo, sio mimi msinilaumu mimi. Nyinyi ndio mnaofanya "Maarufu" na nyinyi mnanyanyua mikono mnasema mnataka kuuliza. Kwa hiyo, sasa na mtu asijekulalamika.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mheshimiwa, tumia rungu lako.

Mhe. Naibu Spika: Naam na mimi nina haraka hivyo hivyo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Tayari?

Mhe. Naibu Spika: Endelea jibu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Nitaomba kujibu swali la Mhe. Mohamed Ahmada Salum Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe Mheshimiwa Makini. Namuhakikishia kwamba nitashirikiana na uongozi wa tawi la Zanzibar bega kwa bega kuhakikisha kwamba tunafahamiana na tunakijua nini tunaenda kukizungumza na nitashirikiana vile vile na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, wakiwemo mawaziri, ikiwemo serikali ikiwa Baraza la Wawakilishi ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inasifika na inajulikana nini tumeenda kukifanya. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa, nenda kakae.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, naomba kura kwa Wajumbe wote *In shaa Allah* Mwenyezi Mungu awajaalie wepesi wanichangue. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: *Amina* haya. Mgombea ni peke yako Mheshimiwa, kwa dalili utachaguliwa tu.

Waheshimiwa, sasa tunakuja kwa Kamati Tendaji tunanza na Mhe. Abdalla Maulid Diwani, naomba ujieleze kwa ufupi sana, anafuata Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: *Bismilah Rahmani Rahim:* Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Manaibu Waziri, Waheshimiwa wenzangu *back bencher*, mimi naitwa Abdalla Maulid Diwani ni Mwakilishi makini sana wa Jimbo la Jang'ombe nimesimama hapa leo kugombea nafasi ya Ujumbe wa Kamati tendaji wa Bunge la C*PA*.

Kwa vile tumeambiwa haraka sana, muda sio rafiki, mimi sitokuwa na mengi ya kueleza. Naahidi kwamba sitowaangusha nitashirikiana na wale wote ambao tutakaochanguliwa kutokana na miongozo yenu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, nahakikisha kwamba tutawawakilisheni vizuri. Naombeni kura zenu, mimi Abdalla Maulid Diwani katika nafasi hiyo ya Ujumbe. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Maswali?

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Maswali?

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Maswali?

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante, nenda kakae Mheshimiwa. Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: *Bismilah Rahmani Rahim.* Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii nikasimama mbele ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wajumbe wenzangu kuweza kuomba kura kwa nafasi hii ya Ujumbe wa *CPA.*

Mhe. Naibu Spika, sitaki kueleza mambo mengi kwa sababu Waheshimiwa wanaijua vizuri historia yangu, uzoefu wangu ndani ya Baraza la Wawakilishi, naamini wakiweza kunichagua nitaweza kuwasaidia sana Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kuwapa uzoefu wa Mabunge ili wanapokwenda kutuwakilisha katika Bunge la Jumuiya ya Madola, naamini wataweza kuchota mengi waweze kuyapeleka. Lakini vile vile na sisi kuchota mengi kuja kuyaleta kwenye Baraza letu la Wawakilishi. Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, naomba kura zenu nyote hasa Mhe. Said Soud Said. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Maswali?

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Maswali?

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Maswali?

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, omba kura ukakae.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamida Abdalla Issa. Waheshimiwa Mhe. Hamida Abdalla Issa, hayupo lakini nyote naamini mnamfahamu ametokewa na dharura, amesafiri kikazi, kwa hiyo, ameniomba mimi Mwenyekiti, nimuombee kura. Siwezi kujibu maswali yake, lakini amenambia nimuombee kura.

Kwa hiyo, Mhe. Hamida, mtakuwa nyie nyote mnamfahamu sawa. Tunaendelea Mhe. Dkt Makame Ali Ussi.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi leo nijieleze kama mmoja kati ya wagombea wa Ujumbe *CPA*.

Mimi kwa jina naitwa Dkt. Makame Ali Ussi, nilishawahi kushiriki kongamano la kimataifa lililofanyika kule Naivasha na kwa bahati nzuri nilichaguliwa mimi kuwa ni kiongozi wa kongamano lile. Kwa hivyo, nina uzoefu mzuri sana wa makongamano haya ya kimataifa.

Naomba kura zenu zote za 'ndiyo'. Ni Mwakilishi wa Jimbo la Mtopepo, kule kuna upepo baridi kule. Kwa hivyo, ninakuombeni sana Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wawakilishi, wote tuliopo hapa nakuombeni kura zenu zote za 'ndiyo' muzimimine kwa mimi ili niweze kuwa Mjumbe.

Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Maswali?

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana. Naomba kura zenu, kura zenu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, muda umekwisha sijakuona samahani, lakini ameshaondoka.
Tunaendelea Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ninathibitisha kwamba niliyesimama hapa ndiye hasa Dkt. Mwinyihaji Makame Mwakilishi wa Jimbo la Dimani.

Mhe. Naibu Spika, nimekuja kuomba kura na mimi kuwa Mjumbe katika nafasi tatu za Kamati Tendaji za Chama chetu cha Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; Mabunge ya *Commonwealth* kwa tawi la Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli sina mengi, isipokuwa ninachosema tu kwamba *branch* yetu ni mpya, changa inahitaji na sisi tujitangaze, tujiuze ili uzoefu waliopata wenzetu yanayosifika Mabunge mengine ya Lusaka, Afrika Kusini na wapi, basi uzoefu ule na sisi tuu-*tape*, tuulete hapa na tuliendeleze Baraza letu la Wawakilishi.

Kwa hivyo, ninakuhakikishieni kwamba tutajitahidi kujifunza na ku-*tape* waliofanya wenzetu tuyalete na hapa tuendeleze Baraza letu nalo liende na liwe la kisasa. Nawaombeni kura zenu.

Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Maswali, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, nimeshamtaja.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kumuuliza mgombea swali moja.

Kwa kuwa tunajua kwamba Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini amekuwa mzoefu katika nafasi ya Uwaziri kwa muda mrefu, lakini uzoefu huo huo umempatia nafasi mbali mbali za ku-*attend international meetings*. Je, ataisaidiaje Jumuiya hii ambayo tunaianzisha changa, uzoefu wako utasaidiaje Jumuiya hii katika kukuza.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Naibu Spika, ninamshukuru sana Mhe. Wanu Hafidh Ameir, kwa swali lake.

Kwa kweli ninachotaka kusema siku zote uzoefu unachanganya na uzoefu wa wenzio, usiseme uzoefu wangu mimi tu aah! na uzoefu wenu na niseme na elimu yenu. Kwa hivyo, yote nikichanganya pamoja na uliyosema na utaalamu wangu ninaamini tutapiga hatua katika kuliendeleza Tawi letu hili la Zanzibar. Ninashukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Maswali, maswali.

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Haya Mhe. Yussuf Hassan Iddi. Mheshimiwa jieleze.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kwa ajili ya kuomba kura.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu, niliosimama mbele yenu naitwa Yussuf Hassan Iddi, almaarufu masharubu. Nimesimama hapa kwa ajili ya kuomba nafasi ya Ujumbe wa Kamati ya Bunge la *CPA*.

Kwa heshima kubwa sana nawaomba kura zenu za 'ndiyo' kwa jina la Yussuf Hassan Iddi. Hivi sasa nimekuwa mtu wa mwisho katika kuomba kura hii. Lakini ninawaomba wakati wa matokeo niwe mtu wa mwanzo.

Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Maswali, maswali.

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, omba kura ukakae.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante sana naomba kura zenu.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa sasa tutamwita Mweka Hazina Mhe. Hassan Khamis Hafidh. Mheshimiwa jielezee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante. Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe, jina langu Hassan Khamis Hafidh ni Mwakilishi wa Jimbo la Welezo au maarufu *DIASPORA*.

Nimesimama hapa kuomba nafasi ya Ushika Fedha. Waheshimiwa Wajumbe na Mhe. Naibu Spika, naomba nyote mutambue nafasi hii ya Ushika Fedha ninaiweza na pesa zenu zitakuwa zipo salama. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nina sifa tatu. Ya kwanza, ninajiamini. Ya pili, ninapenda sana mashirikiano.

Mhe. Naibu Spika, sina wasi wasi na ninataka nyote mutambue na kujiamini kabisa kwamba *method* nitakayotumia katika kuweka hizi pesa ni *transparency* kwamba, kila mtu atakuwa anajua mapato na matumizi ya pesa za *CPA*.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima kubwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi hili la Tisa wana-Mapinduzi wenzangu, wakwezi na wakulima ninawaombeni kura zenu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba kura zenu zote za 'ndiyo'.

Mhe. Naibu Spika: Maswali Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ninashukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mhe. Hassan Khamis Hafidh, almaarufu mkwezi. Mhe. Hassan, umetuomba kura kwa imani kubwa na mbwembwe nyingi za kujieleza, mimi ninakushukuru sana kwa uzoefu wako wa kujieleza.

Lakini wewe ni sehemu ya muumini ambaye unakataa sana wezi na hapa umeomba nafasi hii ya Mshika Fedha na tunakuona bado ungali kijana, unatuhakikishia vipi katika sura ya uadilifu ya kulinda fedha zetu zitakazoingia kwenye mfuko huu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Ndugu yangu Mwenyekiti wa Vijana wa zamani wa Mkoa wa Kaskazini, Ndugu yangu Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Naibu Spika, kuna neno kalitumia mimi sitaki tena kulitumia siku hizi, lakini hilo neno alilolitumia kama mimi ninawachukia watu wa aina hiyo, ni mtu ninayefaa kushika fedha hizi. Kwa sababu na *method* nitakayotumia nimeisema hapa, ni *method* ya uwazi.

Kwa maana hiyo Mhe. Naibu Spika, Mhe. Miraji, usiwe na wasi wasi, pesa hizi zitakuwa katika mikono salama, kwa sababu mimi ndiye nitakayekuwa bosi wao wote hao, kwa sababu ndiyo nitakuwa mwenye pesa. Kama alivyo Dkt. Khalid Salum Mohamed na mimi ndiyo nitakuwa mwenye pesa za *CPA*; mimi ndiyo bosi.(*Makofi*)

Kama tunavyojua bila ya pesa hakuna kinachoweza kufanyika. Kwa hivyo, naomba nyote muniamini kama anavyoamini Mhe. Miraji Khamis Mussa, munimiminie kura zote za 'ndiyo' ili nishike pesa zenu na mutakuwa munajua kila siku tunachokipata ile *income and expenditure*.

Naomba kuwasilisha Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Naomba kumuuliza mgombea Mshika Fedha wa *CPA,* alivyokuja hapa alijilabu kwa sifa tatu.

Lakini bahati mbaya alitaja mbili, hii ya tatu mbona haijaitaja? Naomba anitajie sifa ya tatu ni ipi?

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe, jimbo lenye Makao Makuu ya Polisi Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, sifa yangu ya tatu mimi ni *DIASPORA*, naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kunipa nafasi hii kumuuliza swali mtarajiwa Mshika Fedha wetu wa *CPA.*

Mhe. Naibu Spika, Mheshimiwa mgombea alipokuwa akijibu swali mwanzo la Mhe. Kwaza, alipokuwa akijibu alisema lugha hiyo hatoitumia tena. Lakini sasa hiyo lugha hiyo hajaitaja hapa. Sasa bora aitaje ili na huko anakwenda asije akaitumia tena.

Sasa nilikuwa ninataka hiyo lugha ambayo ulisema hutoitumia tena ututajie ili tuisikie.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hafidh Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Naomba sana nimshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma, ambae ni mzoefu. Ni kweli Mhe. Miraji, aliniuliza swali nikasema lugha hiyo siitumii tena, anasema ni lugha gani basi itaje.

Unajua mimi nililelewa na bibi na bibi alinifundisha maadili na akaniambia ukigombwa na watu wazima usikie. Sasa Mhe. Naibu Spika, ninapenda nimwambie Mjumbe kwamba hiyo lugha siitaji wala siitaji tena kwa sababu nimegombwa na watu wazima. (*Makofi*)

Sasa nikiitaja itakuwa ninavunja jinsi gani bibi yangu alivyonilea vizuri na kunifundisha maadili mema, ukigombwa na watu wazima usikie. Kwa maana hiyo nimesikia.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Haya Mheshimiwa, omba kura basi.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa naomba kura zenu zote za ndiyo. Ahsanteni.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, uchaguzi unaofuata ni wa wanawake (*CWP*). Kwa hivyo, tutaita majina ya wagombea na tunaanza na Mwenyekiti Dkt. Sira Ubwa Mamboya. Dkt. Sira jieleze.

Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Ndugu nyote muliopo hapa kwa nafasi za Bunge letu hili la Zanzibar au Baraza la Wawakilishi umaarufu. Ninajua muna hamu ya kunisikia sauti yangu, tangu nije hamjanisikia. (*Makofi*)

Kwa hivyo, mimi naitwa Sira Ubwa Mamboya kwa wale wasionifahamu. Nimesimama hapa kwa niaba ya Bunge la Wanawake kugombea nafasi ya Mwenyekiti. Ni matumaini yangu kwamba mutanipa imani hiyo na mutaniamini kuchukua nafasi hii ili niwaongoze wanawake wenzangu katika Bunge hilo. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo naomba kura zenu wanawake wenzangu ili niweze kufanya hiyo kazi. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mwenyekiti. Maswali.

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Maswali.

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Maswali.

Mhe. Maudline Cyrus Castico: Mhe. Naibu Spika, ninataka nimuulize mgombea na ninaamini kabisa ninafahamu ana uzoefu, lakini ninataka anithibitishie tu, huko watu hawa wanakwenda kuzungumza Kiingereza, yeye Kiingereza anakijua?

Mhe. Naibu Spika: Swali sijalisikia. lakini kama umelifahamu mwenyewe umelisikia lijibu.

Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya: Mhe. Naibu Spika, ananiuliza huko ninakokwenda kuzungumza ninakwenda Kiingereza, hicho Kiingereza ninakijua.

Naomba nikuthibitishie kwa sababu nilifanyiwa mafunzo maalum na TAKILUKI (Taasisi ya Kiswahili) kwa lugha ya Kiingereza na walinipa cheti kwamba ninakifahamu Kiingereza. (*Makofi/Kicheko*)

Mhe. Naibu Spika: Tena siyo Kiingereza na lugha nyengine ninavyojua mimi Mheshimiwa anazijua pia. Mheshimiwa, omba kura ya mara ya mwisho.

Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya: Waheshimiwa, Wanawake wenzangu kwa heshima na taadhima naomba kura zetu.

Mhe. Naibu Spika: Haya kakae. Sasa anafuata Mhe. Mwanaasha Khamis Juma Makamu Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Niliyesimama hapa mbele yenu jina langu ni Mwanaasha Khamis Juma Mwakilishi wa Jimbo la Chukwani.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa heshima na taadhima pia ni Mwenyekiti wa Baraza hili la Wawakilishi, kwa heshima na taadhima naomba kura zenu.

Mhe. Naibu Spika: Maswali.

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Maswali.

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Maswali.

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, nenda kakae.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe. Sasa kuna Kamati Tendaji ya *CWP*. Kamati itahitaji watu watatu kama vile *CPA*.

Hapa kuna wagombea wanne. Sasa mgombea wa kwanza ambaye ni kwenye Kamati Tendaji anajitoa, yaani mimi mwenyewe binafsi ninajitoa naacha wagombea wengine watatu. (*Makofi*)

Kwa hivyo, wagombea watatu watakaokuja hapa ni Mhe. Zulfa Mmaka Omar, njoo mbele uombe kura Mheshimiwa.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: *Assalama Alaykum.* Kwa jina naitwa Zulfa Mmaka Omar Mwakilishi wa Vijana Nafasi Maalum za Wanawake.

Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wanawake, kwa heshima na taadhima naomba muniamini munipe kura zetu ili tushirikiane na nyinyi katika kujenga taifa letu hili.

Naomba kura zenu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, omba kura ukakae.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Waheshimiwa, naomba kura zenu zote za ndiyo.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa kwa kura, sauti imeshanikauka. Waheshimiwa, kutakuwa na kuhesabu kura. Kwa hivyo, wale ambao wanataka kwenda wenyewe au kama wana mawakala wao basi ninafikiri kwa utaratibu tulioweka sasa hivi kura zitaanza kwenda kuhesabiwa. *Otherwise,* tutakaa hapa mpaka saa kumi.

Kwa hivyo, naomba kama wale ambao tayari waliokwisha kupigiwa kura waende au watafute mawakala waende wenyewe.
Mhe. Hidaya Ali Makame, jitambulishe na uombe kura.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Assalam Aleykum. Jina langu naitwa Hidaya Ali Makame Mwakilishi Viti Maalum kupitia Vijana Mkoa wa Kaskazini Unguja, lakini pia kupitia wanawake.

Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wanawake wenzangu nyote kwa ujumla naomba kura zenu za ndiyo.

Mhe. Naibu Spika: Maswali.

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Maswali.

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Maswali.

Wajumbe: Maarufu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, omba kura mara ya mwisho.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Waheshimiwa nyote kwa heshima kubwa naomba kura zenu za ndiyo.

Mhe. Naibu Spika: Haya nenda kakae. Waheshimiwa, Mjumbe wa mwisho anaomba Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma. Mheshimiwa, njoo uombe kura.(*Makofi*)

Mheshimiwa, jieleze.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *Assalam Aleykum.* Jina langu naitwa Salha Mohamed Mwinjuma, ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokea Kusini Unguja. Wajumbe wenzangu wanawake kwa heshima na taadhima naomba kura zenu za ndiyo.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, omba kura mara ya mwisho.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Waheshimiwa Wajumbe, wanawake wenzangu kwa heshima na taadhima naomba kura zenu za ndiyo.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante kakae.

Waheshimiwa, sasa tumeshamaliza uchaguzi, kwa hivyo, sasa naomba tutulie tusubiri matokeo. Waheshimiwa Wajumbe, ninakumbusha tena katika *CWP* ya wanawake jina la Mgeni Hassan Juma kajitoa. Kwa hivyo, kuna nafasi tatu na wote wapo watatu muwatilie watatu musibabaishe kura.

Mumeelewa akinamama.

Wajumbe Akinamama: Ndiyo.

Mhe. Naibu Spika: Haya. Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa tayari tumeshapiga kura. Sasa kilichobakia ni kwenda kuhesabiwa kura. Kwa hivyo,

kwa utaratibu kwanza tunaahirisha kidogo baada ya dakika kumi na tano tunarudi tena ndani.

(Saa 8.30 Baraza liliahirishwa kwa muda wa dakika 15 kwenda kuhesabu kura za Wagombea)

MATOKEO YA UCHAGUZI WA WAJUMBE WA CPA NA CWP

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukuwe fursa hii kuwashukuru sana wale wote ambao walikuwa katika shughuli hii ya uchaguzi wasaidizi wetu. Lakini vile vile kwa kutuletea sasa matokeo ya uchaguzi huo. Kwa hivyo, sasa hivi nitasoma matokeo yote ambayo yako mbele yetu na nitaanza kwanza na matokeo ya *CPA*, halafu baadae nitakuja na matokeo ya *CWP*.

Sasa kwa kuanza tu nitaanza kinyume nyume, yaani tulianza na Mwenyekiti. *(Makofi)*

Tutaanza na nafasi ya Mweka Hazina, ndio maana ya kusema kinyume nyume, halafu tutakwenda kwa Kamati Tendaji, na mwisho nitamtaja Mwenyekiti, ambaye ameshinda. Kwa hivyo, kwa nafasi ya Mweka Hazina kwa *CPA* ambayo ilikuwa na mgombea mmoja.

Waheshimiwa Wajumbe, waliopiga kura wote ni 60, kura zilizoharibika ni 2, kura zilizomkubali Mhe. Hassan Khamis Hafidh, 52 na kura zilizomkataa Mhe. Hassa Khamis Hafidh, ni kura 5. Kwa hivyo, namtangaza mshindi Mhe. Hassan Khamis Hafidh, kwa kura 52. *(Makofi)*

Sasa nitawataja Kamati Tendaji ambayo ilikuwa na wagombea 6, na nitataja kura za wagombea wote. Tunaanza na Mhe. Yussuf Hassan Iddi, ambaye amepata kura 17, wajumbe waliopiga kura wote ni 60, kura zilizoharibika ni 1. Tuna mgombea mwengine Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame, amepata kura 44, waliopiga kura wote ni 60, kura iliyoharibika ni 1, Mgombea mwengine ni Mhe. Dk. Makame Ali Ussi, amepata kura 14, waliopiga kura ni 60, kura iliyoharibika ni 1. Mgombea mwengine ni Mhe. Hamida Abdalla Issa, waliopiga kura wote ni 60, amepata kura 30. Mgombea mwengine ni Mhe. Abdalla Maulid Diwani, waliopiga kura 60, iliyoharibika kura 1, amepata kura 35, na Mgombea mwengine ni Mhe. Hamza Hassan Juma, waliopiga kura 60, amepata kura 38. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo washindi wa Kamati Tendaji au wajumbe ambao wataingia kwenye Kamati Tendaji watatu, ni Dk. Mwinyihaji Makame, Mhe. Hamza Hassan Juma, na Mhe. Abdalla Maulid Diwani *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, sasa tunakwenda kwenye kura za Makamu Mwenyekiti, Mhe. Nadir Abdul-Latif. Kura zilizopigwa ni 59, kura zilizoharibika ni 1, kura zilizomkubali Mhe. Nadir Abdul-Latif ni 49, kura zilizomkataa ni 9. Kwa hivyo, ninamtangaza Mhe. Nadir Abdul-Latif, kwa kuwa alikuwa mgombea pekee na kura alizopata zinatosha kuwa Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nafasi ya Uwenyekiti, waliopiga kura wajumbe wote ni 61, kura zilizoharibika ni 1, kura zilizomkubali Mhe. Simai Mohammed Said, ni kura 53, kura zilizomkataa ni kura 7. Kwa maana hiyo Mwenyekiti wa *CPA* kutoka Baraza la Wawakilishi ni Mhe. Simai Mohammed Said. *(Makofi)*

Wajumbe, walioshinda baadae nitawapa fursa ya kusimama na kutoa shukrani.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa haya ni matokeo ya *CWP*, nitaanza na wajumbe ambao wamegombea nafasi ya Kamati Tendaji nao ni wajumbe watatu. Mhe. Zulfa Mmaka Omar, amepata kura 21, hakuna kura iliyoharibika, kura iliyomkataa ni 1. Mhe. Hidaya Ali Makame, kapata kura 22 zote hakuna iliyomkataa. Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma, kapata kura 21, kura 1 imemkataa. Kwa hivyo, Kamati Tendaji ya *CWP* wajumbe wake watakuwa Mhe. Zulfa Mmaka Omar, Mhe. Hidaya Ali Makame na Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, sasa ni kwa ajili ya Makamu Mwenyekiti, ambapo kulikuwa na mgombea mmoja naye ni Mhe. Mwanaasha Khamis Juma. Wajumbe waliopiga kura ni 20, kura zilizoharibika ni 2, kura zilizomkubali ni 18, kura zilizomkataa hakuna kabisa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nafasi ya Mwenyekiti mgombea ni Dk. Sira Ubwa Mamboya, waliopiga kura ni 24, kura zilizoharibika ni 1, kura zilizomkubali ni 22, kura zilizomkataa ni 1. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kwa hivyo, kwa ufupi hayo ndio matokeo ya uchaguzi wetu wa leo. Mimi niwapongeze sana wale waliopata ushindi, lakini vile vile wale ambao hawakupata ushindi niwapongeze kwa ujasiri wao wa kuingia ndani ya mchakato huu. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, labda niwape nafasi kidogo wale ambao wameshinda kuwashukuruni kwa kura zenu, halafu

baadae tutaahirisha kikao hadi kesho. Dakika moja moja tu. Naanza na Mwenyekiti wa *CPA*, dakika moja hapo hapo katika nafasi yako.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Nichukuwe fursa hii kwanza kwa sekunde chache kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwako wewe pamoja na Spika wetu wa Baraza la Wawakilishi, lakini pia kwa watendaji wote kwa kusimamia uchaguzi wetu ambao ulikuwa huru, haki na umekwenda kwa muda ambao umepangwa.

Lakini pia nichukuwe fursa hii kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri, pamoja na ma-*back benchers* wenzangu niseme kwamba ahsanteni sana, niahidi tu moja kwa moja ushirikiano wangu kama nilivyouonesha ndani ya Baraza, naahidi kama nilivyosema awali kwamba tutaendelea kushirikiana kwa pamoja, pamoja na ofisi yako Mhe. Naibu Spika, na Mhe. Spika, ili kujenga tawi letu imara. Niseme tu kwa kuwapongeza wajumbe wetu Makamu Mwenyekiti, Mhe. Nadil Abdul-Latif, wajumbe wetu Mhe. Abdalla Diwani na rafiki yangu mpenzi Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame pamoja na Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa niaba yao pia natoa shukrani zao za dhati, lakini nafikiria na wao pengine watapata fursa ya kutoa shukrani. Kwa hayo machache, ahsanteni sana, nimefurahi sana na ninawashukuruni sana *God bless you. Thank you*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Makamu Mwenyekiti, Mhe. Nadir Abdul-Latif.

Mhe. Nadir Abdul-Latif: Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nitaanza na *Alhamdulillah Rabil Alamin*, namshukuru *Allah Subhanahu Wataallah,* kwa kuniwezesha na kuwapa hekima Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote kunichagua mimi katika nafasi hii, na kuweza kufuata demokrasia.

Mhe. Naibu Spika, wale wajumbe waliokuwa hawajanipa namshukuru Mwenyezi Mungu, awape moyo mzuri na afya na wale walionichagua nawashukuru sana, nawaahidi tutafanyakazi nao pamoja. Pia, nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Chaani kwa kuniamini na kuweza kupata nafasi hii kwa mara ya pili, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Sasa Kamati Tendaji tunaanza na Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku ya leo tukaweza kumaliza salama uchaguzi wetu na kuwa miongoni mwa waliochaguliwa kuwakilisha

kitengo hiki. Kwa hivyo, mimi nawashukuru wote nawaambia ahsanteni sana kwa kunikopesha imani zenu na kuwalipa matendo, ahsanteni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Mhe. Hamza Hassan Juma, simuoni, lakini nadhani na yeye anawashukuru hivyo hivyo. Kwa hivyo, tunaendelea na Mhe. Mwinyihaji Makame.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, na mimi nachukua fursa hii kukushukuruni nyoote kwa kunipa ushindi wa kishindo, na nipo tayari kuwatumikia kwa faida ya tawi letu hili kuliendeleza mbele. Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuruni ahsanteni sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe, kwanza na mimi nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya na uwezo. Lakini pia kukushukuru wewe kwa kuendesha uchaguzi na kunitangaza mimi mshindi. *(Makofi)*

Mhe.Naibu Spika, tatu, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wote wa Baraza lako tukufu la Tisa, kwa kunichagua kuwa mshindi katika nafasi ya Muweka Hazina wa *CPA* wa Baraza hili la Tisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyojieleza kwamba fedha za *CPA* zitakuwa salama na kila mtu atajua tunachokipata na tunachotumia, kwani huu ndio uleo. Baada ya hayo machache naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, tunakwenda kwenye upande wa *CWP*, Mwenyekiti Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya.

Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe, niwashukuru na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza letu hili kwa kunipa imani, kwamba niwe kiongozi wao katika kuwaongoza wanawake katika jambo hili ambalo mmenikabidhi. Nitawatumikia kwa kadri ya uwezo wangu kama vile imani mliyonionesha na nitafanya vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Sasa ni zamu ya Makamu Mwenyekiti, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa na mimi niseme namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo

hapa, lakini pia niwashukuru wanawake wote walionipa kura kwa kuniamini, nawaahidi kuwa tutashirikiana na Mwenyekiti katika kufanyakazi kwa pamoja, lakini pia naomba mashirikiano kama mlivyotuonesha imani zenu katika kutuchagua, basi nawahakikishia tutawatetea wanawake katika Bunge hili. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Sasa Kamati Tendaji ya *CWP*, Mhe. Zulfa Mmaka, kweli aliniomba kwamba ana dharura na kwa hiyo, ameondoka. Sasa ni zamu ya Mhe. Hidaya Ali Makame.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa kutujaalia imani wanawake sote kwa kuweza kuungana na mimi mkanipa kura zote za ndio, nawashukuru sana na Mwenyezi Mungu atujaalie imani zaidi kwa sote na tuwe tuna mashirikiano zaidi kwa hapa mwanzo na katikati na mwisho wa hili. Ahsanteni sana nawashukuruni nyote, kwa pamoja nawaomba mashirikiano sana, ahsanteni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma.

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kabla ya yote kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia afya na uzima na kuweza kushirikiana pamoja.

Pili, niwashukuru wajumbe wenzangu hasa wanawake, kwa mashirikiano na kuwa na upendo ambao wamenionesha katika uchaguzi huu. Nawaahidi mashirikiano, tutashirikiana ili tuweze kutekeleza majukumu yetu. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Waheshimiwa Wajumbe, na mimi nichukuwe fursa hii kuwapongeza wale wote ambao wameshinda, na basi tuwaombee kheri na wao waweze kutuongoza katika masuala ambayo yanahusiana na haya ambayo wamechaguliwa ya *CPA* na *CWP*, na wawe Wawakilishi wetu wazuri katika shughuli ambazo zitakuwa zinawahusu.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kumaliza kikao chetu hiki cha leo, nina taarifa ndogo inayohusiana na suala la semina. Nakumbuka tulitoa taarifa kwamba kutakuwa na semina, lakini kutokana na muda uliobakia, semina ile imeahirishwa itafanyika tena kesho, kuhusu saa mtakuja kuambiwa kesho asubuhi. Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana kwa utulivu wenu. Naahirisha kikao hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 9:25 mchana kikao kiliahirishwa mpaka tarehe 02/12/2016 saa 3:00 za asubuhi)